**22 JUNI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

__________

## MAJADILIANO YA BUNGE

__________

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Arobaini na Tisa – Tarehe 22 Juni, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wa Saba, Kikao cha Arobaini na Tisa.

Katibu tuendelee na ratiba.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na maswali, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, aulize swali lake.

Na. 429

### Ukosefu wa mabweni katika Shule ya Sekondari ya Bulamata

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha za kujenga mabweni katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Bulamata?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya mahitaji ya mabweni, hasa kwenye maeneo yenye changamoto ya umbali kwa wanafunzi. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika imetenga kiasi cha shilingi milioni 50 katika bajeti ya Mwaka 2022/2023 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa bweni moja Shule ya Sekondari Bulamata ambapo bweni hilo lilijengwa kwa nguvu za wananchi mpaka hatua ya msingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Moshi Kakoso.

**MHE. MOSI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ilishatenga shilingi milioni 50 na wananchi wamejitolea kwa nguvu zao, wamefyatua tofali takriban milioni moja kwa kata nzima.

Je, Serikali imejipanga vipi kuwasaidia, kuwaunga mkono ili waweze kukamilisha mabweni hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Shule ya Bulamata watoto wanaosoma wanasoma takriban kilometa tano mpaka zaidi ya kilometa tano kuifikia shule hiyo.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni wakati muafaka wa kuwasaidia hawa vijana kupeleka fedha na kuwasaidia gari ambalo litakuwepo pale kwenye hiyo shule ili liweze kusaidia huduma kwenye emeo la shule?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwaunga mkono wananchi katika jimbo lake, ni kwamba jambo hilo Serikali tunalifanya. Moja katika hatia ya kwanza ni tuliwaagiza Halmashauri kutenga fedha za ndani, lakini na sisi, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutatafuta fedha kwenye vyanzo vingine ili tuweze kuongeza na kuwasaidia wananchi hao ambao wamejitahidi kwenye ujenzi wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo ni sawasawa tu na swali lake la pili la msingi, kwamba tutatafuta fedha ili tuweze kuongeza na kumalizia shule yao na hayo mabweni, ili sasa watoto waanze kusoma kutokana na umbali huo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** nimemuona Mheshimiwa Minza Mnyika.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuuliza swali; je, ni lini Serikali itajenga mabweni katika Shule ya Kimali Sekondari, Wilayani Meatu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Minza Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatafuta fedha, na kwa sababu tuna miradi mingi katika Idara ya Elimu basi tutalipa kipaumbele katika fedha ambazo zinakuja kutoka kwenye wafadhili mbalimbali, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nimemuona Mheshimiwa Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Jimboni Kibaha kwenye Kata ya Kwara na Magindu kuna mabweni mawili-mawili kila shule ya sekondari yaliyojengwa kuanzia mwaka 2018 hadi 2019 ambayo hayajakamilika na mabweni haya yangekamilika yangewasaidia watoto wanaotokea katika Kijiji cha Dutumi na Kijiji cha Lukenge ambao ni umbali wa karibu kilometa kumi kila kimoja.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutuongezea fedha ili kukamilisha majengo yale ili watoto wayatumie?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti,

naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika bajeti yetu tumetenga fedha kwa ajili ya kumalizia baadhi ya mabweni ambayo yalijengwa katika *EP4R* Awamu ya Saba na Awamu ya Nane ambayo yalikuwa katika mwaka 2017/2018 katika bajeti kuu, kuhakikisha tunamalizia ili mabweni yale yaanze kutumika yakiwemo ya jimboni kwake. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang.

Na. 430

**Ahadi ya ujenzi wa barabara - Katesh**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza: -

Je, Serikali itaanza lini kutekeleza ahadi ya Makamu wa Rais ya ujenzi wa barabara za ndani kwa kilomita 10 katika Mji wa Katesh?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa ahadi hii ambapo katika bajeti ya mwaka 2021/2022 ujenzi wa

kilomita moja ya barabara ya Mkapa imetengewa shilingi milioni 499.99. Ujenzi umeanza tarehe 14 Machi, 2022 unatarajia kukamilika tarehe 9 Novemba, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza ujenzi kwa kiwango cha lami kilomita moja kwa barabara za Gadafi, Joel Bendera na barabara ya Stendi. Serikali itaendelea kutekeleza ahadi hiyo ya kujenga barabara za Mji wa Katesh ili kuinua hadhi ya mji huo na maisha ya wananchi kwa ujumla kulingana na upatikanaji wa Fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Samwel Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; kwa kuwa, ahadi hii ni ya muda mrefu toka 2005 na utekelezaji wake tukienda hivi utachelewa sana na tumeleta maombi maalum Wizarani.

Je, Serikali ina kauli gani juu ya maombi maalum tuliyoleta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mji wa Basutu ni Makao Makuu ya Tarafa ya Basutu n ani mji ambao una wananchi wengi sana.

Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha ili kujenga barabara chache za lami ndani ya mji huo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali haya Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maombi maalum ambayo tayari yamefika Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tupo kuyafanyia kazi. Kwa sababu unapoleta maombi na sisi tunatafuta fedha na tutakavyopata maana yake tutatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali la pili, kuhusu Mji wa Basutu, na lenyewe tumelipokea na tutaliweka katika mipango yetu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo, nimekuona.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wetu wamekuwa wakitoa ahadi kwa wananchi kwa ajili ya matengenezo ya barabara, na Rais wetu wa Awamu ya Tano alitoa ahadi ya kutengeneza barabara Kabia ile Kata ya Ishozi kuja mpaka njia panda ya Gera ambayo inasimamiwa na *TARURA*, lakini mpaka leo barabara hiyo haijatengenezwa ambayo imekuwa ni maswali mengi kwa wananchi na kuona kwamba, ahadi za viongozi hazitekelezwi.

Je, ni lini sasa barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami, ili sasa wananchi waweze kupita katika barabara hiyo kwa urahisi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, ahadi za viongozi zote zipo katika mipango yetu na kila ahadi ambayo inatolewa lazima tutafute fedha ili utekelezaji wake uwepo. Kwa hiyo, waondoe shaka wananchi, tutatekeleza ahadi hiyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, nimekuona.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niwashukuru sana TAMISEMI kwa kazi nzuri wanayoifanya, swali langu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayotoka Kata ya Burungwa – Kinamapula pamoja na Ngokolo mpaka Makao Makuu ya Halmashauri ya Ushetu pamoja na barabara ya kutoka Burungwa – Sabasabini – Ifunde inayounganisha Manispaa ya Ushetu na Manispaa ya Kahama; ni lini sasa zitafanyiwa marekebisho hizi barabara kwa sababu, mpaka sasa hazipitiki kabisa kwa wananchi wa Jimbo la Ushetu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba bahati nzuei katika eneo lake la Halmashauri ya Ushetu tumeanza utekelezaji wa barabara kwa kiwango cha

lami. Na sisi tutakachokifanya tu ni kuongeza fedha kwa maana ya bajeti katika eneo lake ili barabara alizozitaja ziweze kutekelezeka. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Salome utamalizia.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi za Tabora mjini zimeharibika, hasa hizi za pembezoni zikiwemo Kata za Ng'ambo, Kidongo Chekundu, pamoja na Kata za Mwinyi na nyingine. Lini Serikali itatoa fedha za ukarabati, hata kwa kukarabati kwa kutumia changarawe na *moram?*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe hofu na yeye, kwamba bahati nzuri sehemu ya baadhi ya barabara ambazo ameziainisha hapa zimetengewa fedha katika bajeti yetu na zitatekelezwa katika mwaka wa fedha unaokuja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Na mimi naomba niulize swali dogo la nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara iliyoko katika Jimbo la Shinyanga Mjini, Kata ya Ibadakuli, inayounganisha Kijiji cha Garamba ni mbovu sana kiasi kwamba ikifika wakati wa mvua watoto wanapata tabu hata ya kwenda shule. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, inatengeneza barabara ile kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Kijiji cha Garamba?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Salome Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachozungumza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, mipango ya Serikali ni kuhakikisha barabara zote ambazo zinasumbua zinatengenezwa kwa wakati. Kwa hiyo sasahivi jukumu letu ni, moja tumetenga katika vipaumbele, lakini la pili, tunatafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji. Kwa hiyo, tutatekeleza pia barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya nilikuona.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mapera kuelekea Kambarage tumeleta maombi ya dharura kutokana na mvua zilizokwisha ilitengeneza korongo kubwa sana.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili tukakarabati eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya Halmashauri ya Mbinga yamefika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nay apo katika hatua za mwisho za utekelezaji wa hili jambo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la mwisho kwa Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 431

**Hitaji la gari la wagonjwa Hospitali za Wilaya za Liwale, Nachingwea na Kilwa**

**MHE. TECLA M. UNGELE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia magari ya wagonjwa Hospitali za Wilaya za Liwale, Nachingwea na Kilwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 itanunua magari 195 ya kubebea wagonjwa ambayo yatapelekwa kwenye halmashauri 184 nchini kote zikiwemo Halmashauri za Wilaya za Liwale, Nachingwea na Kilwa. Asante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tecla, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi una maeneo mengi sana yaliyoko mbali na hospitali za Wilaya yakiwepo Kilimarondo kule Nachingwea, Nanjilinji Kilwa, Milola kule Mchinga; je, Serikali itatupa kipaumbele kutupatia magari hayo yaliyoongezwa katika maeneo hayo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari haya yatakayoletwa kuna halmashauri zitapata magari zaidi ya moja. Sababu ya halmashauri hizo kupata magari zaidi ya moja itakuwa ni kukidhi vigezo vya kitaalamu, ikiwemo umbali kutoka kituo hicho kwenda kituo kingine cha jirani, lakini pia *population* ya eneo hilo pamoja na mazingira ya kijiografia. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Ungele kwamba, tutafanya tathmini kwa Halmashauri hizo alizozitaja ili kuona kama zinakidhi vigezo hivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu nimekuona.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Simiyu muda mrefu hatuna gari la kukusanya damu salama; je, ni lini Serikali itatununulia gari la kukusanya damu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari katika hospitali za rufaa za mikoa yanaratibiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, lakini kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Afya. Kwa hiyo, kwa sababu hospitali hii iko chini ya Wizara ya Afya tutawasiliana na Wizara ya Afya ili tuone uwezekano wa kupata gari hilo kwa ajili ya huduma za damu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga nimekuona.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka magari ya wagonjwa katika Jimbo la Mbulu Mji na Mbulu Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, magari mawili yatanunuliwa na kupelekwa Halmashauri ya Mbulu Mjini na Mbulu Vijijini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka nimekuona na Mheshimiwa Agness wa mwisho.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi niulize swali la nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uhitaji mkubwa wa gari la wagonjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale lakini tunayo shida kubwa ya magari ya chanjo. Watoto sasahivi ni miaka miwili hawapati chanjo kwa sababu ya ukosefu wa gari; je, Serikali haioni umuhimu wa kutupatia gari kwa ajili ya chanjo za watoto?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na magari 195 ya wagonjwa Serikali itanunua magari mengine 204 kwa ajili ya shughuli za usimamizi, lakini pia shughuli za chanjo. Kwa hiyo pamoja na halmashauri zote kupata magari ya wagonjwa kutakuwa na gari jingine ambalo litakuwa kwa ajili ya shughuli za usimamizi na shughuli za chanjo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa

Kuchauka kwamba, gari hilo pia litakuja sambamba na gari la wagonjwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Likombe kilichopo Mtwara ndicho pia kinatumika kama hospitali ya Wilaya kwa sababu katika Wilaya hiyo hakuna hpspitali ya Wilaya;

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la wagonjwa kwa sababu kuna wagonjwa wengi hasa akinamama wanaotaka kujifungua?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Kituo cha Afya cha Likombe kina-*serve* kama hospitali ya halmashauri kwa sababu hatuna hospitali ya manispaa. Hata hivyo, nimhakikishie kwamba Manispaa ya Mtwara ni moja ya halmashauri zitakazopata gari la wagonjwa. Kwa hiyo nimuelekeze mkurugenzi kuhakikisha unazingatia vigezo ikiwezekana wapeleke gari hili katika kituo hiki kwa kadiri ya vigezo ambavyo vimewekwa na Serikali. ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Nawashukuru Naibu Mawaziri wote wawili kwa kutoa majibu mafupi yanayoeleweka. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, sasa aulize swali lake.

Na. 432

**Mpango wa Umeme Jazilizi**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, mafanikio gani yamepatikana kupitia mpango wa umeme jazilizi na lini Kituo cha kupooza umeme cha Uhuru kitafanya kazi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwaza Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora una jumla ya vitongoji 122 vilivyonufaika na mradi wa umeme jazilizi *(densification)* ambapo kati ya hivyo, vitongoji 27 vipo katika Jimbo la Urambo. Mradi huu wa umeme jazilizi unatarajia kuunganisha umeme katika majengo, makazi, na shule 7,209 ambapo kati ya hayo, 1,722 yapo katika Jimbo la Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Kupooza Umeme cha Uhuru kipo kwenye mradi wa kuunganisha umeme wa Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Kigoma ambapo katika mradi huo, njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Kidahwe Mkoani Kigoma itajengwa. Mradi huo utahusisha pia ujenzi wa vituo vitatu vya kupooza umeme msongo wa kilovoti 132 kuja 33 vya Urambo, Nguruka na Kidahwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(The National Grid Stabilization Projects)* imetenga

jumla ya Shilingi bilioni 24 katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya kujenga njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Urambo yenye urefu wa kilometa 115, na kukamilisha kituo cha kupooza umeme cha Urambo kilichoko Uhuru. Hivyo, kituo cha Kupooza Umeme cha Uhuru kitaanza kufanya kazi mwezi Juni, 2023 ambapo inatarajiwa kuwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Urambo itakuwa imekamilika, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza: Kwa kuwa ujenzi wa kituo hiki cha umeme umesimama kuanzia mwezi wa Tano mwaka 2022, na kwa taarifa tuliyonayo ni kwamba nguzo zitakazotumika ni za zege: Je, kwanini Serikali isitumie zile nguzo ambazo zimetupwa tangu mwaka 2020 mwezi wa Tano, zitumike kueneza au kusambaza umeme katika maeneo mengine kuliko kuachwa kama zilivyo porini na hata pengine kuzihatarisha na moto na kadhalika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi ambao nguzo hizo za zege zitakazopita wanadai fidia; je, ni lini wananchi hawa watalipwa ili na wenyewe wajiendeleze kiuchumi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Margaret Sitta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba *design* ya awali ilikuwa inatumia nguzo za miti, lakini baada ya maboresho imeonekana ni vema kubadilisha *design* hiyo na hivyo tutatumia nguzo nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimwambie Mheshimiwa Margaret, hizi nguzo tutazitumia kwa kadri ya mahitaji. Vile vile nguzo za kupeleka umeme zinatofautiana kulingana na mahitaji. Zile tulizopeleka kule ni za kupeleka msongo mkubwa wa kilovoti 132, ziko zile za msongo wa kilovoti 33 na ziko zile za *distribution* za kwenye maeneo yetu ya msongo wa kilovoti 400. Kwa hiyo hizi zilizoko kule tukizipeleka kusafirisha na kusambaza umeme kwa wananchi, tutakuwa tunatumia *resource* kubwa katika maeneo ambayo siyo yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutapata nguzo nyingine kwa ajili ya kuwapelekea wananchi na hizi zitafanya kazi katika maeneo mengine ambapo zinatakiwa kufanya kazi bila kuathiri mahitaji yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, nadhani wiki hii kabla haijaisha, wale wataalam ambao walikuwa wanafanya *survey* kwa ajili ya kulipa *compansation,* wataanza kuonyesha yale majedwali ya wale wanufaika wa *compansation* kwa wananchi ili waweze ku-*verify* na kuona kama ndiyo stahiki na baada ya hapo sasa itarudishwa Wizarani kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kusainiwa na kurekebisha upungufu utakaojitokeza. Tunaamini kwamba katika muda mfupi ujao wa mwezi mmoja au miwili basi fidia zitaanza kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Margaret Sitta awaambie wananchi wawe tayari, wiki hii au mwanzoni mwa wiki inayokuja kwenda kukagua zile fidia ambazo wameandaliwa kwa ajili ya kuhakiki ubora wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, nimekuona.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba mradi wa umeme jazilizi kwa kiasi kikubwa sana umefanikiwa, lakini kuna changamoto za upatikanaji wa fedha ili kukamilisha maeneo mengi zikiwemo Kata za Rwanima, Mahina Fumagila pamoja na Kishiri.

Ni lini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha fedha nyingi zinapatikana ili mradi jazilizi uoneshe maana halisi ya kujaziliza kwenye maeneo ambayo hayajapata umeme mpaka leo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mabula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Mabula ananufaika na mradi unaoitwa *Peri-urban* ambao unapeleka umeme katika maeneo ya miji lakini yenye asili ya vijiji. Katika mwaka wa fedha unaokuja imetengwa pesa na eneo lake ni mojawapo ambalo litapelekewa umeme wa kuongezea kwenye yale maeneo ambayo bado hayajapatiwa umeme. Nimwahidi tu kwamba Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan imejikimu na kuamua kupeleka umeme katika kila eneo na pesa imetengwa ya kuanzia itapatikana katika mwaka huu wa fedha unaokuja, na muda sio mrefu ataona wakandarasi wakiwa *site*. Pia ziko jitihada za ziada za kuendelea kutafuta pesa kwa ajili ya kufikisha kwenye maeneo yote ambayo tunayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah Lemburis, nimekuona

**MHE. NOAH L. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwamba Halmashauri ya *Arusha DC* inadai fidia ya umeme wa *line* kubwa inayokwenda Namanga, ni lini sasa Serikali itakamilisha ahadi hii, kwa sababu Halmashauri nyingine zote zimelipwa, imebaki tu Halmashauri *Arusha DC*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lemburis Noah Saputi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mradi mkubwa anaosema ulikuwa unatoa umeme Iringa kupita Dodoma - Singida kwenda Arusha mpaka Namanga, na kuna maeneo ambayo tayari fidia ilishafanyika. Yalibakia yale maeneo machache ambayo yalikuwa yana matatizo na kutoeleweka kwa nani alipwe fidia au pengine fidia ilitakiwa ilipwe Serikali, wamepewa maeneo mbadala ili wajengewe majengo. Jambo hili tumekubaliana Wizarani kwamba kabla mwaka huu haujaisha, basi yale maeneo ambayo tayari fidia zilishaanza kulipwa yakamilike na pale ambapo pana changamoto kubwa, tujue namna ya kuitatua.

Kwa hiyo, namwahidi kwamba jambo hili tunalifanyia kazi na tutalikamilisha katika muda mfupi ujao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi aulize swali lake.

No. 433

**Makocha wa Tanzania kutofundisha nje ya nchi**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Je, kwa nini Makocha wa Mpira wa Miguu Tanzania hawafundishi nje ya nchi hata katika Ukanda wa Afrika Mashariki au Nchi za *SADC*?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Tanzania ina makocha 19 wenye viwango vya *CAF A Diploma* ambao wanakidhi viwango vya kufundisha nje ya nchi. Hata hivyo, makocha hawa hawafanikiwi kupata fursa za kufundisha nje ya nchi kutokana na historia ya elimu walizonazo. Hivyo basi, Wizara kwa kushirikiana na *TFF* wanaratibu mpango wa kutoa mafunzo ya Ukocha kwa wanafunzi wa vyuo vinavyotoa mafunzo ya michezo ikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Butimba na Vyuo Vikuu nchini ili kupata Makocha wenye sifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Antipas.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, hao makocha ambao amewataja, wamesoma Leseni A ya *CAF* mwaka 2016, mpaka leo *TFF* haijawapatia vyeti vyao, hali ambayo inawakwamisha kutafuta ajira nje ya nchi. Je, ni lini watapewa vyeti vyao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Ni utamaduni wa nchi yetu kulinda ajira za ndani dhidi ya wageni mpaka pale itakapothibitika taaluma hiyo haipo hapa ndani. Hapa tuna makocha wengi ambao wapo mtaani hawana kazi, lakini wageni wamekuwa wakija kwa wingi sana kufundisha vilabu vyetu hata vile vya daraja la kwanza. Wenzetu wa Zambia na Namibia wameweka utaratibu kuwalinda makocha wazawa kwa maana ya kwamba, kufundisha ligi kuu ya kwao, mpaka uwe umefundisha timu ya Taifa huko ulikotoka: Je, Serikali ya Tanzania ina mpango gani kulinda walimu wa mpira wa ndani?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Antipas Zeno, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mheshimiwa Antipas amependa kufahamu hatima ya makocha hawa ambao walipewa mafunzo mwaka 2016 chini ya *TFF* pamoja na *CAF*. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba jambo hili limekuwa likifuatiliwa kwa karibu na wenzetu wa *TFF,* na bahati nzuri miongoni mwa watu ambao walikuwa kwenye mafunzo haya ni pamoja na Katibu Mkuu wa *TFF* Kidau na jambo hili wamekuwa wakiwasiliana ni jinsi gani walimalize ili hawa makocha waweze kupata haki yao.

Swali la pili, alipenda kufahamu mkakati wa Serikali wa kuweza kuwalinda makocha wa ndani kwa sababu sasa tumeshaanza kuwazalisha. Sisi kama Wizara tunafahamu kwamba vijana wetu wanapokuwa na sifa lazima tuwalinde. Tuna mkakati wa Wizara yetu wa kukuza michezo wa mwaka 2021 mpaka 2031, miongoni mwa vitu ambavyo tunakwenda

kuzingatia ni kuhakikisha tunatoa kozi kwa makocha wetu. Ndiyo maana hata sasa kozi inaendelea, zaidi ya nchi tatu zinashiriki. Watakapofuzu vijana zaidi ya 20 wa Kitanzania, maana yake wataendelea kupewa fursa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq nimekuona na Mheshimiwa Ndulane pia.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali la nyongeza. Nilipenda kufahamu: Nini mkakati wa Serikali wa kuwaandaa makocha wengi wanawake ili waweze kufanya ukocha hapa nchini na nje ya nchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati tuliyonayo pia ni kuhakikisha kwenye ile michezo yetu ya kipaumbele kwa Wizara ambayo tuna michezo sita ya kipaumbele kwa Taifa ni pamoja na kuhakikisha pia tunapata makocha wanawake. Kwa hiyo, jambo hili Mheshimiwa Toufiq tunalizingatia pia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba kuuliza swali baada ya swali namba 431 la msingi kuulizwa, siyo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Tumeona michezo mbalimbali ya wanawake wanafika mbele wanaenda hadi Kombe la Dunia: Ni nini mkakati sasa wa Serikali kuhakikisha kwamba michezo yote; *Volleyball, Basketball* na michezo mingine tunapata makocha wanawake ambao wanaweza wakazi-*train* hizi timu ili ziweze kufika mbali zaidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu tumedhamiria kwa dhati kuhakikisha kwamba tunanyanyua vipaji vya wanawake wa Kitanzania. Vile vile kwenye michezo ya kipaumbele mchezo wa mpira wa miguu wanawake upo na mchezo wa mpira wa pete upo. Kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha walimu wa michezo hiyo wanatokana na wanawake wenyewe. Mheshimiwa Grace utuamini, tunaendelea na kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali lingine kwa Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde, aulize swali lake.

Na. 434

**ZFA kupata uanachama wa FIFA**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza:-

Je, Serikali inaisaidiaje Zanzibar kupata faida ambazo *TFF* inazipata katika kuendeleza soka la Tanzania?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TFF* imeendelea kuhakikisha kuwa Zanzibar inanufaika na fedha za misaada kutoka *FIFA* ambapo hadi sasa miradi kadhaa ya kuendeleza soka imetekelezwa ikiwa ni pamoja na kusaidia timu za Taifa, mashindano ya ndani, mawasiliano na mafunzo kwa wadau wa michezo. Hata hivyo, Serikali inatambua changamoto zilizopo baina ya *TFF* na *ZFF* katika uendeshaji soka katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua changamoto hizi, Wizara yetu pamoja na Wizara ya Michezo na Vijana Zanzibar zimeitisha kikao maalumu baina ya *ZFF* na *TFF* kwa lengo la kutatua changamoto hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, swali la nyongeza

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza, kwa kuwa suala la michezo siyo suala la Muungano; na Zanzibar imekosa kuwa mwanachama kwa sababu ya Tanzania tayari ni mwanachama: Je, ni lini sasa *TFF* itabadili jina badala ya kuwa *Tanzania Football Federation* iwe *Tanzania Bara Football Federation* ili kuipa nafasi Zanzibar kuwa mwanachama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama hilo haliwezekani, basi ni lini Serikali itaunda *MOU* ili kuipa faida za kuwa mwanachama wa *FIFA* Zanzibar kisheria? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu swali la pili.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba kujibu swali la pili la Mheshimiwa Mohamed Saidi Issa, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu langu la msingi nimeeleza kwamba ni kweli sisi Wizara yetu tunakiri kuna changamoto kupitia *ZFF* pamoja na *TFF*. Waziri wetu Mheshimiwa Mchengerwa ameshakutana na Mheshimiwa Waziri wa Zanzibar wa Michezo, dada yangu Mheshimiwa Tabia wamezungumza, na hivi karibuni baada ya Bunge, tutakutana na vyombo hivi viwili; *ZFF* pamoja na *TFF* ili tuweke *MOU* ya pamoja kuona jinsi gani Zanzibar pia inafaidika na mgao wa fedha za *FIFA*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimemwona Mheshimiwa Prof. Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Soka la Wanawake Tanzania limetuletea heshima kubwa sana. Mbali ya kwamba hatuna makocha, lakini pia hatuna waamuzi uwanjani kwenye soka la akina mama.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha tunapata waamuzi akina mama ili wasaidie katika soka hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Prof. Ndakidemi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la soka la wanawake kwetu sisi ni kipaumbele. Nawapongeza wanawake wote Tanzania kwa jinsi ambavyo wamemwelewa Mheshimiwa Rais wetu Mama

Samia Suluhu Hassan kwamba tunahitaji kushiriki na kushinda. Suala la makocha pamoja na ma-*referee* liko kwenye mpango kazi wetu kuhakikisha kwamba tunakuwa na ma-*referee* pia wa kutosha.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Madini, tunaenda na Mheshimiwa Ndaisaba George Luhoro, Mbunge wa Ngara, aulize swali lake.

Na. 435

**Wananchi wa Ngara kunufaika na uchimbaji wa madini ya *Nickel***

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Ngara wananufaika na uchimbaji wa madini ya *Nickel*?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Madini.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Jimbo la Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa madini ya *Nickel* katika eneo la Kabanga unafanywa na Kampuni ya *Tembo Nickel Corporation Limited* iliyopewa leseni mnamo tarehe 25 Oktoba, 2021. Mradi huo unatarajiwa kuchangia ushuru wa huduma kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kiasi cha dola za Marekani milioni 65, sawa na takribani shilingi bilioni 151 kwa

kipindi cha uhai wa mgodi huo. Aidha, mradi huo unatarajia kutoa ajira za moja kwa moja 978 kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2022 mradi ulikuwa umetumia jumla ya dola za Marekani milioni 1.5 katika ununuzi wa bidhaa na huduma ndani ya nchi. Kati ya hizo, Dola 125,673 zilitumika kufanya ununuzi katika Wilaya ya Ngara**.** Hivyo, nitoe rai kwa wananchi wa Wilaya ya Ngara na Taifa kwa ujumla kuchangamkia fursa zilizopo katika mradi huo. Aidha, kupitia Sheria ya Wajibu wa Makampuni kwa Jamii (*Cooperate Social Responsibility - CSR),* mradi huo ulichangia takribani Shilingi milioni 39 kwa mwaka 2021 na unatarajiwa kuchangia jumla kiasi cha shilingi milioni 207.8 mwaka huu 2022, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa ilitokea katika historia ya Nchi yetu Tanzania ikatawaliwa na wakoloni na kwa kuwa wakoloni hawa walifanya tafiti mbalimbali za madini hapa nchini, sambamba na kuchimba madini hayo.

Je, ni lini Wizara ya Madini itawaomba wakoloni hawa waje kufunga mashimo waliyoyaacha kwa maana ya kufanya *mining closure*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; naomba kujua kama Wizara ya Madini wanazo tafiti zilizoachwa na wakoloni ili waweze kuziweka wazi kwa Watanzania ili waweze kuwekeza kwenye madini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la kwanza, kuhusu wakoloni ambao walifanya tafiti, wakachimba madini na wakaacha mashimo na yeye kutaka kujua mpango wa haya mashimo kuja kufungwa, nipende kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, wakoloni wa Kijerumani ambao walifanya utafiti mkubwa wa madini ya makaa ya mawe na hata dhahabu katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwepo kule Ngara na maeneo ya Sekenke Singida waliondoka kabla hawajayamaliza madini katika machimbo hayo, hivyo hawakuhangaika kuyafunga na mashimo haya yamekuwa msaada kwetu katika kuendeleza tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengine leseni zimeshatolewa na mashimo haya yamekuwa yakitoa mwongozo wa kubaini madini yaliyopo ili tuendelee kuyavuna na hivyo basi kwa ajili ya jibu la swali lake hilo pia kwa kipengele cha hayo mashimo, wale waliopewa leseni sasa kulingana na Sheria yetu ya Madini, Sura ya 125 ndio wamepewa wajibu wa kuandaa *closure plan,* mpango wa ufungaji wa mgodi kulingana na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 ambao unamtaka mwenye mgodi aweke utaratibu wa jinsi atakavyorejesha ile ardhi katika hali yake salama baada ya mradi kumaliza uhai wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la pili, hizo takwimu za tafiti zilizofanywa na wakoloni tutazipataje. Kwa bahati nzuri wajerumani walivyofanya tafiti za madini katika nchi hii kuanzia mwaka 1925, waliacha takwimu za kutosha, *data* zipo katika *archives* zetu katika taasisi yetu ya *GST* hapa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuibua hilo swali ili nitumie fursa hii kutoa rai kwa Watanzania wanaopenda kufanya biashara za madini kwamba tunazo *data* za tangu enzi za ukoloni mwaka 1925, waje wazifuatilie kule, maktaba ipo na wanaweza wakapata taarifa za kijiolojia za kuwaongoza katika kwenda kuendeleza kwenye uchimbaji wa madini husika katika maeneo yaliyofanyiwa utafiti. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, nimekuona.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali sasa itawaangalia wachimbaji wadogo wa Mkoa wa Njombe ambao walishaomba leseni za kuchimba makaa ya mawe kule Ludewa na Wizara imeshawaahidi na wakaunda vikundi, lini watawapa leseni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna wachimbaji wengi nchini ambao wameomba leseni za uchimbaji na bado hawajapata na hasa wa jimbo lake ambapo kuna maeneo ya machimbo ya makaa ya mawe ambayo yapo katika eneo linalomilikiwa na Taasisi nyingine ya umma ya *NDC*. Kwa sababu ya utaratibu kwamba yale maeneo yana wamiliki wengine sisi tukitoa leseni ni lazima wale waliopewa leseni wakaombe mwenye *surface right* kuingia katika uchimbaji na mchakato wa kuwasaidia wachimbaji wadogo ili wapate maeneo ya kuchimba ni moja ya dhamana tuliyopewa sisi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nimwahidi tu Mbunge kwamba baada ya Bunge hili mwezi Julai, mimi binafsi nitafika katika maeneo hayo yenye wachimbaji ambao wamepata leseni au wanaomba leseni hawajapata, tujue changamoto zinazowakabili ili tuzitatue na waweze kupata maeneo maana ni dhamira yetu kwamba wachimbaji wadogo wapewe maeneo ya kuchimba ili wapate tija kutokana na rasilimali madini yaliyopo katika nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Wizara ya Madini kwa majibu hayo ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, sasa aulize swali lake.

Na. 436

**Ujenzi wa VETA – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Meatu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Ujenzi wa Vyuo vya *VETA* kwa awamu katika mikoa na wilaya mbalimbali kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika kipindi ambacho Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Meatu, wananchi wa Meatu wanashauriwa kutumia Vyuo vingine vya *VETA* na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo kwa ajili ya kupata elimu ya mafunzo ya ufundi, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jeremiah Komanya, swali la Nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa Serikali imetenga fedha ya kujenga *VETA* katika bajeti inayoanza Julai, imetenga fedha ya kujenga *VETA* 36.

Je, Serikali inaweza ikawaambia nini vijana wa Meatu ambao tayari wameshaandaa eneo la kujenga *VETA*?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoanza kueleza kwenye majibu ya msingi kwamba Serikali ina sera ya kujenga chuo katika kila wilaya nchini. Katika bajeti yetu ya Serikali ni kweli tumetenga zaidi ya shilingi bilioni mia moja kwa ajili ya ujenzi wa vyuo 36 au vyuo katika wilaya 36 nchini. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwa vile tutaweka vigezo vya namna gani zile Wilaya 36 tunakwenda kuzipata na kwenda kufanya ujenzi na kwa vile ujenzi unafanyika kwa awamu, nimhakikishie tu na niwahakikishie

wananchi wa Meatu katika mgao huo ujao tuwahakikishie kwamba na wao Wilaya ya Meatu tutaweza kuzingatia ili tuweze kupata chuo katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakuona Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nataka kuuliza Je, Serikali katika hivyo vyuo 36 itakavyojenga na Wilaya ya Ubungo nayo imo katika orodha hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ambazo hazina vyuo hadi hivi sasa ni Wilaya 62 na katika bajeti yetu ijayo Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi katika Wilaya 36, ni ukweli usiokuwa na shaka kwamba siyo wilaya zote zitakazoweza kupata kwa hiyo tunaweka vigezo na vielelezo vya *demand analysis* ili kuhakikisha yale maeneo yenye uhitaji mkubwa ndio tunaweza kujenga kwanza halafu vingine tutakwenda kujenga katika mwaka ujao wa fedha, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Siha ina vijana wengi sana ambao hawajapata nafasi ya kuendelea na masomo ya juu.

Je, Serikali ina mpango gani katika hivi vyuo 36 na yenyewe kupata nafasi ya kujenga Chuo cha *VETA*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Mbunge Viti wa Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwamba ujenzi huo unakwenda kwa awamu, kwa hiyo kuna maeneo tutayafikia na kwa vile tutaweka vigezo, cha msingi tutaangalia ule uhitaji mkubwa katika maeneo tutakayoyaainisha. Kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwenye hili, kwa vile Wilaya ya Siha ina uhitaji mkubwa na vijana pale ni wengi kwa vyovyote vile Wilaya ya Siha tutaipa kipaumbele, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Juma Othuman Hija, Mbunge wa Tumbatu, aulize swali lake.

Na. 437

**Benki Kuu kufikia lengo la kutoa mikopo kwa sekta binafsi**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Je, ni kwa kiasi gani lengo la Benki Kuu la kutoa mikopo kwa sekta binafsi limefikiwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Fedha ya Mwaka 2021/2022, imeainisha shabaha ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 10.6 ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa gharama nafuu na kuongeza ukwasi katika uchumi. Kutokana na utekelezaji wa sera hiyo, kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kimeendelea kuongezeka kufikia wastani wa asilimia 8.4 katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuanzia mwezi Desemba, 2021, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa zaidi ya asilimia 10 ambapo mwezi Aprili, 2022, ukuaji huu ulifikia asilimia 13.4. Kutokana na mwenendo huu ni matarajio yetu kuwa, lengo la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi la asilimia 10.6 kwa mwaka 2021/2022 litafikiwa na hivyo kuchangia uwekezaji, uzalishaji na kuongeza ajira nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Othman Hija.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto zinazoikabili mtaji wa sekta binafsi ni viwango vya riba katika benki zetu. Je, Serikali ina mpango gani kudhibiti viwango hivi vya riba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilishatoa trilioni moja kwa benki ili kutoa mikopo hasa ya kilimo kwa riba nafuu, isiyozidi asilimia 10 na zipo Benki zetu kama vile *CRDB, NMB* katika dirisha la kilimo wapo na single *digit*. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imezingatia na itaendelea kuangalia viwango vya riba kulingana na hali ya uchumi nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Juma na Mheshimiwa Paresso ajiandae.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Benki Kuu ya Tanzania ndio *custodian* wa waendesha biashara za benki nchini Tanzania.

Je, ni lini Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania itachukua hatua ya kuwafidia waliokuwa wateja wa *SBNE* pamoja na wafanyakazi kuwalipa haki zao kama vile inavyofanya SMZ - Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imewalipa wateja wa *Master Life* waliopata kadhia kama hiyo? Sasa Serikali hii yetu ya Tanzanzania itafanya nini na kwa nini haiwapi taarifa wananchi kuhusu kadhia hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali moja katika hayo mawili unaloona wewe sawa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mshua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua mbalimbali kutoa fidia kwa wale waathirika wa benki kama zilivyotokea wakati huo na bado Serikali ipo inafanya upembuzi, fedha itakapojitosheleza na kujiridhisha Serikali itatoa fidia kwa wananchi wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Tunatambua kwamba kuna mwongozo ambao umetolewa na Wizara ya fedha ku-*regulate* riba kwenye *microfinace* hapa nchini, lakini mwongozo huo haufuatwi na hizo taasisi za kutoa fedha wakati mwingine zinachukua hadi kadi za *ATM* za watumishi wanaokwenda kukopa pale, Serikali inasema nini juu ya hili ili miongozo hiyo iweze kufuatwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali siku zote inafuata miongozo na taratibu ambazo zimewekwa, kama zipo changamoto ambazo ameziona acha tuzichukue twende tukajadili, tuangalie, tukijiridhisha basi tutazifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia Wizara ya mwisho ambayo ni Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 438

**Kujenga Bwawa la Yongoma – Same**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kujenga Bwawa la Yongoma ambalo lilifanyiwa michoro ya awali mwaka 1984?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, usanifu na uandaaji wa michoro ya awali ya Bwawa la Yongoma ulifanyika mwaka 1984 na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani *(JICA)*. Bwawa hili litakapokamilika litaweza kuhudumia wananchi katika Vijiji vya Misufini, Ndungu, Makokane na Mpirani. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Same ipo katika hatua ya awali ya kufanya mapitio ya upembuzi yanikifu na usanifu wa Bwawa la Yongoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa mapitio hayo, ujenzi wa bwawa hili utawekwa katika mpango wa ujenzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha Skimu za Umwagiliaji za Same ambapo kwa sasa imepeleka mitambo katika Skimu ya Ndungu kwa ajili ya kufanya ukarabati wa dharura. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina swali la nyongeza; kwa kuwa Bwawa la Kalemawe lililopo Jimbo la Same Mashariki lililojengwa na wakoloni mwaka 1958/1959 limejaa tope sana na hili lilikuwa linasaidia sana wakulima wa kata ya Kalemawe, Kihurio na Bendera. Je, Serikali ina mpango gani kusaidia kutoa tope hilo ili ikusanye maji ya kuweza kusaidia kwenye kilimo cha umwagiliaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaelekeza timu ya wataalam waende kuangalia eneo hilo ili wapate tathmini halisi na baadaye waweze kufanya utekelezaji katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya nimekuona.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Katika Jimbo la Manyoni Mashariki tuna Bwawa la Mbwasa ambalo tayari upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulishafanyika. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu lini itaanza ujenzi wa bwawa hilo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Mbwasa liliwekwa katika mpango kupitia Benki ya *BADEA* na hivi sasa tunajiandaa kwa ajili ya ujenzi wa bwawa lenyewe, lakini vile vile na skimu za umwagiliaji katika bajeti ya fedha ya mwaka 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, nimekuona.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Waziri kutembelea Jimbo la Kalenga ambalo najua Waziri ataifanya, lakini napenda kujua ni lini sasa atatupa fedha za haraka angalau turekebishe Bwawa la Wellu katika Kata ya Ruanda ili lisaidie wananchi pale katika kilimo cha umwagiliaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaelekeza timu ya wataalam kufika katika eneo husika, mimi mwenyewe pia nitafika, ili tuone hali halisi na tuone namna ya kuweza kuwakwamua wananchi katika eneo hilo kwa sababu tumejipanga kuhakikisha kwamba sekta hii ya umwagiliaji inachukua hasa kipaumbele katika bajeti yetu inayokuja. Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mimi mwenyewe nitafika na wataalam watafika kuoa namna ya kuweza kuwa-*rescue* wananchi katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Saashisha, nimewaona.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Jimbo la Ndanda tuna skimu mbili za umwagiliaji ambazo ni Mkwera, Kata ya Nanganga pamoja na Skimu ya Ndanda, skimu hizi ziko kama zimekuwa *abandoned,* sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ya uwekezaji mkubwa ambao ulifanyika pale, nini malengo ya Serikali na skimu hizi mbili ili ziweze kufanya kazi iliyokusudiwa vizuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya kazi kubwa ambayo tumeipa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ni kuhakikisha inapitia miradi yote ya umwagiliaji nchini Tanzania kwa maana ya kufahamu *status* zake, tujue ipi inafanya kazi, ipi imekwama na ipi inahitaji namna gani iweze kutoka hapo ilipo iendelee kufanya kazi. Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo dhamira yetu kuiacha na kui-*abandon* miradi hiyo mikubwa ya umwagiliaji, tutaifanyia kazi kuhakikisha kwamba inafanya kazi ili tutimize lengo la kuwa na eneo kubwa la umwagiliaji hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Bolutu lililopo Kata ya Masama Magharibi lilifanyiwa tathmini na kugunduliwa lina maji

mengi sana, lakini Bwawa la Kikafuchini kwa Tito na lenyewe lina maji ya kutosha.

Je, Serikali ni lini itajenga mabwawa haya ili yaweze kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Hai?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea rai ya Mheshimiwa Mbunge, tutajielekeza katika eneo hilo sisi na wataalam wetu kuona namna ambavyo tunaweza tukayafanya mabwawa hayo yatumike kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na wananchi waweze kunufaika. Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, maelekezo yangu ni kwamba mtaalam wetu wa pale Mkoa wa Kilimanjaro atafika kwa ajili ya kuangalia na kufanya tathmini na baadae tufanye utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umefikia mwisho, niwapongeze kwa jitihada nzuri mnazozifanya za kuuliza maswali mafupi ya Kibunge. Mmeona leo muda wa saa moja tumeuliza maswali mengi sana, kwa hiyo endeleeni hivyohivyo. Pia nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, nao majibu yao ni mafupi na yanayoeleweka. Kwa hiyo, tuendelee hivyo ili Bunge letu liwe zuri na la maana zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninawatangaza wageni ambao wamekuja kwenye Bunge letu asubuhi hii.

Kuna wageni ambao wako kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika ambao ni wageni 30 wa Bunge kutoka Shirika la *Henry Jackson Foundation Medical Research International (HJFMRI)* maarufu kama *Water Reed Program* wanaotekeleza afua za kupambana na maambukizi ya VVU. Wageni hao wameongozwa na Ndugu Kimberly Bohince ambaye ni Mkurugenzi wa Afya wa Shirika la *Henry Jackson Foundation Medical Research International (HJFMRI)* duniani kutoka Marekani. Naomba asimame tumuone, karibu. *(Makofi)*

Mwingine ni Ndugu Sally Chalamila ambaye ni Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la *Henry Jackson Foundation Medical Research International (HJFMRI)* hapa Tanzania. Hawapo katika hao ninaowataja?

Ndugu David Maganga, *Chief of Party* wa Mradi wa Nyanda za Kusini, karibu. Dkt. Magnus Ndolichimpa, *Chief of Party* wa Mradi wa Shirika la *Henry Jackson Foundation Medical Research International (HJFMRI)* anayehudumia Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania, karibu sana wageni wetu. *(Makofi)*

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambaye ni Ndugu Alma Agapinus Tax, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Liaoning Petrochemical cha nchini China, karibu sana mgeni wa Waziri wetu wa Ulinzi. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wapo hapa Bungeni waliotembelea kwa siku ya leo, naomba wote wasimame kwa pamoja. Karibuni sana katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsanteni na karibuni. *(Makofi)*

Tuna wageni pia ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao waimbaji 32 wa Kwaya ya Mwangaza kutoka Kisaki - Mkoani Singida Mjini, karibuni sana waimbaji wetu wa kwaya kutoka Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 120 na walimu saba wa Shule ya Msingi Martin Luther kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi 40 wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi wa Kata ya Nkuhungu - Dodoma. Vijana hawa wako wapi? Naona hawajaingia, labda wataingia baadae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo matangazo yetu kwa asubuhi hii. Katibu, tuendelee.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu. Tutaanza na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge wajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa mara nyingine tena, kwa namna ambavyo aliweza kuunda Wizara ya wanawake, jinsi na watu ambao hawajiwezi, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Nimesimama hapa kuomba kuongezewa fedha kwenye asilimia 10. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Kaka yangu, 'Kalumbu' ulikuwepo nilipochangia hapa kwamba ninaomba sana ile asilimia 10 niliyoiweka kwa ajili ya kusaidia, asilimia Nne wanawake, asilimia Nne vijana na asilimia Mbili watu wenye ulemavu. Niliomba sana kwa dhati ya moyo wangu, kwamba wanawake wana majukumu mazito sana. Majukumu mazito kwa maana ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wewe naamini ni shahidi, mtoto akizaliwa wa kike kitu cha kwanza unamuita mama, umekuja, unamfurahia unamuita mama. Tayari ameshajiunganisha kwenye majukumu, nilitegemea hapa ombi langu la kuongezewa asilimia nyingine badala ya asilimia 10 waweke 15 ambapo asilimia tisa iende kwa wanawake kulingana na majukumu yao, kwenye asilimia hizo ni kwa sababu wanawake hao ndiyo hao hao wajasiriamali, ndiyo hao hao machinga, ndio haohao ambao wanatunza familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri anavyokuja hapa kuhitimisha alichukulie uzito sana suala la wanawake. Wanawake wana majukumu mazito. Vijana hapa ambapo wanakuwa wanapata hiyo mikopo, akipata tatizo wa kwanza kuhangaika ni mwanamke ambaye ni ama mama yake au dada yake, lakini hatamwambia kwamba naomba fedha ya kukuuguza hospitali, hatamwambia hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa kilio cha Wabunge wote amekisikia, kuhusu kutokuondoa asilimia tano kwenye asilimia 10. Naomba iongezeke, badala ya asilimia 10 iongezeke iwe asilimia 15, Tisa kwa wanawake, Tatu kwa vijana, Tatu kwa watu wenye ulemavu kulingana na majukumu waliyonayo wanawake. Hata mabinti hawa niliomba kwamba mpaka sasa hivi kwa sababu ni wanawake wameshaunganishwa huko, wanakopa fedha kupitia Mfuko huo wa Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru sana endapo hapa Mheshimiwa Waziri atalisemea hili, kwamba amebadilisha msemo wake ule wa kuondoa hata asilimia tano, bali ataongeza asilimia nyingine tano ili asilimia tisa iende kwa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Tanzania hasa wanawake wa Mkoa wa Mbeya Wilaya za Kyela, Rungwe, Mbarali, Chunya, Mbeya Mjini na Mbeya Vijijini, wanawake wajane wa Taifa hili wanasumbuliwa sana. Ninaomba sana kwenye hili Serikali iwaone wanawake. Wanapokuja kuhitimisha ninatamani kama inawezekana ile sheria ya kusema mama anapofiwa na mume anasumbuliwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hapa juzi, imenipasa nirudie kwa sababu baada ya mchango ule nilipotoka nje hapa kumbe kulikuwa na wageni wengi sana wanawake na kati ya wale wengi sana walikuwa ni wajane. Walijitokeza wanawake kuja kunisalimia na kunishukuru sana juzi nilivyowasemea wanawake wajane wa Tanzania hii. Mama mmoja nilipata uchungu sana, kati ya wale wanawake waliokuja kunishukuru, wanawake Wanne walikuwa na kesi Mahakamani za kudhulumiwa zao. Mmoja akaniambia, Mheshimiwa naomba samahani namba yako ya simu, mimi mume wangu nimeishi nae miaka 16 lakini amefariki, kesi ninayo Mahakamani. Baada ya kufariki anakuja Baba yake mdogo anasema mimi hii nyumba

lazima iwe mali yangu niimiliki kwa sababu mume wako mimi ndiye liyemtafutia kazi! Ni uonevu wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ichukulie kwa uzito kilio cha wanawake Tanzania nzima, hasa Mkoa wa Mbeya. Wanawake wengi sana hata kabla ya nafasi hii mimi kuwa Mbunge, walikuwa wakija kulia getini kwangu wakiniomba msaada, nilikuwa nikiwasaidia ili wapate haki zao waweze kusaidia watoto wao na familia zao. Nitashukuru sana kama nimeeleweka juu ya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili jambo la *TCRA*. Kwenye Nchi yetu ya Tanzania tumeendelea sana kwa mawasiliano. Sasa hivi mfanyabiashara anakuwa yuko Mbeya, ameingia mteja dukani anahitaji kifaa yeye hana, anapiga simu dukani, anapiga simu Dar es Salaam anakipiga picha anauliza kama kifaa hicho kipo. Ni ndani ya dakika moja jawabu limepatikana na anaweza kukiuza kifaa kile. Mtu anasafiri anaweza akawa yuko Uturuki, anapiga picha vitu ambavyo amevikuta, mali mpya kule Uturuki, anauliza huku maduka ya Dar es Salaam; Je, nikileta hivi ili tuweze kuuza, je tutauza? Ndani ya dakika moja jibu vinapatikana, lete kwa wingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vifungu wanavyosema viondolewe kwenye *TCRA,* hivyo vifungu vitaturudisha nyuma, mawasiliano yatapotea, yataisha, tutarudi nyuma. Ishu ya kidigitali hii itakuwa ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake tumeingia kwenye mfumo wa kidigitali lakini matokeo yake tunaambiwa kwamba hivi vifungu viondolewe; *TCRA* watakuwepo kama nani, watakuwa wanafanya shughuli gani? Tutakuwa tumewaondolea kufanya kazi watu wa *TCRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui mlikaa na *TCRA* lini na wapi mkafikia mwafaka wa haya, lakini kwa vifungu vya sheria jinsi ambavyo tumevichanganua haitawezekana *TCRA* ikafanya kazi kwa ufanisi endapo vifungu hivi vitaondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano sasa hivi kwa jinsi ambavyo yamekuwa yametuletea, wakati fulani unaweza ukawa una mawazo yako, una mambo mengi kichwani kulingana na hali ya maisha, lakini wakati mwingine unaona kwamba hebu nishike hii simu nijaribu kupata furaha yangu. Ukishika simu utacheka wakati umekasirika, utapata furaha pale, utapunguza *stress,* utapunguza maradhi, utatoa sumu ya mawazo kwenye mwili wako kwa kucheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunakotaka kwenda, tukitoa vifungu hivi vya *TCRA,* vifungu vya sheria, tunakwenda kupoteana. Tutarudi kulekule, ukitaka kufungua mtandao ndiyo ukae baada ya siku moja, mbili au tatu, hatupendi Watanzania turudi nyuma, tunahitaji tusonge mbele kwa ajili ya maendelea ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, kulikuwa na kilio kikubwa sana cha wazabuni ambao ni ma-*supplier* Serikalini, wengine walikuwa wanadai madeni ya hata miaka 20 iliyopita, lakini Mheshimiwa Rais, Mama Samia, baada ya kuliona hili alituma fedha na baadhi yao walipunguziwa mzigo, nadhani yuko kwenye mchakato, ataendelea nalo hili. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa haya anayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Watumishi wa Serikali ni wazembe, wanatengeneza madeni wao wenyewe kwa uzembe wao. Baadhi yao wanafanya kazi nzuri, baadhi yao ni wazembe wanaiangusha Serikali. Fedha zinakuwepo kwenye akaunti, wanaagiza vifaa kwa *supplier,* akishaagiza fedha zipo

lakini anafanya uzembe wa kumlipa *supplier,* mwisho wa siku zile fedha unaingia mwaka mpya wa Serikali zinavutwa zinakwenda Hazina, kuja kurudi ni ndoto. Hilo linakuwa linaunda madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan nilimsikia hapa akisema Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu, alieleza kwamba wameacha utaratibu kuanzia sasa hakutakuwa na kurudishwa fedha. Fedha zilizoingizwa kwenye Halmashauri zetu, zilizoingizwa Serikalini kwa ajili ya kazi, zitabaki huko bila kurudi kule Hazina. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ameondoa kilio cha wafanyabiashara walio wengi ndani ya hii nchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Suma muda wako umekwisha, kengele ilishagonga, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mjitahidi sana kutumia dakika zenu Kumi kwa yale mambo muhimu ambayo mnayaona ili Wabunge wengi wapate kuchangia. Tunaendelea na Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya, Mheshimiwa Ally Kassinge na Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro wajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia katika Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutambua jitihada za Serikali katika kuongeza bajeti katika sekta za uzalishaji. Jambo ambalo Wabunge wote tumelifurahia, kwamba kuongeza bajeti katika sekta za uzalishaji kwa maana ya kilimo, mifugo na uvuvi, tunakwenda kufanya uzalishaji mkubwa. Na kama tija ambayo tumeiongea sana katika Bunge hili itatokea, basi tunakwenda kujikwamua mahali pakubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipende kupongeza jitihada na hatua ya Serikali ambayo imetambua kwamba kuna sababu kubwa na ya msingi ya kuziba mianya ya upotevu wa fedha katika matumizi ya Serikali. Jambo la kwanza, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipendekeza juu ya hasara inayopatikana kutokana na watumishi waliopumzishwa majukumu yao. Wabunge wengi wameongelea, na nipende kukumbuka kwamba Mheshimiwa Janejelly alisema kwamba kama Kanuni zetu zinaruhusu basi kweli huo mpango wako uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi ninapenda kusema kwamba, ili Serikali isipate hasara juu ya watumishi hawa ambao wanapumzishwa majukumu yao, basi muda mchache uwekwe baina ya wao kupumzishwa na kurudishwa katika majukumu yao. Serikali ijipe *timeline* ni wiki mbili au mwezi mmoja, mtumishi awe amerudi kufanya majukumu yake, lakini anapokaa mwaka mzima, mtumishi huyu kwanza anakuwa *demoralized* halafu anajisikia ni *reject.* Sasa Serikali inapata hasara hapa, mtumishi yuko *demoralized* hapa kwa sababu hajarejeshwa katika kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili tufunge *loop.* Wakati Serikali haitaki kupata hasara tufunge *loop* upande wa pili mtumishi arudi mapema katika majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika kupunguza matumizi ya Serikali ni kuhusu matumizi ya magari. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri juu ya hili; lakini napenda huku nako tufunge *loop,* kuna *loose loops* hapa mahali pia. Yaani tumeona hasara inayopatikana kwasababu ya wingi wa magari, lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha wale wakala wa kutengeneza haya magari hebu jiulize unao watumishi wa kutosha kule ndani? Kama hawa watumishi hawatoshi wanaotengeneza wanatoka upande gani? Na kwanini usilipe zaidi ya ambavyo unapaswa kulipa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo si ajabu ukakuta; nitoe mfano ambao ni rahisi sana; wote hapa tunajua kuwa *wind screen* ya gari 250,000 lakini inapotoka *voucher TEMESA* unakuta imekuja mara tatu au mara nne zaidi ya hiyo, *wind screen*. Huu nimeutoa mfano ambao ni halisi nimekutana nao. Wote tunajua kwamba *wind screen* ni 250,000 au 300,000 ya *Prado* au *Landcruiser* lakini angalia katika *voucher* zako za matengenezo ya magari yako hutakuta hiyo bei. Mara nyingi utaambiwa 750,000 au 1,000,000. Hapo napo, kwa zile gari ambazo utaamua zibaki kwa wale watendaji wakuu wa Wizara basi hebu funga *loop* upande wa *TEMESA* uone kwamba bei unazoletewa za vipuri vya magari ndizo bei halisi za soko kama ambavyo unatamani pia kupunguza upande wa umma *procurement*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine; Ofisi ya *CAG* imependekezwa kuongezewa watumishi na pia kufanya *technical* pamoja na *financial audit*. Hata hivyo hiyo bado ni *audit*. Mimi ninapendekeza, kwasababu kazi yao ni ku-*audit* na una *audit* na una *audit* kazi iliyokwishafanyika sasa tija itatoka wapi? Mimi nadhani kama tuna mpango wa kunusuru nidhamu ya matumizi bora ya fedha za Serikali basi hawa watu katika hii Ofisi ya *CAG* wapewe pia jukumu la *monitoring and evaluation* pamoja na kufanya *audit*. Wakiendelea kufanya *audit* bado watamkuta mtu ambaye amekwisha kutumia vibaya fedha za Serikali halafu anakuja kuwajibishwa. Sasa, tunapaswa tuzuie matumizi hayo, ambapo ni pamoja na kufanya *monitoring and evaluation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niongelee kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii, na nitambue mchango mzuri kabisa na maono ya Mheshimiwa Rais ambaye kwakweli amekwenda kutanzua kitendawili ambacho mataifa ya nje; watu wengi wanadhani kwamba mataifa ya nje wao ni werevu, lakini kama wangekuwa ni werevu na *atlas* wanazo kwanini kila wakati walipokuwa

wanauliza Mlima Kilimajaro upo wapi wanasema huu upo nchi nyingine. Kwa hiyo, si kwamba lazima wawe werevu, walikuwa ni wajinga. Sasa Mheshimiwa Rais ametusaidia kuwaondolea ujinga waliokuwa nao wa kujua vivutio vipi vipo upande gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kupata tija katika hilo *our hospitality* na *tour guides* wetu wanapaswa kuongezewa uwezo wapenzi. Bado *hospitality* yetu kama nchi haipo *top watch*. Kwa hiyo hili wizara husika na Serikali ikae pamoja ione kwamba tunahitaji ku-*improve* sana upande wa *hospitality* yetu pamoja na *tour guides;* hilo litatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za karibuni tumeona wachezaji wakubwa wa vilabu vikubwa vya Ulaya wakija, na wanakuja Serengeti; lakini hawa pia tunawaona wakati wa mapumziko yao ya wakati wa kiangazi wakienda kupata mapumziko katika fukwe na hasa za Bahari ya *Mediterranean Barbados* pamoja na Dubai. Kwanini sisi, yaani tunajua wanalolitaka tuna joto lote na jua lote na mchanga wote wanaoutaka, kinapungua nini Tanzania? Hatujaweza kuimarisha *beach sports,* maana ndicho wanachokitafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pale Pwani ya Dar es Salaam kuna visiwa vizuri; kwanini Serikali isione kwamba kuna sababu ya ku-*improve* mazingira ya uwepo wa visiwa katika ufukwe wa Dar es Salaam halafu ikaingia pamoja na sekta binafsi ku-*improve beach sports* ili tuwateke waje Serengeti wakimaliza wapumzike pale kwenye beach zetu? Kwa hiyo kuna sababu ya kuanzisha kile wanachokitapata katika Bahari ya *Mediterranean* visiwa vya Ibiza, *Barbados* na Dubai tukilete pale Dar es Salaam ili waweze kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika ku-*improve* habari ya utalii; watu wengi sana tunapokwenda katika miji

unasema kwamba nita *spend* siku moja ya ziada au ya pili kwa ajili ya *shopping* au kwa ajili ya kuangalia mji, lakini miji yetu haijatoa hayo mazingira. Kwa hiyo, watalii wanakuja wanaishia Serengeti wanapanda ndege na kuondoka; na sababu kubwa ni kwasababu hatuna *museums* zinazovutia. Yaani tuna *museum* lakini yawezekana vilivyomo ndani ya *museum* haviwavutii kusema kwamba nita *spend* siku moja Arusha, nita *spend* siku moja Dar es Salaam kwa ajili ya kuangalia, *what's is there to see* hatujaweza kuwapa hicho watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa napendekeza kwamba, mbona Tanzania tunavyo vitu vya kuwapa? Kwa mfano; tumekuwa tukiongea katika hili Bunge juu ya mjusi yule wa Tendaguru aliyoko Ujerumani. Kwani Tendaguru siniyakwetu? na Tendaguru ambayo hamuijui vizuri kijiolojia ni mahali ambapo katika Bara la Afrika ndipo panapoongoza kuwa na masalia ya wale mijusi na viumbe wale wa zamani. Kwa hiyo, haya mabaki yalichimbwa mwaka 1905. Hivi Serikali ilishawahi kuwekeza kiasi kwamba tuone kama tunaweza tukachimba na sasa tukapata mjusi wetu wa kuchimba sisi wenyewe? Maana yule alichimbwa na Wajerumani karne imepita sasa. Kwa hiyo, mimi ninapendekeza Serikali iweke fedha katika utafiti pale Tendaguru ili ikiwezekana watu wetu wa archeology waende pale wajaribu kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kwamba kazi ya kumuunganisha ni kazi kubwa sana lakini tupate na sisi mifupa baadhi baadhi tuiweke katika *museum* yetu. Lakini pia jambo ambalo tunalo la kuvutia zaidi … *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele yako imeshalia ya pili. Ahsante sana, nakushukuru Profesa Shukrani Manya ahsante sana. Mheshimiwa

Ally Kassinge nilimtaja Mhesimiwa Ndaisaba Ruhoro ajiandae na Mheshimiwa Stella Manyanya. *(Kicheko)*

**MHE: ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi asubuhi ya leo ili nami niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha na Mipango inayohusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka uliopita Mpango wa Maendeleo kwa mwaka ujao lakini pia Mpango wa Mapato na Matumizi kwa mwaka ujao wa fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana Wizara ya Fedha kwa kuja na mpango na bajeti ambayo inakwenda kugusa matarajio ya Watanzania. Bajeti ya mwaka huu tutakayoipitisha ni bajeti ambayo imezingatia kwa ukamilifu wake masuala ya maendeleo na ya huduma za jamii pongezi sana Wizara ya Fedha na Mipango. Wakati unatuletea mpango huu pamoja na mambo mengine tulizingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ambao tuliupitisha hapa Bungeni. Mpango huo wa Tatu wa Maendeleo pamoja na mambo mengine ulikuja na mikakati ya kuhakikisha kwamba tunajenga bandari za uvuvi katika maeneo yetu ya mwambao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Serikali kwamba katika eneo hili tumeanza na Kilwa, na ninayoheshima kutoa taarifa kwamba mkataba wa kujenga bandari ya uvuvi pale Kilwa Masoko umesainiwa na tayari mkandarasi wa kutoka China ameanza kuoneshwa eneo la kufanyakazi. Hii ni faraja kubwa sana kwa Tanzania kwa ujumla wake lakini kwawana Kilwa kwa upekee wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo la bandari pamoja na mambo mengine ambayo Wizara ya Uvuvi na Mifugo imejiandaa ninayo ya kupendekeza. Jambo la kwanza ujenzi wa bandari ya uvuvi uendane na uwepo wa miundombinu mingine rafiki au taasisi zingine rafiki zitakazoendosha au zitakazowezesha

bandari ya uvuvi kufanyakazi vizuri. Taasisi au miundombinu hiyo ni pamoja na hizi zifuatazo: -

Jambo la kwanza tunapendekeza chuo cha uvuvi kijengwe pale Kilwa Masoko ili bandari ya uvuvi na masuala ya kuelimisha watu masuala ya uvuvi yawe maeneo hayo hayo ya karibu. *(Makofi)*

Jambo la pili; tunapendekeza kwamba miundombinu ya barabara ya uhakika kutoka Bandarini Kilwa Masoko pale mpaka Nangurukuru kwenye Barabara Kuu *(highway)* ya Dar es Salam mpaka Mikoa ya Kusini ya Lindi Mtwara na Ruvuma iimarishwe ili iendane na mahitaji na kukidhi haja ya bandari ambayo tunakuja kuijenga. *(Makofi)*

Suala la tatu ambalo tunapendekeza; nimepitia mpango wa Wizara ya Uvuvi katika ujenzi wa bandari hii na nimeona kwamba tutajenga Soko la Uvuvi pale Kilwa Masoko. Mapendekezo yangu ni kwamba pale Kilwa Masoko tujenge kituo cha kukusanyia samaki au mazao ya bahari, badala yake soko la samaki likajengwe Kilwa Kivinje ambako kuna fursa za kutosha na kuna wadau wengi wachuuzi wengi, wavuvi wengi pale Kilwa Kivinje ambao ni mji jirani na Kilwa Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne katika mapendekezo haya nipendekeze kwamba Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko uimarishwe na ujengwe katika viwango vya kukidhi matakwa ya kimataifa. Hi ni kwa sababu sasa tunapojenga bandari ya uvuvi maana yake ni kwamba tunakuja kufungua fursa za kimataifa. Hatuwezi kufungua fursa za kimataifa kwa uwanja wa ndege tulionao sasa hivi ambao ni wavumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulikuwa na mpango wa kujenga uwanja huu wa ndege kwa kiwango cha changarawe. Uwanja huu unamita 1,800, Serikali imeweka

changarawe mita 1,000 tu bado mita 800. Sasa niseme kwamba mita 800 zile zimaliziwe lakini tuwe na mpango sasa wa kujenga Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tuendane na kwenda kuwalipa fidia. Kulikuwa na mpango wa muda mrefu, na ninaomba niukumbushe hapa; upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko ambapo wakazi wengi maeneo ya mashamba pamoja na nyumba zao zimewekewa alama, kwamba zitabomolewa ili kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege wakalipwa fidia na utekelezaji wa uwanja huu uanze mara moja kadri ambavyo Serikali itakuwa imejipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka kwenye eneo hilo la masuala ya uvuvi na miundombinu yake rafiki nije katika eneo la menejimenti ya utumishi wa umma, usimamizi wa utumishi wa umma. Utumishi wa umma usimamizi wake unaanzia katika mchakato wa ajira mpaka mtumishi anastaafu. Hata hivyo kwa *experience* ambayo imejitokeza tokeza tumeona kwamba watumishi wa umma hawako katika hali ya kufurahi sana; kuanzia ajira zao mpaka ukomo wa ajira wanaishi maisha yaliyo ya mashaka mashaka kutokana kutosimamia vyema eneo hili la utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano eneo la *pension* kwa watumishi wa umma hivi tunavyozungumza bado kuna watumishi hawajalipwa mafao yao ya *pension* ilhali wamestaafu miaka miwili, miaka mitatu bado hawajalipwa. Vilevile kuna eneo la usafirishaji wa mizigo mtumishi baada ya kustaafu. Wapo watumishi wamestaafu miaka mitatu sasa, miaka minne bado hawajalipwa. Niikumbushe Serikali kwamba mwaka 2008, 2009 mpaka 2010 Ofisi ya Rais, Menajimenti ya Utumishi wa Umma ilikuwa na zoezi la kusafisha taarifa za watumishi maarufu kama *data cleaning* ili watumishi wenye sifa waweze kuwepo katika

utumishi na taarifa zao zikawe sawa katika utaratibu wa kimtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dhana hiyohiyo ya kusafisha taarifa za watumishi *data cleaning* niombe sasa Serikali ijisafishe yenyewe kwa kuhakikisha kwamba watumishi hawaidai Serikali yao. Sambamba na hilo kwenye eneo hilo la usimamizi wa menejimenti ya utumishi wa umma nigusie kidogo masuala ya uteuzi na utenguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi katika eneo hili uko wa namna mbili; wapo wanaoteuliwa kupata nafasi za uteuzi ndani ya utumishi wa umma, lakini wapo wanaopata nafasi nje ya utumishi wa umma. Niiombe Serikali kwamba *treatment* za makundi mawili haya zisiwe sawasawa. Kwa vyovyote vile mtumishi wa umma anapoteuliwa kwenye nafasi ya utumishi maana yake ametoka kwenye ajira anakwenda kule kwa mkataba utumishi wake huku haujakoma na sheria ndiyo inaelekeza hivyo tofauti na yule ambayo ameteuliwa nje ya utumishi wa umma ambaye anakwenda kwenye mkataba, ukiisha mkataba wake inakuwa basi atarudi kwenye shughuli ambayo alikuwa akiifanya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtumishi wa umma anapoteuliwa baadaye mkataba wake wa uteuzi au mamlaka ya uteuzi ikasema kwamba sasa inatosha halafu anaachwa arudishwi kwenye majukumu yake hili lazima tulizungumze kwa masikitiko; kwasababu limetokea, watumishi wameathirika sana kisaikolojia na familia zimeathirika. Hata hivyo, nilishukuru sana, dada yangu Jenista alivyoingia tu katika Wizara hii jambo la kwanza kushughulikia ni kurudisha watumishi wote ambao walikuwa na sifa za kurudi kazini; ahsante sana Mheshimiwa Jenista. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika dhana hiyo hiyo ya kufanya *data cleaning,* niiombe Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma, ifanye *data cleaning* kwa kuhakikisha kwamba watumishi waliobakibaki wale waliokuwa *Ma-DAS*, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Wilaya lakini walitoka kwenye utumishi wa umma, mamlaka ya uteuzi ikasema sasa inatosha wapo wachache wamebaki Wizara izingatie ifanye *data cleaning* kuhakikisha wale waliobaki wanarudi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la watumishi walioteuliwa utakapokoma muda wao wa uteuzi kushushwa; hili limezungumzwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba Dkt. katika hotuba yake ya bajeti. Niikumbushe Serikali, kwamba utumishi wa umma unazingatia haya yafuatayo; Sera ya Menejiment na Ajira ya Mwaka 1999, Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2002 na mabadiliko yake, Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, Kanuni za Utendaji Bora, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na miongozo mbalimbali inayoongoza utumishi wa umma. Kama hivyo ndivyo Serikali tunakwama wapi? Sheria hizi, miongozo hii tuliitengeneza wenyewe, tulitunga wenyewe, kwanini hatuzingatii hizi taratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi anapoteuliwa kwenye nafasi ya uteuzi aidha alikuwa afisa daraja la kwanza, afisa mwandamizi, au afisa mkuu, anapopata barua yake ya uteuzi inasema kwamba yahusu kuteuliwa na kupandishwa cheo kuwa... Sasa unapomteua na kumpandisha cheo maana yake ni kwamba unamtoa katika daraja lile na kwa maana hiyo maslahi anayopata ikiwa ni pamoja na mshahara ni kwa sababu ulimteua na kumpandisha cheo. Utumishi au uteuzi wake unapokoma nafasi yake ya kupandishwa cheo ndiyo inayomfanya abaki na mshahara huo wa nafasi aliyoteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kwa dhati kabisa ninapendekeza kwamba watumishi hawa wanaoteuliwa pindi wanapotenguliwa wasishushwe mishahara yao kwa sababu wamepandishwa cheo; na kupandishwa cheo ndugu zangu siyo adhabu, kupandishwa cheo ni tija na ni faraja na niheshima inakuwaje mtu anayepandishwa cheo baadaye unamvunjia ile heshima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri sana Serikali eneo hili mpango wake wa kuwashusha mishahara watumishi waliotumbuliwa isiendelee nao…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele ya pili, ahsante sana nashukuru. Tunaendelea na Ndaisaba Ruhoro, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Jafari Chaurembo, ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa nami ya kuchangia Bajeti ya Serikali. Nipende kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake uliotukuka na maono makubwa aliyonayo kwa ajili ya kuiendeleza Tanzania. Watanzania wote ni mashuhuda na wameona kupitia bajeti iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango. Mheshimiwa Rais wetu ametoa maelekezo na ameelekeza bajeti hii iende kusaidia watanzania wa hali ya chini, na ndiyo maana fedha nyingi imepelekwa kwenye sekta ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu Waziri wake na timu nzima ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa

utumishi wao mzuri ambao umetukuka na kwa kuweza kupokea maono na maelekezo ya Mheshimiwa Rais na kuyatekeleza kwa kiwango cha hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ngara walionichagua kwa imani kubwa sana waliyonayo juu yangu na kwa kunipa ushirikiano mkubwa hasa ninapokuwa natekeleza majukumu ya kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielekeze mchango wangu kwenye eneo la kilimo. Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizojaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na ardhi nzuri, maji pamoja na hali ya hewa inayosapoti kilimo cha kahawa. Matokeo yake, Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa kuweza kuzalisha kahawa bora ndani ya Bara la Afrika ikifuatiwa na nchi ya Ethiopia pamoja na Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya 15 duniani kwa uzalishaji wa kahawa bora kwenye hii dunia. Wanaozalisha kahawa Tanzania ni kaya 450,000 za Watanzania ambazo zinazalisha kahawa asilimia 90 ya kahawa yote inayozalishwa nchini. Kati ya kaya 450,000, kaya 120,000 zinatoka Mkoa wa Kagera na Ngara ikiwemo. Tunazalisha *metric ton* 50,000 kwa wastani kwa mwaka na mwaka tunaofanya vizuri tunazalisha tani 68,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri yote haya, eneo linalotumika kwa kilimo ni hekta za mraba 265,000. Ilitakiwa tutumie hata zaidi ya hekta milioni moja, lakini uzalishaji unaofanyika, unafanyika kwenye eneo dogo ambalo halileti tija kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto kwenye eneo la kahawa hasa kwenye utaratibu mpya wa mnada wa kahawa. Hapo nyuma changamoto ilikuwa ni kubwa sana kwenye soko la

kahawa, lakini nashukuru Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo yaliyopokelewa vizuri na Waziri Mkuu na baadaye kuchagizwa na Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussen Bashe na kuleta utaratibu wa kuuza kahawa kwa njia ya mnada. Nashukuru sana kwa hatua kubwa waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto zinatakiwa kufanyiwa kazi kwa haraka. Moja, kwenye mnada anajitokeza mnunuzi mmoja, matokeo yake anaanza kuringa na kuweka bei anayoitaka. Ngara tumeonja bei nzuri ya kuuza kahawa. Tumeuza kwa mara ya kwanza kilo moja Shilingi 3,740/=, hatuwezi kurudi nyuma kwa sababu bei ya soko la kahawa kwenye dunia iko juu. Nimeshawaeleza wananchi wote wa Jimbo la Ngara na wakulima wa kahawa, kama bei haitashuka kwenye soko la dunia, nasi hatuuzi kahawa yetu kwa bei ya chini, na msimamo ni huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaomba Watanzania wajisimamie, kwa sababu wanapoenda kwenye mnada anatokea mnunuzi mmoja anaweka bei wasiyoitaka. Kahawa siyo nyanya wala vitunguu waka biringani zinazoona. Kahawa zina uwezo wa kukaa muda mrefu, hatuuzi kama mnunuzi hatafika bei. Napenda kuwaomba Watanzania waweze kujisimamia katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango amwezeshe Mheshimiwa Bashe ili aweze kuboresha miundombinu na utaratibu mzima wa kufanya mnada. Kwanza, wakati wa mnada *internet* imekatika zaidi ya mara mbili, matokeo yake wakulima wanashinda pale, wanashindwa kufanya biashara. Ni aibu mtandao kukatika wakati watu wanasubiria kuuza bidhaa zao wapate fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba lifanyiwe kazi ni kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kwa kuhakikisha

vijana wanawezeshwa kuanzisha mashamba mapya kwa sababu mashamba mengi yamezeeka, ni ya muda mrefu, yamepandwa na wazee. Sasa vijana hawana ardhi ya kutosha na mashamba ya kulima. Tuwawezeshe vijana kupata mashamba ili waweze kuanzisha mashamba mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielekee kwenye eneo la miundombinu. Nimeshaeleza, Jimbo la Ngara ni jimbo ambalo liko mpakani na ni jimbo la kimkakati. Jimbo la Ngara linapakana na Rwanda na Burundi na ukitoka Ngara kwenda *DRC Kongo* ni karibu sana. Nimeshaeleza kwamba Ngara hitaji letu kubwa ni miundombinu ya barabara za lami za kisasa. Kuna kipande cha lami kutoka Nyakahula mpaka Rusumo kilomita 92, kama hakitatengenezwa wafanyabiashara wa Rwanda na Burundi watahama kutumia Bandari ya Dar es Salaam, wataenda kutumia Beira, *Mozambique* na watakwenda kutumia Mombasa, Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba sana Wizara ya Fedha na Mipango, tutumie utaratibu ule wa *EPC+F (Engineering, Procurement, Construction plus Financing)* ili tuweze kupata Wakandarasi waje kujenga barabara hiyo. Pia kuna barabara ya kutoka Mrugarama kwenda Rulenge mpaka Kwemubuga kilomita 75. Barabara hii imeahidiwa mfululizo kwa ziadi ya kipindi cha miaka mitano, na Marais wamekuwa wakija na kuahidi. Naomba barabara hii ipatiwe fedha kupitia utaratibu huo wa *EPC+F* iweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara inatoka Mzani inakwenda Kumbuga mpaka Murusagamba kilomita 34. Barabara hiyo inaiunganisha Tanzania na Burundi. Naomba sana Wizara ya Fedha na Mipango toeni fedha kwa Wizara ya Ujenzi ili barabara hii iweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna kipande kidogo cha kilomita 32 kutoka Rulenge kwenda mpaka Tembo *Nickel*. Naomba tena kipande hicho kiweze kujengwa kwa utaratibu huo wa *EPC+F.* Wizara ya Fedha tunaomba muidhinishe *term sheet* zinazoletwa na wawekezaji ili waweze kuleta fedha na waweze kujenga barabara hizi kwa utaratibu wa *EPC+F. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Ngara hitaji letu lingine kubwa ni reli ya kisasa ya *SGR* kutoka Isaka kwenda Rusumo mpaka Rwanda. Nimeona kwenye mpango wa muda mrefu Serikali imeshatusikia na imeweka. Sasa nawaomba Wizara ya Fedha na Mipango waanze sasa kutafakari, kufanya *feasibility study,* kufanya *design* na kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga kipande hiki cha reli kutoka Isaka mpaka Rusomo Irala kuelekea mpaka Rwanda ili kurahisisha biashara mpakani katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende pia kwenye upande wa afya. Serikali imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba inajenga vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo mbalimbali nchini. Nami kwenye Jimbo la Ngara hivi karibuni nimeweza kukamilisha ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya mbalimbali kikiwemo Kituo cha Rusumo, Kigina, Kabulanzimili pamoja na Kihinga. Vituo hivi vya kutolea huduma za afya, havina vitendanishi, havina vifaa tiba, havina watumishi na matokeo yake popo na mende ndiyo wanaotumia hivyo vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Fedha na Mipango, toeni fedha TAMISEMI waweze kuleta watumishi. Toeni fedha waweze kununua vitendanishi na vifaa tiba ili vituo hivi viweze kufanya kazi. Pia tuleteeni watumishi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako naomba dakika moja tu nimalizie eneo la mwisho la kikokotoo kwa sababu eneo hili limeleta kelele sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kikokotoo kwa sasa linaleta *pressure* kubwa sana kwa watumishi wote nchini hasa wale wanaokaribia kustaafu. Watumishi wote Tanzania wana taarifa kwamba mwaka 2023 ndiyo mwisho wa kuahirishwa matumizi ya kikokotoo kilichokuwa kimeletwa na kikapandisha joto hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kila mtumishi ambaye umri wake umekaribia kustaafu wala hasubirii. Muda wake umefika wa kustaafu kwa hiyari, haraka haraka anamtafuta Mbunge, anawasilisha nyaraka zake, anastaafu kukimbia kikokotoo cha mwaka 2023. Naomba kikokotoo hicho ki-*rest in peace* huko huko ambako kilipelekwa, kisirudi tena kwa sababu mpaka sasa kinaleta joto kubwa na *pressure* kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro. Tunaendelea. Nilimtaja Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Jafari Chaurembo, ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nyasa nianze na kumshukuru sana sana sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake yote na kwa bajeti hii inayoongozwa sasa na Mheshimiwa Waziri Mwigulu kwa jinsi ambavyo wameweza kutekeleza shughuli za kimaendeleo katika Jimbo langu la Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi wao kwa kazi zote zinazoendelea. Kwavile siyo rahisi kumshukuru kila mmoja, niseme tu nawashukuru wote waliohusika katika kuleta maendeleo katika Jimbo langu la Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishukuru Serikari kwa kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami, barabara ya kutoka Kitai kwenda Litui hadi Ndumbi. Pia naomba watusaidie juu ya Daraja la Mitomoni ambalo liko katika Mto Ruvuma ambalo kwa kweli limekuwa ni kilio kikubwa kwa wananchi na wananchi wamekuwa wanapata shida wengine kiasi cha kufariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri yalipotokea yale maafa, Serikali ilipeleka timu wakafanya *feasibility study* kiasi kwamba lile daraja sasa liko tayari kwa kuanza kujengwa. Ni imani ya wananchi kwamba daraja hilo litajengwa ili kuondoa adha iliyopo na pia hata hali ya kimawasiliano ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii napenda nizungumzie kama ushauri kwa upande wa Serikali. Serikali imetufundisha jambo moja kubwa sana kupitia mkopo wa masharti nafuu ambao ulilетwa kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa madarasa. Katika hilo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo mkopo huu ulifanyiwa kazi. Fedha iliyotolewa ni Shilingi trilioni 1.3, lakini fedha hii inajulikana na kila Mtanzania, kila mtu anajua kwamba kuna mkopo wa Shilingi trilioni 1.3 umeenda kufanya kazi hii na hii na hii, kiasi kwamba mpaka unaweza kufikiria kwamba ah, hivi ina maana kumbe kwa mwaka mzima yawezekana fedha iliyofanya kazi ni hiyo tu. Kwa sababu zile fedha nyingine tunazokusanya tumeambiwa ni karibu Shilingi trilioni 20 na kitu, hazioneshi moja kwa moja zimeenda katika matumizi yapi? Pamoja na kwamba kweli tunajua zimeenda kwenye wilaya zetu, lakini hazijawekwa kwa uwazi mzuri kama zilivyoweka hizi fedha za *COVID-19*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuona kwamba, kwa kuwa tunafanya hayo makusanyo na tumekuwa tukipeleka fedha huko, basi kila Wizara iwe inatoa orodha ya vitu ambavyo vinaenda kutekelezwa huko kunakotekelezwa, tuweze kuona kabisa Wizara hii ilipata fedha kiasi fulani na zimeenda mahali fulani ili tuweze kusimamia kwa karibu kama ambavyo tulisimamia haya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijaribu kuona kwamba kama shilingi trilioni 1.3 ilifanya kazi kubwa hiyo nchi nzima, haya matrilioni mengine je, ukiondoa ile mishahara ya wafanyakazi na vitu vingine! Tukiamua hata Shilingi trilioni tatu tu hizi kwamba sasa zitaenda kufanya hili na hili, nina uhakika na tukijipangia muda tutaweza kupiga hatua kubwa sana katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ninalopenda kuchangia ni eneo la Wamachinga na ile asilimia 10 iliyozungumzwa kwamba ipunguzwe asilimia tano kwa ajili ya miundombinu. Kwa bahati nzuri eneo hili nimelifanyia kazi kwa kipindi kirefu. Niseme tu kwamba kundi hili la Wamachinga, siyo kwamba Wamachinga ni wale wanaotembea tu. Wamachinga wamekuja kutoa jina hilo kutokana na ule ubunifu wao wa kufanya biashara kiasi kwamba sasa hata wale wajasiriamali wadogo wenye mtaji kuanzia shilingi 1,000 mpaka shilingi milioni 50 wanaangukia katika kundi hilo la Wamachinga. Kimsingi ni wale wajasiriamali wadogo wadogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuzungumza kwamba ipo haja ya kuiga mtindo tunaowafanyia nyuki. Nyuki unamtengenezea mzinga, yeye anakupa asali. Sasa na hawa Wamachinga wanafanya biashara ambazo ukijumlisha katika ile thamani ya kazi wanayofanya ni fedha nyingi sana na wanatengeneza ajira nyingi sana katika nchi yetu. Ila kwa kuwa kundi hili hatujalitambua kikamilifu na kulipa haki kamili ya maeneo ya kufanyia kazi, ndiyo maana wakati mwingine

tunampa *pressure* hata Mheshimiwa Rais, Wamachinga wetu wapate maeneo ya kufanyia kazi; wote tunachangia humo. Leo linapokuja suala la kusema kwamba tuanze sasa kutengeneza mazingira bora ya hawa watu kufanyia kazi, wote tunaruka. Tunasema ah, bora watu wakakopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie ukweli, katika baadhi ya maeneo, hata ufuatiliaji wa hawa watu wanaokopeshwa unakuwa ni mgumu kwa sababu hawajulikani waliko. Unakuta watu wanapewa fedha tu kwenye kikundi wanaganagawana mambo yanakwisha. Imekuwa ni kama fedha za msaada badala ya kuwa ni fedha za kuwawezesha katika masuala ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nasema mimi kama mimi na ninasimama mimi kama mimi. Najua Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa upande tofauti, lakini kazi ya Bunge ni kila mtu anashauri anavyoona. Nasema wazo hili ni zuri sana, isipokuwa tunaweza tukaamua kuanza na maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Jimbo langu la Nyasa natamani liwe mfano, nami naunga mkono asilimia tano ikatengeneze miundombinu na asilimia tano wakopeshwe, na wale watakaokuwa wamekosa, waendelee kwenda benki kwa sababu benki zipo. Benki ya *NMB* ipo, *CRDB* ipo na mabenki mengine yapo. Hayo ndiyo tuwape sasa kazi ile ya kukopesha zaidi. Isitoshe mifumo yetu ya ukopeshaji inabidi na yenyewe itengenezewe utaratibu kama wa kibenki. Kwa sababu sasa hivi hata ukopeshaji wake saa nyingine hata taarifa haziko sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano. Pale kwangu Bambabay palikuwa hapana mazingira mazuri kabisa ya kupata chakula, nikaamua bora nitafute fedha ili waweze kupewa sehemu ya kufanyia kazi. Nikakaa nao, nikawashawishi, tukavunja mabanda yale ya biashara ambayo yalikuwa ya ovyo kabisa.

Baadaye tukajenga mabanda mazuri, sasa hivi kila mtu anaenda pale na shughuli za kibiashara zimekuwa kubwa zinazidi kuongezeka. Huu ni mfano mdogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mialo yetu mingi ni mibaya, ya ovyo kabisa. Ninazo picha hapa nitawaonesha. Hawasaidiwi hawa watu, kila siku wanakuwa ilimradi tu, ndiyo maana hawakui. Tunajiuliza kila siku, kwa nini hawa wafanyabiashara wadogo wadogo hawakui? Moja ya sababu ambayo kiutaalam imeelezwa ni maeneo ya kufanyia kazi ni hafifu. Siyo lazima kujenga soko kubwa sana, labda eneo kubwa kama labda tulivyofanikiwa Dodoma, hapana. Hata kama ni maeneo madogo madogo, lakini mtu afanye kazi zake kiunadhifu; na wanapokaa pamoja, wanapeana ujuzi na pia wanasaidiana hata katika mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasimama, nasema Serikali hata kama wazo hili itatokea kwamba wengi wamelikataa, mimi naliunga mkono. Naomba mkafanye *pilot,* yaani kama sehemu ya kujifunzia; kwenye Wilaya yangu ya Nyasa naliunga mkono. Yaani ninachoomba, tutoe *flexibility*. Wanaotaka zote kukopesha, hiyari yao; wanaotaka 50 kwa 50, hiyari yao; ilimradi taarifa ziwe wazi na watu waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stella Manyanya. Nilimtaja Mheshimiwa Jafari Chaurembo na Mheshimiwa Nusrat Hanje, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Mbagala, naomba sana nikishukuru chama changu cha Mapinduzi kwa kuandaa ilani ya uchaguzi ambayo inaenda kutatua shida za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi kwa maana kwa asilimia kubwa yale yote ambayo yameahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi tumeona yameletwa kwenye bajeti zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa zimefanyika katika majimbo yetu. Tumeona mambo ya elimu, afya, barabara, maji na umeme. Kila Mbunge hapa ameona vitu vilivyofanywa. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuendelea kumshukuru kwa kazi hiyo aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote mliotuongoza katika Bunge hili. Kwa maana mlitupa nafasi za kutosha katika Wizara mbalimbali tumechangia, tumeonesha mbwembwe za hali ya juu katika kudai miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawashukuru Mawaziri wote, yale ambayo tulikuwa tukiyaomba mmeendelea kuyaweka katika ilani, na katika bajeti kuu za Serikali. Kwa maana hiyo tunatarajia mambo tuliyoyaomba yanaenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyobaki sasa ni kwetu sisi Wabunge kuona namna ambavyo tutaisaidia Serikali namna bora ya kuweza kukusanya fedha ili fedha zile sasa ziende

kutekeleza miradi ambayo tumeiomba hapa kwenye Bunge letu. Miradi mingi imeandikwa katika vitabu, lakini ili itekelezwe lazima zipatikane fedha za kwenda kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchango wangu nataka niutoe katika Wizara ya Ardhi na namna gani Wizara ya Ardhi itaenda kuongeza pato katika Serikali. Ukisoma kitabu cha bajeti cha Waziri wa Ardhi ukurasa wa nane, kimeelezea, kulikuwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 221 lakini makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 115 sawa na asilimia 52. Na ukikisoma kitabu hiki, kimesema sababu ya kutokufikia hayo malengo ni taasisi na mashirika 114 yana deni la zaidi ya shilingi bilioni 78.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati muafaka sasa wa kuhakikisha hizi wizara na taasisi zinalipa madeni haya, lakini vilevile wamesema wananchi wamekuwa hawalipi pango la ardhi kwa wakati. Mawaziri wetu sasa wa Ardhi na wa TAMISEMI ni wakati wa kushirikiana kwa pamoja kuona namna gani wananchi hawa wanaenda kulipa pango la ardhi. Utaona katika halmashauri karibu zote wanapitisha magari ya matangazo, wanatangaza na kuwahamasisha wananchi waende kulipa leseni za biashara zinazotozwa na halmashauri. Kuna shida gani katika gari lile linalotangaza, wakatangaza na wakahamasisha wananchi kwenda kulipa kodi ya pango la ardhi. Kwa kufanya hivyo, na hakika wananchi wataamasika na pango la ardhi litalipwa na hatimaya tutafikia malengo ya wizara yetu hii ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kufanya *transfer* katika miliki zetu ambazo tunanunua kutoka kwa watu mbalimbali. Tulio wengi humu tuna zile *sales agreement* kwenye kufanya *transfe*r tunakuwa hatufanyi na sababu kubwa aidha uhamasishaji unakuwa mdogo au mtu akishakuwa na ile *sales agreements* inamwezesha kufanya mambo mengine ambayo kama yangezuiliwa, tafsiri yake ingemlazimu kila mtu kwenda

kufanya *transfer* ya ile hati aliyokuwa nayo. Hapa tunapoteza sana mapato kwa maana katika kufanya *transfer* kuna asilimia kumi ya thamani ya lile jengo zinakwenda *TRA* na tulio wengi kwa sababu hatufanyi *transfer,* basi mapato haya tumekuwa tukiyapoteza katika miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala zima la mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Ukisoma sheria zilizokuwepo za mabadiliko ya matumizi ya ardhi, ni elfu 30 tu ambayo inatakiwa iende wizarani, lakini ukiangalia taratibu zenyewe za kubadilisha matumizi ya ardhi, ni taratibu ndefu ambazo Serikali inatumia gharama kubwa kufanya hayo mabadiliko ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu na ushauri wangu, tuangalie namna ya kubadilisha hizi sheria angalau katika mabadiliko ya ardhi yaendane na thamani ya ardhi yenyewe. Leo mtu anabadilisha ardhi kutoka matumizi ya kawaida kuwa matumizi ya ujenzi wa *petrol station* lakini gharama ya kisheria anatakiwa alipe Sh.30,000 ebu tuangalie uhalisia, naamini haya yote tukiyafanyia kazi, basi katika sekta ya ardhi tutapata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la viwanja vilivyopimwa na vikamilikishwa. Kwa mujibu wa sheria zetu ndani ya miezi 36 huyu mtu anatakiwa akiendeleza kile kiwanja, lakini utakuta viwanja vingi havijaendelezwa. Kwa kufanya hivyo, tunakosa zile kodi za majengo. Niombe sana mamlaka husika, zizingatie hii sheria ya kuhakikisha wale wote waliopewa ardhi wanaziendeleza ardhi zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ulikuwa ndio mchango wangu katika kuhakikisha Serikali inaendelea kupata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza hiyo?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, endelea.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie juu ya Mradi wa Uendeshaji wa Jiji la Dar es Salaam. Tumekuwa tukipata maelezo hapa ambayo yamekuwa hayana mwelekeo miaka yote. Tunaambiwa uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam awamu ya pili upo katika michakato mbalimbali, tuwaombe sana hasa Waziri wa Fedha tumalize mazungumzo haya na kama hizi fedha zikipatikana zitaenda kutatua suala zima la miundombinu ya barabara katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye Jimbo langu la Mbagala ukiangalia kata zangu zote kumi, Kata ya Chamazi Kiburugwa, Mianzini, Charambe, Kilungule, Mbagala, Mbagala Kuu, Kijichi, Tuangoma na Kata ya Kibangulile. Kata hizi zinasubiri kwa hamu Mradi huo wa Uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo tumwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mradi huu aendelee kuusimamia hili uende kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam tumefanyiwa mambo ya kutosha mambo ambayo bado hayajakaa sawa, sasa hivi ni suala zima la miundombinu ya barabara. Tuwaombe sana mawaziri wetu wote wanahusika watilie mkazo suala la uboreshaji wa miundombinu ya barabara katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo yaliyo mengi na machache, naomba kuunga mkono Bajeti Kuu ya Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chaurembo. Tunaendelea na Mheshimiwa Nusrat Hanje na Mheshimiwa Kasalali Mageni na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud wajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali, lakini namshuru Mungu kwa afya na uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa saba wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametanabaisha kwamba lengo la Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni kujenga uchumi kukabiliana na umaskini pamoja na ukosefu wa ajira hasa kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya umaskini kwenye Taifa letu bado ni kubwa mno, Watanzania bado wanaishi kwenye maisha ambayo wana umaskini uliokithiri. Kwa miaka 10 mfululizo takwimu zinatuonyesha kwamba hali ya umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kwa asilimia 1.8 tu, kuanzia mwaka 2012 umaskini ulikuwa kwa asilimia 28.2, lakini mwaka 2021 umaskini upo kwa asilimia 26.4 asilimia 1.8 tu, kasi ya kinyonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanajitahidi kupambana kujikwamua kwenye umaskini, lakini pamoja na jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba Watanzania wanajikwamua kwenye lindi la umaskini, bado utitiri wa kodi ni mzigo kwa Watanzania. Watanzania wanaishi kwa kusaidiana Wabunge kwenye simu zao wana meseji za wapiga kura wao wakiwaomba hela ya kula, wakiwaomba hela ya matibabu, wakiwaomba michango ya shuleni, majukumu ni mengi, tunatumia simu zetu kufanya miamala kusaidiana kama Watanzania kujikwamua kwenye lindi la umaskini, lakini tozo za miamala ya simu, tulizungumza Bunge lililopita tunazungumza tena sasa hivi, pamoja na kwamba zimeshuka lakini Mheshimiwa Waziri kuendelea kuhangaika na trilioni 1.2 kwa sababu makadirio ya makusanyo ya tozo za miamala ya simu mwaka Julai, 2021 ilikuwa ni kukusanya shilingi trilioni 1.2 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka mwezi Machi, 2022 Serikali imekusanya bilioni 261 tu, sawasawa na asilimia 25.6. Wakati Serikali inapanga tunaamini walifanya utafiti na waliona miamala ni mingi, kilichotokea kwa kukusanya asilimia ndogo hizi ni watu kuacha kufanya miamala ya simu. Kwa hiyo watu wanalazimika kuendelea kubaki kwenye umaskini uliokithiri kwa sababu wanajiepusha na kufanya miamala, maana yake Serikali imekosa mapato na Watanzania bado ni maskini, wanahangaika hata pato la kuishi kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ku-*deal* na trilioni moja wakati ina uwezo wa kutafuta pesa nyingine kwenye kodi nyingine kubwa ni kufikiri kimaskini. Tuna kesi za kodi mahakamani, ziko kwenye Mahakama ya Rufaa za Kodi, ziko takribani Sh.357,000,309,000,000 kwenye Mahakama za Kodi. Miaka mingi na muda mrefu sana tuna hizo pesa huko, bajeti ya Serikali ni trilioni 41, trilioni 41 kwenye pesa zilizopo kwenye Mahakama za Rufani za Kodi inaingia mara nane, tuna bajeti, tuna pesa za bajeti za miaka nane mfululizo Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anahitimisha naomba atujibu nini kinaendelea Mahakamani kwenye kesi ambazo sisi tunadai. Miongoni mwa pesa hizi kuna shilingi 5,000,594,000,000 ambayo Serikali iko kwenye *negotiation* na makampuni ya madini Barrick, Bulyanhulu, *Pangea Minerals* na *AGB exploration* ziko kwenye *negotiation*. Kwa hiyo Serikali imalize *negotiation* lakini watujibu hizi pesa nyingine tunazipata lini? Waache kufikiri kimaskini kuwatoza Watanzania trilioni 1.2, wakati wana trilioni 350 ziko mahakamani. Naomba majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, asilimia 10 ya halmashauri…

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Nusrat, Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka taarifa.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayechangia kwamba kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo, anaomba yeye kwamba Bunge litoe taarifa za mahakamani, Bunge hili haliwezi kuingilia mashauri yaliyoko mahakamani, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie asilimia kumi za halmashauri. Siipokei hiyo taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kufikiri kuenda kupunguza asilimia 10 za halmashauri ni kufikiri vitu vidogovidogo ambayo sio *level* yao, Mheshimiwa Waziri yeye ni wa *level* ya juu sana, hivi vitu vidogovidogo aachane navyo. Naamini hizi pesa kuna watu zinawasaidia, Mheshimiwa Waziri mwenyewe kuna vijana wake kule, wale wanakimbiakimbia kipindi cha kampeni hizi pesa zinawasaidia. Asitafute ugomvi na laana za Watanzania kwenye vitu vidogovidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na kujenga miundombinu ya masoko kwa wamachinga, lakini nataka nimwoneshe Waziri sehemu atakayopata pesa, aachane na hizi atapata laana za watu kwa hawa maskini zinawasaidia. Kuna kitu kinaitwa Mifuko ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; mwaka 2020, Mifuko hii imetoa shilingi bilioni 894 kwa Watanzania wajasiliamali, mwaka 2021 imetoa shilingi bilioni 903, pesa nyingi.

Hizi pesa wakachukue mwaka mmoja wasiwape wajasiriamali waende wakawajengee masoko, Waziri aachane na hela za halmashauri atapata laana bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko linalochukuliwa kama mfano, lililojengwa ni la Dodoma, limejengwa kwa bilioni saba na kama milioni mia 200 hivi. Ukichukuwa shilingi bilioni 900 ukagawanya halmashauri 114 Tanzania kila halmashauri itapata bilioni saba na milioni 900, Mheshimiwa Waziri anaiona hiyo hesabu, yeye ni msomi, hivi vitu vidogo asihangaike na watu, asilimia 10 kila Mbunge analia na hii aachane nayo, achukue hizi hela za mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, aende akawajengee watu masoko. Hii hesabu niliyomwambia ni *practical* ni kitu ambacho *practical* kabisa kwa sababu Mifuko ni ya kwetu na halmashauri ni za kwetu. Tunajua sio halmashauri zote zinazohitaji soko kubwa kama hapa. Kwa hiyo tunaamini hii pesa itatumika na itabaki na Watanzania watatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, elimu, ukurasa wa 50 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza kuhusu *higher education for economic transformation.* Sasa Mheshimiwa Waziri amezungumza kuhusiana na kujenga vyuo *its well and good* ni kitu kizuri, shida yangu iko sehemu moja, kwanza itambulike huu mradi ni mradi kati ya Serikali ya Tanzania na *World Bank,* una takribani shilingi milioni 425. Lengo ni kuhakikisha kwamba *the project is design to revitalize and to expand the capacity of the universities to contribute to key areas for innovation economic development and labour market relevancy* kwa kuhakikisha kwamba wanawajengea uwezo Vyuo Vikuu ku-*train* Walimu watafiti na watu wa maofisi, *semi administrators* wawe katika *fully exponential,* wawe ni watu ambao watasaidia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi pesa ni nyingi mno pamoja na kujenga vyuo vikuu mimi shida yangu iko kwenye *content labor market relevancy,* ubainishaji bayana kati ya kinachotakiwa

kwenye soko la ajira na kinachotolewa vyuo vikuu. Vyuo vyetu Tanzania vinajiendesha vyenyewe, kuna kitu kinaitwa *Senate* za vyuo, kina *autonomy power,* ni kitu ambacho kilipitishwa Kiserikali na ni *well and good,* lakini vyuo siku hizi vinajianzishia kozi ambazo sio hitaji ya soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kozi inaitwa *social protection* katika Chuo cha *IFM* hata kwenye *portal* ya ajira ya Serikali haitambuliwi, lakini kuna kozi inaitwa *bachelor of science in physics* inatolewa *UDOM Bachelor of Science in Mathematics,* hakuna kwenye *portal* ya ajira. Watanzania wanajinyima wanasomesha watoto wao vyuo vikuu, wanaenda ku-*apply* kazi, hata *portal* ya ajira hazitambui hizo kozi. Naomba Serikali iingilie kati, ianzishe chombo ambacho kita-*oversee* mitaala ya vyuo vikuu kwa sababu hata kinachofanyiwa mapitio sasa hivi ni sera elimu ya msingi, awali na sekondari, vyuo vikuu vinajiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha hata zile Wakala za Serikali sasa hivi zinatoa elimu, kuna chuo kinaitwa *ADEM* kipo Bagamoyo, sio chuo *actually* ni *agency,* ni Wakala wa Serikali, lakini leo wanatoa *diploma,* lakini pia wamepeleka maombi wanataka waanzishe *degree* yaani kila mtu anajifanyia kiholela, hatuwezi kufika. Kianzishwe chombo ambacho kitaratibu mtaala wa vyuo vikuu ili kozi zinazoanzishwa ziendane na hitaji la soko la ajira, lakini na dira na mwelekeo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili kwenye elimu ni mitaala. Sasa hivi Wizara ya Elimu inapitia mitaala lakini kinachofanyika ni kama mchezo wa kuigiza, linafanyika kongamano, watu wanapewa dakika mbilimbili watoe maoni, halafu kikosi kazi kinakusanya maoni, kinaenda kujifungia kichakate. Kwenye nchi hii hatujaanza leo kukusanya maoni ya kurekebisha mitaala mwaka 1981, Mzee Nyerere aliunda *Makwetta Commission* ya kwenda kupita mfumo wa elimu,

wabobezi wasomi walikaa, wakachakata, wakaandika, wakapelekea Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 Mzee Mwinyi aliunda *National Task Force* ya kwenye elimu, wakachakata, Wizara ya Elimu ilikaa pembeni ikaangalia, hiki kinachofanywa hapa tutarudi tuje kuambizana humu. Mzee Kikwete kuna *Professor* wangu, Mwalimu wangu wa Chuo Kikuu, *Professor* Kitila Mkumbo, Mheshimiwa Mbunge, ameandika *ten years of Jakaya Kikwete Presidency, promises, achievement, and challenges,* ameeleza aliyoyafanya Jakaya Kikwete kwenye elimu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Tunaomba itengenezwe *commission* ya Rais ambayo itafanya mchakato wa kupitia sera tunachokifanya ni mchezo wa kuigiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa dakika moja…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa nilikuachia umalizie sentensi yako.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamtaja mchangiaji anayefuata kuna wageni ambao wameingia naomba niwatambue na niwatangaze.

Kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika yupo Ndugu Kimber Bohenc ambaye ni Mkurugenzi wa Afya, Shirika la *Henry Jason Foundation Medical Research International* amefika yuko hapa, karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna mwingine Ndugu Sely Chalamila, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la *Henry Jason Foundation Medical Research International,* karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia kuna viongozi 40 wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi wa Kata ya Nkuhungu hapa Dodoma ambao walikuja kutembelea hapa, walikuwa hawakupata fursa. Wale pale, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna wageni vile vile ambao wameingia, Madiwani 11 wa Wilaya ya Wete pamoja na Kamati ya Siasa ya Wilaya ikiongozwa na Katibu wa Chama Wilaya, ndugu Bilali Maulid. Karibuni sana katika Bunge letu. Hawa wageni wanatoka kwa Mheshimiwa Chande nafikiri. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Kasalali Mageni na baadaye Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. KASASALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima. Niwashukuru vile vile wapiga kura wa Jimbo la Sumve kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakinionesha tangu nichaguliwe kuwa Mbunge wao katika kutekeleza majukumu ya kuleteana maendeleo na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajielekeza katika hoja yangu, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana ambayo ameifanya na anaendelea kuifanya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi sisi watu wa Jimbo la Sumve, Mbunge wa Sumve anaposimama na kupongeza, anapongeza kwa mifano ambayo ipo bayana. Tangu Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, sisi watu wa Sumve alitukuta tunazo zahanati 21 tu, lakini leo ninapozungumza, zahanati 10 ndani ya mwaka mmoja, yaani

ninapozungumza zahanati 21 nazungumza tangu uhuru, lakini ndani ya mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, watu wa Kijiji cha Mwashilalage, Zahanati; Kijiji cha Bung'egeja, zahanati; Kijiji cha Nyamikoma, Zahanati inaanza kujengwa; Kijiji cha Busule, Zahanati; na Kijiji cha Kinamweli, Zahanati. Naweza kuzungumza hapa vijiji vingi lakini ndani yam waka mmoja kwa hiyo tunaposema Rais Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kubwa nadhani ni kazi ambazo zinaonekana kwa urahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa wakulima na wafugaji, katika Jimbo la Sumve tunalima pamba Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametukuta tunauza pamba kwa Shilingi 800 lakini mwaka jana tumeuza pamba kwa bei ya juu kabisa ya 1,500 lakini sasa hivi pamba tunaendelea kuiuza kwa bei ya Shilingi 2,000. Kwa hiyo tunaposema Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imetusaidia wakulima mifano inaonekana na ni bayana, ndiyo maana naona kwamba nikisimama hapa nikaacha kupongeza nitakuwa sijawatendea haki watu wa Sumve. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa na mimi nielekee kwenye kushauri katika bajeti ambayo Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ametusomea humu bajeti ya Serikali yetu pendwa ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunatakiwa sisi ambao wenzetu hawa ambao mmepewa kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika Wizara mbalimbali mnatakiwa mtumie muda mwingi kujifunza namna ambavyo Mheshimiwa Rais anavyotaka nchi iende. Mheshimiwa Rais ametuonyesha kwenye *TARURA* kwamba anataka kila eneo lipate kwa usawa. Wabunge ni mashahidi kwenye Majimbo yetu, Mheshimiwa Rais alipoingia tu alitupatia Milioni 500 kila Jimbo akiwa na maana kwamba hii nchi ni moja, watu wote wapate maendeleo kwa usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye fedha maarufu za Mama Samia ambazo tulikopa Mama ametupatia kwa usawa kila Jimbo linajenga madarasa watu wanaona, kwa hiyo tunatakiwa sasa na maeneo mengine mfahamu nia ya Mheshimiwa Rais kupitia mifano hii. Katika sekta ya umeme sote tunaona nchi nzima vijiji vyote vinawekewa umeme, Mama anataka nchi iende kwa usawa. Sasa ipo shida moja kwenye eneo la miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hii kuna maeneo ambayo yanabandua lami yanaweka mpya na kuna maeneo ambayo hayana hata milimita moja ya lami. Katika jumbo la Sumve ambalo mimi ninatoka, ambalo ninadhani wote tukipitishana kwenye historia ya nchi yetu Jimbo la Sumve liko kwenye Wilaya ya Kwimba, Wilaya ya Kwimba ni moja ya Wilaya ambazo zimeachwa ni Wilaya ambazo zilianzishwa kabla hata hatujapata uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Nyanza *Province* kulikuwa na Wilaya ya Mwanza, Wilaya ya Kwimba, Wilaya ya Maswa, Wilaya ya Musoma, Wilaya ya Shinyanga, Wilaya ya Kahama na Wilaya ya Bukoba, baada ya Nyanza Province kutoka ukaja Mkoa wa Mwanza Wilaya Nne za kwanza Kwimba imo, Kwimba Mwanza Geita na Ukerewe lakini baada ya Geita kutoka Wilaya Kwimba bado ipo na Jimbo lake la Sumve imezaa Wilaya ya Misungwi, Wilaya ya Misungwi ina lami, imezaa Wilaya ya Magu, Makao Mkuu ya Magu na Mkoa wa Mwanza na Mikoa mingine imeunganishwa na lami, tukazaa mjukuu Busega ameunganishwa na lami. Sasa Kwimba tunashida gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wa Fedha, naiomba sana Serikali ya CCM igawe maendeleo kwa usawa hasa kwenye sekta ya barabara. Haiwezekani kila siku tangu Rais Mkapa alisimama akatuahidi watu wa Kwimba na sisi tutapata lami haikufanikiwa, akaja Rais Kikwete akatuahidi haikufanikiwa,

akaja Hayati Magufuli akatuahidi haikufanikiwa! Hapa sasa hivi tuna amani Rais Samia ameonesha dhahiri anataka nchi iende kwa usawa. Sasa nimepitia hii bajeti bado mnaonekana hamko *serious* kwenye jambo la barabara kwenye baadhi ya maeneo hasa Jimbo ninalotoka la Sumve.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Sumve tulikuwa tukiimba wimbo wetu hapa kuanzia bajeti iliyopita tunataka walau basi kwenye bajeti na sisi mtuone mtujengee barabara yetu ya kimkakati na ya muhimu inayoanzia Magu inapita Bukwimba inaenda Ngudu mpaka Hungumalwa, barabara yenye urefu wa kilimeta 71 katika bajeti iliyopita Serikali ikatupangia kutujengea kilomita 10 hawajajenga hata milimita moja, katika bajeti hii ndiyo sioni kabisa hata mwelekeo, sasa tukienda namna hii nchi yetu tutakuwa tunapendelea baadhi ya maeneo na kutekeleza baadhi ya maeneo,.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike wakati tufahamu kwamba ili maendeleo yafaidishe watu wetu lazima kuwe na usawa kwenye ugawanaji wa keki ya Taifa, haiwezekani wenzetu wanabandua lami sisi hatuijui, ukichukua mtoto wa Sumve ukamwambia neno lami hajui! Ninaposema hapa mnaweza mkawa hamnielewi kwa sababu ninyi wengi mnalami kwenu lakini Sumve hatuna hata milimita moja ya lami. Baada ya miaka yote hii ya uhuru sasa tufike wakati tuweke mstari na sisi sasa muda wetu umefika, eleweni Mheshimiwa Rais anataka watu wote wapate haki, watu wote wagawiwe keki hii kwa usawa, twendeni mtugawie kwa usawa zipo barabara za muhimu sana kwenyeJimbo letu, katika Serengeti ya Kusini…

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**T A A R I F A**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri sana wa Mheshimiwa Mbunge makini, jambo hili ni jambo ambalo haliwezi kuachwa liendelee hivi. Wengine tulioko Kaskazini tunazungukwa na Wilaya zenye lami na zingine ndiyo hizo ambazo ni bandika bandua imefika wakati wale ambao wanapata barabara za lami sasa hata za zamani wasimame tupate lami wengine ili na wao waweze kupata na wale walipata kupitia *TANROADS* wasipewe barabara nyingine kupitia *TARURA* mpaka Watanzania wengine tuwe tumepata lami, tumeahidiwa haitekelezwi! Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mageni taarifa hiyo unaipokea.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naipokea kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kwamba tugawiwe kwa usawa nafikiri tunatakiwa tufike wakati tuelewane, Mheshimiwa Mwigulu na wewe unatoka Iramba huko angalau labda ninyi mmeungwa kwa lami, lakini tuelewe kwamba watu wetu wanahitaji maendeleo, tunapotaka utalii ukue Serengeti Kusini kote mimi nilikuwa juzi Mwandoya wananchi wanachukia Tembo, wanachukia mbuga za Wanyama kuliko kitu chochote, kwa sababu hawafaidiki nazo. Barabara za msingi zinazotakiwa kupeleka watalii waende mpaka Meatu, waende kwenye maeneo ya utalii ya Serengeti ya Kusini zote ni za vumbi! Barabara inayotakiwa kutoka Mwanza ikaja ikapita Fulo, ikaenda ikapita Sumve, ikaenda ikapita Nyambiti, ikaenda Malya mpaka Maswa, barabara hii imekuwa ni *story* na barabara ya kujazwa ukurasa wa Ilani inaandikwa kila siku, haijengwi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tufike wakati jamani kama alivyosema Mheshimiwa Ole-Sendeka waliopata wasimame,

Mheshimiwa Waziri angalia hii bajeti yako haiwezekani sisi watu wa Sumve tukawa tunakuja kukusindikiza humu, tunasindikiza wengine wanawekewa lami sisi tuko tu hapa tunapiga makofi, wananchi wa Sumve wameniambia nisipige makofi kwenye mambo ya hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitapiga makofi kwenye mambo ya hivi, haiwezekani sisi tukasindikiza watu tukabaki kuwa watazamaji wa lami za watu. Inafika wakati mimi wakati kwa historia mwaka 2000 kuna binti anatusaidia nyumbani, Mimi naenda Shinyanga nikapanda naye basi nilipofika eneo ambapo kuna lami, kwenye eneo la Mabuki pale, yule mtoto akaniambia Kaka hivi kumbe barabara za huku zimewekewa *cement* yaani haelewi lami na *cement* anaonaga ndani sasa ifike wakati muwakumbuke hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi ni ya kwetu sote tunataka maendeleo, msisitizo wangu ni kwamba maendeleo na keki ya Taifa tuigawane kwa usawa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kasalali Mageni. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud Mheshimiwa Emmanuel Shangai na Mheshimiwa Lucy Mayenga, ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wake na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa bajeti nzuri yenye kutatua changamoto mbalimbali za wananchi wa Tanzania ikiwemo wakulima, wafugaji na wavuvi na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa pia ndiye Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi kwa kuiongoza nchi yetu kwa kutumia

busara na weledi wa kuhakikisha nchi yetu inavuka salama katika matukio mbalimbali yaliyotukumba ya kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na sekta ya kilimo. Naipongeza Serikali kwa kuweka bajeti kubwa kwenye Wizara ya Kilimo ambapo sasa kilimo chetu kitakwenda kuwa kilimo chenye tija lakini kilimo kitachomkomboa mkulima mdogomdogo na mkubwa pia kuongeza uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na bajeti kubwa hiyo ya kilimo ambapo nitakwenda kujikita kwenye kilimo cha umwagiliaji, mambo ya viuatilifu, Maafisa Ugani, tunayo mazao ya biashara ambayo wakulima wetu wanapata tija kupitia biashara na Serikali inapata mapato. Naomba kuishauri Serikali pamoja na mazao yetu ya biashara nashauri kwamba kutokana na changamoto zetu za ndani ya nchi tuchague mazao fulani ya kimkakati kwa maana ya kwamba tujikite kwa kipindi cha miaka miwili au mitatu Tanzania tunakwenda kuondokana na tatizo ama la mafuta ya kupikia, sukari au jambo jingine ili tukifika hatua hiyo tukaweza kujitosheleza na tukaweza kuuza baadae tunajiwekea kipindi kingine kutatua changamoto nyingine ambayo inatukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu sekta ya uvuvi, naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali za kuinua uvuvi hapa nchini, kwa kununua vifaa mbalimbali vya uvuvi na kuwasaidia wavuvi wetu. Katika kuimarisha uvuvi wa Bahari Kuu lazima taasisi mbili ziimarishwe ambayo ni *TAFICO* na *ZAFICO*. Kwa upande wa *TAFICO* bado miundombinu yake haijawa kamilifu na kwa bajeti hii itachukua muda kukamilika pamoja na bajeti iliyotengwa nashauri Serikali itafute fedha zaidi ili kuhakikisha *TAFICO* inafufuka na inafanya kazi zake. Kwa sababu kwenye *TAFICO* kuna miundombinu ambayo inagharimu fedha nyingi ikiwemo vyumba vya kuhifadhia samaki, vyumba vya kuweka majokofu ya baridi, inatakiwa kutengenezwa gati, inatakiwa kujenga majengo.

Majengo ambayo sasa yapo kwenye fukwe ambazo fukwe zinaliwa na bahari, kwa hivyo, panahitajika fedha za kutosha ili kulifufua hili Shirika la *TAFICO* liweze kujikimu na kujikita katika uzalishaji utakapofika huu uvuvi wa Bahari Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Serikali pia kwa kuwekeza kwenye sekta ya maji kwa kununua mitambo na vitendea kazi vya kuchimba visima na mabwawa na hili ndiyo hasa dhamira ya Serikali kwamba kumtua ndoo mwanamke kichwani pia kuhamasisha kilimo, ufugaji na uvuvi. Kwa hivyo, vitu vitatu hivi vimeenda sambamba naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kwenye sekta ya mazingira tumeona kwenye bajeti yetu ya Serikali kuna mambo ya mazingira yanakwenda kutekelezwa, lakini mazingira tuyatazame kwa ukubwa na upana wake kulingana na mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi yanaharibu sana mazingira yetu, kwa hivyo ni vizuri kuwekeza zaidi kwenye kuhifadhi mazingira yetu ili tubaki na nchi ikiwa salama na ubora wake kama ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika bajeti hii kutambua mchango wa asasi zisizo za Kiserikali katika kuinua uchumi wa Taifa, kuinua uchumi wa wananchi na kuleta maendeleo katika jamii yetu, nampongeza sana kwa kutambua mchango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongozea pale katika kuwekeza sekta ya kilimo tumeona kuna fedha hapa zimetengwa Bilioni 6.1 kwa ajili ya kumalizia kiwanda cha mbolea. Bado naendelea kusisitiza mbolea ni silaha, tunahitaji mbolea ya kutosha kwa ajili ya kilimo chetu hapa nchini, mbolea za aina mbalimbali kutokana na udongo wetu na mazingira yetu. Kwa hivyo, kuna haja Serikali kuwekeza zaidi kwenye viwanda vya mbolea ili

tuweze kujitosheleza hapa nchini kwa mbolea na tuache kuagiza nje mbolea. Kwa sababu ardhi tunayo, malighafi tunayo na fedha tunaweza tukapata katika maeneo mbalimbali kama hizi tulizozitafuta na tutafute kuhamasisha wananchi wa humu ndani ya nchi kuwekeza katika sekta ya viwanda vya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi kumpongeza Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake katika ukurasa wa 74 ameeleza kwa hisia jinsi ya kukitumia Kiswahili na kukienzi Kiswahili. Kiswahili ni fursa, Kiswahili ni ajira, Kiswahili ni bidhaa, pindi tukikitumia vizuri Kiswahili nchi yetu tutazidi kuitangaza na hapa tuunganishe na tuongeze na utalii wa lugha, utalii wa lugha utatuongezea mapato katika nchi na kuitangaza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii si kwa watu wa rangi ya aina Fulani, sasa hivi tunapata watalii wa Afrika wenzetu wanaokuja Tanzania kwa sababu tu ya lugha ya Kiswahili na wakifika hapa Tanzania wanapata fursa ya kuona hivyo vivutio vingine vya utalii kwa maana walikuja tu kwa sababu ya kuona hiyo Tanzania inayosifika na lugha ya Kiswahili inayokua duniani wanataka kuja kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosisitiza hapa tuwekeze kwenye watalaam, tuwape motisha wataalam wetu wa lugha ya Kiswahili pia tuweke motisha kwa wanafunzi waweze kujikita katika kusoma Kiswahili na kukisomea na kuwa watalaam, kwa maana ya kuwapatia mikopo na motisha mbalimbali ili tukipende Kiswahili kama tunavyopenda masomo ya sayansi na Kiswahili nacho tukipe kipaumbele. Hayo ni mawazo yangu kwamba wasomi wa Kiswahili tuwaongezee weledi kwa maana ya kwamba tuwekeze wajifunze lugha zaidi ya mbili ndiyo soko linapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili chetu tusiruhusu kikatekwa, ninachotaka kusema sasa hivi kuna lugha zinazungumzwa kwamba Kiswahili kimeanzia nchi fulani kimekuja Tanzania kimefia mahali fulani. Kiswahili ni mali yetu Watanzania tusikubali kikaporwa ikawa kama Mlima Kilimanjaro, sasa hivi Kiswahili ni rasilimali ya nchi tukienzi, tukitunze, tuhakikishe kinakua na kitambulisha nchi yetu, wajanja wasije wakatupora lugha yetu na ndiyo maana nasisitiza tuwekeze kwenye lugha ya Kiswahili kwa kuhamasisha vijana wetu wasome lugha zaidi ya moja au mbili ili tupate soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kiswahili tunapokwenda kupeleka watalaam katika nchi fulani ambayo hawazungumzi kiingereza sisi tunapata nini? Tuhakikishe na zile nchi wanafundishwa wanafunzi wetu lugha nyingi kama Kifaransa, Kibelgiji, Kireno, kwa sababu sisi tunawapa lakini baada ya muda Walimu wetu watakua hawana tena kazi, watafundishana wenyewe kwa wenyewe hilo tuweke angalizo. Watafundishana wenyewe kwa wenyewe ndani ya nchi kutokana na zile lugha zao za ndani wanazozitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kuna nchi inaongea Kifaransa baada ya muda hawa watu wetu wakifika huko Wafaransa watachukuana na nchi nyingine za Kifaransa watakwenda huko watasomeshana, ndiyo maana nasema tuwape na sisi tuchukue kwa maana na sisi tupate zile lugha zingine za Kifaransa, Kireno, Kigiriki tuzipate Watanzania, tusibaki tu na Kiswahili na Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namalizia kwa kuipongeza sana Serikali, tumuunge mkono Rais wetu katika kuwaletea wananchi maendeleo tupo nae bega bega. Ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud nilimtaja Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mheshimiwa Lucy Mayenga na Bonna Kamoli, wajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Serikali. Mimi nimshukuru na kumpongeza Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa bajeti nzuri pamoja na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka mikakati mingi sana lakini mwisho wa yote tunachokusanya ndicho kitakacho-*determine* kile ambacho tutaenda kufanya. Tusipokusanya vizuri hatuwezi kutekeleza mikakati yote ambayo tumeweka kama Serikali. Bajeti hii itaenda kutekelezwa vizuri kama tutaweka nguvu nyingi sana kwenye ukusanyaji wa fedha pamoja na kuamua kuondoa mianya yote ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wilaya yangu ya Ngorongoro nilishamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba tunahitaji tujengewe kituo cha forodha mpakani mwa Kenya na Tanzania. Wananchi wale wanataabika sana kufanya biashara. Kutoka Loliondo mpaka Namanga ni zaidi ya kilomita 120. Kwa hiyo, mpaka wetu bado ni mkubwa sana, tukijenga Serikali itakusanya mapato makubwa katika lile eneo pamoja na wananchi kufanya biashara kiurahisi katika lile eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine Mheshimiwa Waziri *is not your classic* kwenda kuchukua fedha za asilimia 10 ya Vijana pamoja na akina mama kwa ajili ya kuwapa machinga. Kwa hiyo, na mimi nishauri kama alivyosema Nusrat Hanje, kwamba tuache hilo, tusifikirie kabisa. Tunaweza kukusanya fedha katika maeneo mengine ambayo itaisaidia Serikali na wale akina

mama pamoja na Vijana nao wanufaike na hiyo asilimia 10 katika ngazi ya halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshauri katika halmashauri zetu kuna upotevu mkubwa wa mapato; nina uwezo wa kutoa ushuhuda. Nilipokuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro niliamua siku moja kwenda kukusanya mapato mwenyewe kwenye mnada ambao wataalamu walikuwa wanakusanya shilingi 1,000,000, nilikusanya shilingi 5,000,000. Nikasimamia mnada huo *consecutively for four months;* kwa sababu tarehe 15 na tarehe 02 nikakusanya shilingi milioni 40. Lakini ukiangalia data za wataalam wetu wao kwa miezi minne wanakusanya shilingi 5,000,000. Sasa kule chini kuna upotevu mkubwa. Nikawapa Madiwani kwenye minada mingine. Nikawaambia hebu tusimamie tuone kwamba ni kwamba hakuna fedha au ni wataalam hawakusanyi. Kila mnada aliyesimamia Mheshimiwa Diwani ili-*double* na ku-*triple* kwa wakati mwingine. Mnada ambao wao wanakusanya 1,000,000 sisi tukawa tunakusanya zaidi ya 4,000,000 kwa mwezi, lakini wao wanakusanya 1,000,000. Fedha nyingi za Watanzania zinaenda kwenye mifuko ya watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe *TAMISEMI* msimamie ukusanyaji wa mapato, kule Wakurugenzi hawakusanyi mapato. Tulitakiwa kukusanya zaidi ya bilioni 800, tumekusanya 700 na hamsini na kitu. Kwenye Halmashauri zetu tuna uwezo wa kukusanya mpaka trioni mbili tukiamua kuwapa watu waadilifu, lakini tukiendelea hivi tutaendelea na *story* zilezile kila siku. Hata hii asilimia 10 wananchi wetu wangekuwa wananufaika sana kama makusanyo yangefanyika. Lakini pia *TRA* tunapoteza fedha nyingi sana kwenye misamaha ya kodi ambayo haina maana. Ni lazima sasa Mheshimiwa Waziri usimamie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni suala la kuondoa ada kidato cha tano na sita; niipongeze Serikali, lakini

iendane sambamba na kuondoa michango ambayo haina maana. Kwa mfano leo mwanafunzi anaenda kuripoti shule hiyo ina zaidi ya miaka 50 unamwambia aende na kiti na meza. Ina maana kwa miaka yote kila mwanafunzi anayemaliza anaondoka na meza na kiti chake? Kila mwaka tunachanga fedha kwa ajili ya viti na meza? Haiwezekani! Kwa hiyo, niipongeze Serikali kwa kuondoa ada hiyo kwa sababu itawasaidia Watanzania wengi, lakini iendane sambamba na kuondoa michango ambayo haina maana kwa Watanzania kama kweli tunataka kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza haya niende kwenye hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia. Wengi hawajui kinachoendelea katika eneo la Pori Tengefu la Loliondo. Mimi ni Mbunge, ni wananchi wangu ndiyo wanaoteswa kule. Naomba niwaambie kitu kimoja, watu wengi hapa wanasema, akinyanyuka mtu anasema kwamba ardhi ya Tanzania ni ya Rais. Tusimchonganishe Rais na wananchi, ardhi ya Tanzania kwa mujibu wa Sheria ni ya Umma. Rais amepewa kama mdhamini tu. Kwa hiyo kwa mtu yoyote anayesimama ukitaka soma *Land Policy* ya Tanzania ya mwaka 1997. Naomba kunukuu kipengele "(a) *All land in Tanzania is public land, versed in the President as a trustee on behalf of all Tanzanian.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wengine tunasimama wanaofanya kazi inayofanyika Loliondo siyo Rais ni watendaji wake ambao hawataki kujifunza kutoka kwa waliyowatangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni lazima tujue, ardhi *square kilometer* 1,500 katika eneo la Loliondo ni ardhi ya vijiji; kata nane, vijiji 14. Na kwa nini ardhi ile inatwaaliwa, Sera yetu ya Ardhi inatuambia nini kuhusiana na unapotaka kuchukua ardhi ya wananchi, ardhi ya vijiji? Kipengele Na. 4 inasema;

"*Consultation and consent of all Village council will be required whenever alienation of Village land is necessary*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Loliondo kinachofanyika ni unyakuaji wa ardhi, hakuna mwananchi, hakuna Serikali ya Kijiji ambayo imeridhia ardhi ile kutengwa, hakuna. Lakini watu wanasema ni ardhi, *it's not a bared land*, *is the land with people*. Kwa hiyo, kinachofanyika pamoja na masuala mengine lakini ieleweke wananchi wa Loliondo…

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Ridhiwani.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa msemaji anayesema sasa asipotoshe. Kinachofanyika Loliondo ni uwekaji wa mawe kuonesha mipaka baina ya ardhi ya kijiji na ardhi ambayo inatumika kwa ajili ya kupita maeneo ya mifugo. Kwa hiyo asiseme kwamba hapa kuna ardhi inayochukuliwa, hakuna ardhi inayochukuliwa kinachowekwa ni mipaka kuonesha baina ya maeneo ambayo yanatumika na wananchi na maeneo ambayo kwa shughuli nyingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai, unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni watu wazima, unatenga ile ardhi kutoka ardhi ya nani? Unatenga kutoka kwenye ardhi ya nani.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mzungumzaji, kwamba eneo la Pori Tengefu la Loliondo kwa mara ya kwanza lilitangazwa na Serikali ya Kikoloni kupitia *Fauna Conservation Ordinance* ya Mwaka 1959. Na tangu wakati huo hatujafuta, tumekuwa tukifuta Sheria tuna-*repeal* na kutengeneza nyingine. Kinachofanyika ni kuweka alama kwenye eneo la *square kilometer* 1,500 kati ya *square kilometer* 4,000 za eneo la Pori Tengefu la Loliondo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai, unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utunze muda wangu, hawa wana nia tu ya kumaliza muda wangu. Lakini ukweli ni kwamba mimi ninajua kinachoendelea. Ardhi ile ni ardhi ya vijiji kwa mujibu wa sheria zote za Tanzania.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hajaanza hata kusema jambo jingine, msubiri aseme halafu utaomba taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaongopa, anavuruga, haongei ukweli.

**MWENYEKITI:** Hata akimaliza kusema nitakupa utoe taarifa. Mheshimiwa Shangai endelea.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea suala la ardhi tunaongelea maisha ya wananchi na uchumi wao. Naomba ni-*quote* maneno kwa ruhusa yako ya Bwana William Tenga ambaye ni Mtaalam wa masuala ya ardhi, ambaye amehusisha suala la migogoro ya ardhi kwamba ni sehemu ya maisha ya wananchi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema hivi; "*Nobody can live without land and most people have to share it, creating, competing right. This be about righting land the not be avoided. People relationship to land depend on many factors and have a strong cultural element*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia ardhi ile ya Loliondo ninazungumzia maisha ya watu wanaoishi pale na Wilaya zote za wafugani kwa sababu…

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

Taarifa Mheshimiwa Shangai.

**T A A R I F A**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata huyo Mheshimiwa anayezungumza sasa hivi Mbunge wa Loliondo, hata kwenye hiyo *definition* aliyoitoa sasa hivi inasema hakuna mwananchi anaweza akaishi bila ardhi. Hata hawa wanaohama Loliondo kwa hiyari yao wameonyeshwa maeneo

mengine ya kuishi, kwa hiyo wako *within* hiyo *definition* ambayo yeye ameisoma sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai, unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei kwa sababu hajui anachozungumza. Mimi nazungumzia Loliondo hakuna mwananchi anayehama Loliondo, yeye akarejee Ngorongoro, ndicho anachotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee pia maneno ya Profesa wa Sheria Chris Maina Peter, anasema; *"Land is an important resource in the world today, it is the main source of live loud and survivor. Therefore, whoever control land logically control the lives of others. This is because that person or persons control what guarantee survivor of human being. Due to the proximity of land to survivor it is frequently related to the right to live"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la ardhi ile tunazungumzia maisha ya wananchi wetu. Mimi nadhani Serikali inatakiwa kufikiria upya. Pamoja na kwamba wameweka mipaka lakini ile ardhi bado ni muhimu kwa ajili ya wananchi wale. Wananchi wale ukijaribu kuangalia katika wilaya zetu za wafugaji, ukiangalia lile eneo la Loliondo kuna vijiji. Naibu Waziri juzi alisema kwamba hakuna vijiji, wapo wananchi. Ukienda Longido kwenye lile eneo ambalo wanataka kupandisha liwe pori la akiba kuna vijiji 22.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Shangai.

**T A A R I F A**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri sana wa Mbunge makini wa Ngorongoro; kumekuwepo na hoja zinazozunguka za kuzungumza habari ya maslahi ya taifa na urithi wa dunia. Tunazungumza urithi wa dunia ipi bila Ngorongoro? maslahi ya taifa lipi bila Ngorongoro? Wale ni binaadamu wenye haki sawasawa na binaadamu wengine ni sehemu ya urithi na ni sehemu ya Taifa hili. Hivyo, wana haki waachwe kwenye eneo lao kwa sababu eneo hilo ni lao ni ardhi ya wazazi wao walikowazika mababu zao. Waendelee kupata maisha yao na Sheria inawalinda na *repealing clauses* zote za Sheria ya Mwaka 1974 na Sheria ya mwaka 2009 Kifungu cha 120 na Kifungu cha 85 na 86 ya *Wildlife Conservation Act* ya 1974 zote zime *repeal* mambo hayo ambayo yanazungumzwa. Ni vizuri watu wakasoma Sheria kwa ukamilifu na hasa hawa waliyokuwa wanadai jana kama ni wanasheria waende kwenye *repealing clause* na *transition clause*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai, unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya napokea. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia ninajua kwamba wengi wanacheka kwa sababu siyo maisha ya watu wao. Lakini mimi ni maisha ya wananchi wangu, wazazi wangu, wadogo zangu na kaka zangu; lakini watu wanafanya michezo, tunapotosha; kwa sababu yaliyofanyika Loliondo kwa wale wananchi *very inhuman*. Wananchi wametoroka wameenda Kenya, wananchi wanakimbia kwenda kutibiwa Kenya kwa sababu wamenyimwa *PF3*, kwa sababu na Hospitali zenyewe zilizopo kilomita 70 na nyingine kilometa 30…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai, samahani hayo unayosema una uthibitisho nayo maana usije ukazungumza hapa Bungeni jambo ambalo huna uthibitisho nalo, halafu mwisho wa siku badala ya kusema wewe usahihi ikawa ndiyo wananchi wanapotoshwa.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba wananchi wameenda kutibiwa Kenya. Naomba unilinde na watu waniheshimu.

**MWENYEKITI:** Malizia maana muda wako kengele ilikuwa imepiga kwa hiyo kutokana na muda huu nakuongezea dakika moja tu umalizie.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumaliza.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nakushukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Bonnah Kamoli na Mheshimiwa Hassan.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii. Nisipoteze muda nitoe pongezi nyingi sana kwa Wizara hii, watendaji wote wa Wizara hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu lakini bila kumsahau Kamishna Mkuu wa *TRA* ambaye anapambana sana kuhakikisha kwamba Taifa letu linapata mapato kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niongee kwa kifupi, najua wapi nitamalizia muda wangu. Nataka nitoe ushauri mmoja, wenzetu wengi wamezungumza, Wabunge wengi wamezungumza kwamba katika nchi yetu kazi ambayo

amekuwa akiifanya *CAG* ni kazi ambayo inakuja mwisho kabisa, na amekuwa akigundua udhaifu mkubwa. Sasa wengi wametoa mapendekezo, kwamba tathmini, *evaluation* pamoja na *monitoring* inaonekana kama kuna yaani haipo. Ninafahamu kwamba chini ya Wizara ya Fedha Kitengo hiki kipo lakini nazani pengine kutokana na mfumo imekuwa ngumu kuweza kusimamia hii miradi kiasi ambacho imekuwa ikisababisha *CAG* kuja kugundua madudu mengi sana kwenye miradi yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kutoa pendekezo, pendekezo langu ni kwamba naomba, kwamba kazi ya *CAG* ipo kwenye ukaguzi, naomba kupendekeza Serikali na hasa Mheshimiwa Rais aunde *Presidential Bureau* ambayo itakuwa inafuatilia kuweza kufanya *monitoring* na *evaluation* ya miradi yetu yote hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba hii ikiwepo kwanza watu watakuwa na heshima kwa sababu najua kwa mfumo uliopo sasa hivi Viongozi mbalimbali Mikoani, Wilayani, *sometimes* hawana mkono wa moja kwa moja kwenye kusimamia miradi kwa sababu ya hali halisi iliyopo; kwamba ni *eyes on, hands off*. Kwa hiyo unaweza ukaona kuna hitilafu lakini kuweza kusema kwamba mradi huu una hitilafu inakuwa ni shida. Lakini hata Kamati mbalimbali za Bunge, zipo, inakuwa ngumu sana kuweza kwenda na kuweza kuona kwa sababu ni wanakwenda kipindi ambacho, kwa mfano kama tunapokuwa tuko Bungeni wanatembelea mradi lakini baada ya hapo unakuta kwamba mradi unakuwa unaendelea. Kwa hiyo inakuwa si rahisi; madudu yakiendelea kule *monitoring* yake inakuwa ngumu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaomba, kwamba hili suala la hiki Kifungu kwenye *TCRA* ambacho mlikuwa mnataka kuondoa, nilikuwa naomba kifungu hiki majukumu haya ya *TCRA* yaendelee kubaki ya kwao. Ninasema hivyo kwa sababu wengi

wamesema kwamba ubora wa utendaji kazi wa *TBS* wanapopima ubora na ubora wa *TBS* ni vitu viwili tofuati. Na *next time* ningeshauri Wizara hii wakati wanataka kufanya vitu kama hivi wawe wawe wana-*consult* hizo Sekta mbalimbali. Kwa mfano Wizara ya Kilimo kuna vifungu, na huku *TCRA* na maeneo mengine. Kwa sababu vitu hivi mnaweza mkaleta siku nyingine ikaja ikaleta hitilafu kubwa sana kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu *Royal Tour*. Mimi nilikuwa naomba kuzungumza jambo moja. Mheshimiwa Rais wetu, kipenzi chetu, Mama yetu anafanya kazi kubwa sana. Kila Mbunge anayesimama hapa anakubali kwamba kuna kazi kubwa sana ambayo inafanywa. Lakini nilikuwa naomba kutoa angalizo kubwa sana kwa Waheshimiwa wabunge. Ipo tabia imezuka kwa baadhi ya wabunge kuleta maneno mengi sana dhidi ya Rais na Serikali yake. Ninasema hivi kwa sababu kuna tabia ya watu, mtu anaweza akasimama, asilimia kubwa sana hapa Bungeni tunaiunga mkono Serikali na tunatambua mchango mkubwa ambao Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akiufanya. Lakini bado wapo baadhi ya Wabunge wachache ambao wao wanaamua makusudi kabisa kuipotosha Serikali, kupotosha wananchi, lakini kwa lengo la kutaka Rais wetu aonekane dhaifu, hawezi kusimamia mambo na kwamba kuna upigaji. Kwa hiyo, maneno yamekuwa ni mengi sana katika Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nitoe angalizo kwa Wabunge hawa. tabia hii iweze kWisha na ife mara moja na ninaomba niwaambie Wabunge wageni ambao mmekuja ambao hamjui mambo ya humu Bungeni, leo hii mnaweza mkaona baadhi ya Wabunge wanapita kunong'ona ooh, kuna upigaji hapa, Wizara hii hiki na hiki; lakini nataka niwaambie, ikifika mwaka 2024 hamtaamini kama ndiyo hao. Kwa sababu kila atakayesimama ataipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo limekuwa likizungumzwa sana hapa na kaka yangu Mheshimiwa Sanga, jana amezungumza kuhusu suala zima kwenye sekta ya mbolea. Mtu anasimama hapa anasema kwamba yapo maeneo (upotoshaji wa makusudi kabisa), Serikali inaweza ikapata mbolea kwa bei rahisi ya Dola 300 kwa tani. Ni kitu ambacho hakipo. Sasa huu upotoshaji maana yake inakuwa ni nini? Kwa sababu mambo haya yanavyoendelea namna hii, matokeo yake tunakwenda kupeleka *wrong message* kwa wananchi wetu. Wananchi wetu kule watakuwa wanaona Serikali inashindwa kusimamia na Serikali haiumizwi na matumizi makubwa ya fedha za Serikali. Jambo ambalo ni baya sana sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba niwape moyo Waheshimiwa Mawaziri, hata Bunge lililopita, kuna Waziri alisimama hapa, Wizara ya Nishati sijui imefanya hivi, kila siku ukisimama unasikia. Kama ninyi mna mapendekezo mengine, kwa nini msiende huko Serikalini kusema? Kwa nini mmekuwa mnakaa mnaongea? Wako wengine, Mbunge akisimama hapa anaongea ovyo, unajua kabisa kwamba *ana-criticize,* unaona kabisa kwamba huyu yuko *genuine*, lakini wako wale wengine ambao unakuta wana mambo yao, hebu mshindwe na mlegee. Hatutaki kuona huo mchezo hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa naomba kusema, tumpe muda Rais wetu. Mama yetu huyu jamani amekaa kipindi kimoja, amefanya kazi nyingi sana, amefanya kazi kubwa sana. Watu wanasimama hapa, anasema, kwenye Jimbo langu sijui shule, kwenye Jimbo langu zahanati; lakini akitoka hapo anakwenda huko kunong'ona maneno ya ovyo maneno ya kipumbavu kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba lingine nimalizie kwenye suala zima la amani ya nchi yetu. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge, sisi wanasiasa dunia nzima chokochoko nyingi

machafuko na vita huwa vinaanzishwa na midomo yetu. Nasema hivyo kwa sababu wapo watu ambao wamepoteza maisha kwa sababu ya kauli moja ambayo ameongea mwanasiasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu ambao wameingia kwenye machafuko makubwa, wanahamahama duniani kwa sababu ya maneno ambayo wameongea wanasiasa, lakini wanasiasa wenyewe na hasa wakubwa wanakuwa wako salama. Kwa nini nasema namna hiyo? Wako viongozi wa kisiasa ndani ya Bunge pamoja na nje ya Bunge.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Sitaki taarifa na wewe!

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**T A A R I F A**

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima sana, natambua mchango mzuri wa dada yangu Mheshimiwa Lucy, lakini naomba nimpe taarifa kwamba Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumepitisha mara kadhaa matamko humu ndani ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa hiyo, naomba nimpe taarifa kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais. Kama yupo Mbunge ambaye anaongea hayo maneno huko nje, tutakaa kwenye vikao huko, lakini Bunge hili tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Lucy Mayenga, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kwanza nimwambie Mheshimiwa Mbunge aliyeongea, ameingia hapa Bungeni kwa mara ya kwanza. Bunge hili, sijasema Bunge lote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy, useme kwanza unaipokea au huipokei?

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa hii na nimesema kwamba sio Wabunge wote, ni baadhi ya Wabunge. Nina ushahidi kama mtahitaji ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee. Machafuko mengi ambayo yamekuwa yakitokea maeneo mbalimbali katika hii nchi, ni kwa sababu ya kauli za viongozi. Sasa nilikuwa naiomba Serikali hiki kinachoendelea kwenye hili sakata la Loliondo na ngorongoro…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. LUCY J. MAYENGA:** ….nilikuwa naomba Serikali iwe makini kuweza…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Sasa ni Kuhusu Utaratibu au ni Taarifa? Maana naona kuna wawili.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu haya, Mheshimiwa Musukuma.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mzungumzaji, dada yangu Mheshimiwa Lucy Mayenga haya mambo anayozungumza ni makubwa sana. Maana Wabunge humu tuko wengi, tunawakilisha wananchi wanaompenda Mheshimiwa Rais. Sasa kusema kuna watu Wabunge wanafanya hivi, tunafanya hivi, na ushahidi anao, halafu Kiti hakiwezi kumuomba, kwa sababu hili Bunge liko *live;* sasa wakitajwa, na sisi Wabunge tuwajue ili tuwaogope, maana sisi wengine tunamthamini Rais wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma ingawa hujataja kanuni ipi imevunjwa, lakini hilo analozungumza ni sahihi. Mheshimiwa Lucy naomba ujielekeze kwenye mchango na kama kuna watu wanafanya hivyo na una Ushahidi, basi inabidi upitie utaratibu ambao unafaa zaidi kuliko kuzungumza hadharani kama hivi, na Watanzania wanasikia, wakaona kwamba kuna Wabunge na ingewezekana labda wengi sana wanaharibu hayo mambo. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Wapo, wapo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy naomba uendelee.

**MHE. LUCY J. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. *Message* imefika, waifanyie kazi, ndiyo cha muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho nilikuwa nataka kusema kingine ni kuhusu suala zima la hiki kinachoendelea huko kuhusu mambo ya Loliondo na Ngorongoro. Wapo wanasiasa ambao wanaingilia hili suala, lakini wana maslahi. Naiomba Serikali isinyamaze kimya. Naomba Serikali i-*deal* na hawa wanasiasa ambao kwenye hili suala wana maslahi. Hatuwezi kunyamaziana

na mambo ya ovyo yakawa yanaendelea kwenye hii nchi. Haiwezekani, kwa sababu jambo hili likiendelea, mambo haya yanayoendelea huko yatashindikana, na vitu vyote…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. LUCY J. MAYENGA:** Ndio walewale, nilijua…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy kengele ilikuwa imelia ya mwisho.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. LUCY J. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Wafanyie kazi na mbadilike. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Lucy alikuwa ameshamaliza muda wake. Kengele ilikuwa imelia.

Tunaendelea. Nilimtaja Mheshimiwa Bonnah Kamoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Mtenga na Mheshimiwa Asia Mwadini ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika hii Wizara. Nitaendelea Mheshimiwa Lucy alipoishia. Naomba niongelee suala la asilimia 10 ambalo na wenzangu wameongelea sana. Namwomba Waziri asiitoe hii asilimia 10 kwa sababu, kwa sababu inawasaidia sana akina mama, mfano Mkoa wetu wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Dar es Salaam asilimia 90 ya watu wanaoishi Mkoa wa Dar es Salaam ni wafanyabiashara. Kama unavyojua, asilimia nne inaenda kwa akina mama, asilimia nne inaenda kwa vijana na asilimia mbili kwa walemavu. Asilimia nne inayoenda kwa vijana ni hawa vijana ambao wamemaliza vyuo na hawana kazi. Sasa tutakapowaondolea hii asilimia nne itakuwa kwamba tumewaumiza sana. Kuna vijana wengi ambao wanafaidika kutokana na hii asilimia nne ambayo wanaipata kutoka kwenye Manispaa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wengi sana ambao wanaendesha familia zao ni kutokana na hii asilimia 10 ambayo inapatikana kwenye Manispaa zetu. Nami nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala pamoja na Afisa Maendeleo Francisca Makoye, wanafanya kazi kubwa kuangalia Wilaya ya Ilala akina mama wanapata fedha hii asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tu katika Jimbo langu la Segerea, katika mwaka ambao umepita tu, watu ambao wamekopeshwa kutokana na hii asilimia 10 wamekopeshwa Shilingi bilioni 4.6 kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, tunaomba hii fedha isitolewe, inasaidia kuendesha maisha ya watu na pia inawatengenezea vijana ajira. Tuna vijana wengi ambao wamemaliza vyuo vikuu hawana ajira, na tumekuwa tukiwaomba kwamba mtu anayetafuta kazi, wakati anaendelea kutafuta kazi basi wajiunge vikundi waende kutafuta mikopo Manispaa. Mkisema kwamba muitoe hii asilimia 10 ikabaki hiyo ambayo mnaipeleka kwenye miundombinu, mtakuwa mmewaumiza sana vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuliongea ni suala la miundombinu hususan mradi wa *DMDP*. Tumeshakuja kwako Waziri Dkt. Mwigulu tukiongelea mradi wa

*DMDP*. Mkoa wa Dar es Salaam tunataka huko mbele uwe ni Mji wa biashara. Haiwezekani tukawa na mkoa ambao ni wa kibiashara lakini miundombinu yake mibovu. Kila nikisimama hapa huwa naongelea suala la *DMDP* na miundombinu. Miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam, ikinyesha mvua dakika 10, Dar es Salaam nzima inasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, asilimia 70 ya mapato ya Tanzania yanapatikana Dar es Salaam. Sasa ni kwa nini Wizara ya Miundombinu pamoja na Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu huu mradi wa *DMDP* bado haujaanza? Ndiyo mradi ambao tunautegemea sana na ndiyo unaoweza kutuokoa. Haiwezekani Mji wa biashara ukaonekana una miundombinu mibovu. Hata sasa hivi ukishuka pale Segerea Kata ya Kipawa, kitu cha kwanza kuona ni barabara mbovu. Tunahitaji tupate wawekezaji kutoka nje. Tutapataje wawekezaji na barabara hizo mbovu? Tumekaa sana na Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu tukiomba huu mradi uanze, tukaambiwa kwamba huu mradi utaanza mwezi wa Tatu, leo tuko mwezi wa Sita. Ameongea pale mwana-Dar es Salaam mwenzangu, mpaka sasa hivi hatujui huu mradi unaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mradi wa Mto Msimbazi. Mradi huu ilikuwa uanze mwezi wa Tatu mwaka huu 2022, wakasema tayari wameshapeleka Wakandarasi wako wanafanya *designing* na mambo mengine ya kitaalam, lakini mpaka sasa hivi hatujapata taarifa ni lini huu mradi wa Mto Msimbazi unaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, Mkoa wa Dar es Salaam mvua inanyesha saa yoyote, na kutokana na miundombinu mibovu maji yanaenda kwenye nyumba za watu. Kwa hiyo, nilitaka nijue, ni lini mradi wa Mto Msimbazi utaanza? Kwa sababu kuna nyumba nyingi sana zimeondoka kutokana na huu Mto Msimbazi. Kama ninavyochangia siku zote, ni kwamba,

Mto Msimbazi au maji yanayoingia kwenye nyumba za wananchi siyo kwa sababu wananchi wameufuata Mto Msimbazi, ni kutokana na miundombinu mibovu, na ule Mto kutokana na kutokufanyiwa matengenezo au marekebisho; ule mto umepanuka na mvua kidogo tu ikinyesha unaingia kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba, mliahidi mwaka 2021 kwamba mtaanza kujenga mwezi wa Tatu, umeshafika, na hakuna kinachoendelea. Mpaka sasa hivi sijajua ni kitu gani kinaendelea kutokana na huu Mto Msimbazi pamoja na mradi wa *DMDP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya masuala ya miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam ni muhimu sana, kwa sababu sisi tunavyotoka hapa, tunaenda kuwaahidi wananchi kwamba kuna hiki kitatengenezwa na hiki kitatengenezwa, lakini tukirudi hapa, kinaendelea kitu kinaitwa mchakato; tukitoka mchakato, tunaingia *process*. Hivi vitu haviishi! Watu wanasema kwamba Dar es Salaam inajengwa sana barabara, nataka niwakumbushe, Dar es Salaam ndiyo inayokusanya mapato asilimia 70 ya hili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakapopata barabara nzuri, na wafanyabiashara wetu watakapofanya kazi vizuri, ndiyo na fedha zitakapopatikana ili kwenda kujenga sehemu nyingine. Kwa hiyo, tunaomba Dar es Salaam Mheshimiwa Waziri aiangalie kwa macho mawili, kwa sababu, ndiyo Mji wa wafanyabiashara. Kama nilivyosema, asilimia 90 ya wakazi wa Dar es Salaam ni wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililokuwa nataka kuongelea ni kuhusiana na fidia ya wananchi. Leo siongelei tu fidia ya Kata ya Kipawa, kuna fidia mbalimbali. Unapoenda kuchukua sehemu ya mtu ambaye alikuwa amejenga nyumba

yake, ardhi yake, unaichukua, unakaa nayo kwa kipindi cha miaka 10 bila kumlipa yule mtu, unamletea umasikini. Tuna sehemu nyingi ambazo Serikali imechukua na imewaahidi wananchi itawalipa, mmeweka miundombinu yenu, wananchi wanashindwa kufanya kazi, inabaki wananchi wanaendelea kudai. Yaani wananchi wanatoka Dar es Salaam, wanakuja Dodoma. Sasa hii Serikali ni kuwatia umasikini wananchi. Tunaomba Mheshimiwa Waziri hii tabia muache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnataka kuchukua eneo la mtu, basi mpeni fedha ili yeye aondoke na ninyi mchukue ile sehemu. Kama mlivyofanya kwenye Kata ya Kipawa *Airport,* mpaka sasa hivi, tangu mwaka 1997 hamjawalipa wale wananchi. Halafu pia mkaenda mkaweka na jiwe lenu la msingi, yaani kuonesha kwamba ninyi mmeshaichukua ile ardhi kabla hamjawalipa wale wananchi. Wale watu wameendelea kuteseka. *(Makofi)*

Mheshi,iwa Mwenyekiti, sasa juzi nimeuliza swali, Mheshimiwa Waziri akasema kwamba wale wananchi wanafanyiwa tathmini upya. Nami nimefurahi kwa sababu wanafanyiwa tathmini upya, na wakasema kwamba wameshapeleka barua Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *last week* nimekwenda Dar es Salaam, hakuna barua yoyote ambayo imekwenda Jiji. Kwa hiyo, ninachokiomba Mheshimiwa Waziri utakaposimama, nilikuwa naomba Waziri husika aweze kuniambia hiyo barua ya wananchi wa Kata ya Kipawa Mtaa wa Kipunguni imepelekwa wapi, ili hao wananchi waweze kujua wanaanza lini kulipwa? *(Makofi)*

*(Hapa kengele iliia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo la muhimu sana. Jambo lingine la kuongelea ni kuhusiana na wafanyabiashara wa Mkoa wa Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kamoli, kengele ya pili ilikuwa imeshalia.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bonnah Kamoli. Mheshimiwa Hassan Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Mwadini na Mheshimiwa Joseph Mkundi wajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini nami niungane na wenzangu kumshukuru Rais wetu mpendwa, kwa kazi kubwa anazozifanya za kutuletea maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wetu kwa bajeti nzuri ambayo ina matumaini kwa wananchi. Nadhani bajeti hii ikitekelezwa vizuri, inakwenda kutatua matatizo ya wananchi. Kabla sijaanza kuchangia, mimi ni Mwenyekiti wa Maadili wa Wabunge wa CCM hapa Bungeni. Napenda kulisema hili; Mbunge mwenzetu aliyetoka kuzungumza juu ya baadhi ya Wabunge kutokumuunga mkono Rais, hiki ni kitu kimoja kibaya sana na hapa haikuwa mahali pake kukizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna moja au nyingine, Rais huyu amemgusa Mbunge kila mmoja kwenye Jimbo lake, na kwa hali ya kawaida, sidhani kama kuna Mbunge humu ndani inawezekana akatoka huko nje akamshambulia Rais. Haya nayazungumza, kesho tutasikia magazeti mengi sana yanaandika hicho kitu. Ambacho kinakwenda kufanyika sasa, ni kuwachonganisha Wabunge na Rais wao. Sasa hili siyo jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Wabunge, kila mwenye shida ambayo inahusiana na suala zima la kiongozi, basi mtuone. Katika Kamati yetu tumeshaita Wabunge zaidi ya 14 humu ndani, lakini kwenye mambo tofauti, siyo masuala ambayo yanamhusu Rais. Kila tulipokaa nao hao Wabunge, hali ipo shwari na tunaendelea na Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendelee na mchango wangu. Kwanza, nataka nizungumze kuhusu mapato. Hatuwezi tukaizungumzia bajeti, kila mwaka tunapokuja tunapandisha vitu bei, kila mwaka, lakini *still* tunavyo vitu vyetu ambavyo viko tayari. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake amezungumza, kuna baadhi ya watumishi ambao wanahusika na ukusanyaji wa kodi, wanamwangusha. Hili Mheshimiwa Waziri tunakupongeza kwa kuliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumza, yuko mtu mmoja alipeleka korosho nje lakini kwenye ushuru aliotozwa ametozwa ushuru wa mbaazi. Sasa huu ni upotoshaji, lakini pia ni wizi mkubwa ambao unaendelea kufanyika. Kwa hiyo, twende tusimamie rasilimali zetu. Hatuna shida ya kufika mahali sasa tunasema tuhangaike na viwanda vya pipi, tupandishe bei kwenye ushuru wa pipi wakati bado tuna rasilimali ambazo tunashindwa kuzisimamia ili ziweze kuleta tija zaidi. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna watu wanaagiza magari nje, unaagiza gari *IST* kwa gharama ya milioni tatu, linaposhuka bandarini ushuru wake *TRA* ni milioni sita. Tunakwenda wapi? Kama tungepunguza bei ya ushuru, wangapi wangeagiza hayo magari *IST* na yangekuja kwa wingi gani na sisi tungekusanya kodi ya aina gani? Sasa kuna vitu vingine inawezekana kwamba, tunasema kwamba, tunapandisha ushuru ili tupate kodi kubwa kumbe tunakwenda kujiangamiza wenyewe. Ushauri wangu kwa Serikali, katika vyanzo vyote vya kodi tuangalie *population* ya

bidhaa ambayo inakuja kwetu, tukipunguza kodi bidhaa hizi zitakuja kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine la wamachinga limezungumzwa sana. Asilimia kumi ambayo tunachangia sisi kutoka kwenye halmashauri zetu, fedha hizi ni msaada mkubwa sana kwa wananchi wetu. Leo tunapoamua kutoa asilimia tano kuipeleka kwenye huduma nyingine kwa sababu, ile asilimia kumi hata Wabunge wengi wamesema haitoshi kwa jinsi ambavyo tumewapa mikopo wananchi wetu, haitoshi kabisa. Sasa naiomba Serikali asilimia kumi hii ibaki palepale ilipo, lakini kama kuna uwezekano wa kuitengenzea sheria tena, tuongeze fedha katika hii asilimia kumi, ni hela ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu tunaondoaondoa na leo hapa nimepigiwa simu kuna maaskari huko wanafukuza na bunduki, wanafukuza wananchi kwenye maeneo. Sisi tunalo eneo pale nyuma ya Benki Kuu, eneo lile linaota nyasi, eneo lile lina vichaka zaidi ya eka 18, liko pori mjini kwenye manispaa; nimepiga kelele hili eneo tuwajengee hawa wamachinga wakae hapa waache kazi ya kutembeatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapomtembeza mmachinga barabarani athari zake nini? Tunakosa kukusanya kodi. Hatukusanyi kodi kwa sababu, hakuna mmachinga anayetoa risiti, lakini mmachinga anapotembea barabarani hana *insurance* yoyote. Leo tunazungumza tunataka tuwape mikopo, watu wa benki ukiingia kwenye mikopo wanakwambia tunataka hati ya nyumba au ofisi yako iko wapi, mkataba wako uko wapi? Kwa hiyo, hili nalo tuliangalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wafanyabiashara wanakopa kwenye benki na hawa watu wanapokopa mikopo yao wanaweza wakalipa takribani zaidi ya asilimia 80. Anaposhindwa kulipa japo ameshalipa zaidi ya asilimia 80, watu wa benki

wanaingia wananyang'anya nyumba za watu, wanauza nyumba. Hili ni hatari sana kwa wananchi wetu na hii ni kwa nchi nzima, wako watu wamekaa na pesa zao, kazi yao wao ku-*coordinate* na watu wa benki, nyumba gani itauzwa kesho, keshokutwa. Sasa hatuwasaidii wananchi wetu, tunakwenda kuwaharibu wananchi wetu. Hili nalo naomba nalo tufike mahali tuliangalie, lakini tuwasaidie wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie pia kwenye eneo moja la ujengaji wa reli yetu. Kwanza niishukuru Serikali, kwa kweli inajenga reli, lakini nataka niseme jambo moja ambalo ni ushauri kwa Serikali. Tulikuwa tuna *reli* ya *TAZARA,* reli hii ilijengwa na Mchina. Reli ya *TAZARA* hatukukata kipande kipande, Mchina alijenga mwanzo mpaka mwisho, lakini tukawa na reli ya kati ilijengwa na Wajerumani. Wajerumani wale walijenga reli ile mwanzo mpaka mwisho. Ushauri wangu kwa Serikali hebu tuache kuingia kwenye kuweka wakandarasi zaidi ya watatu, wanne kwenye reli kwa usalama wa Taifa letu. Reli hii ni kitu muhimu sana hatuwezi kuweka zaidi ya watatu, wanne wanakwenda kujenga reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwenye dhana ya usalama wa nchi, hebu turudi sasa tuangalie ni mkandarasi gani bora, yeye anawezekana akaingia *joint venture* na kampuni nyingine yoyote ikamsaidia kwenda kujenga. Kwa hili natoa mfano, tunazo barabara zetu za lami. Mimi natoka Mtwara, kule Mtwara ukiingia pale Lindi walijenga pale *Kharafi,* lakini kipande alichojenga *Kharafi* cha lami ni mkandarasi bora, mpaka leo hakijaharibika, lakini vipande vingine hivyohivyo walivyojenga kwa muda huohuo barabara hazipitiki na kila siku ziko kwenye *maintenance*. Sasa ombi langu kwa Serikali hebu turudi tuangalie mkandarasi mmoja anaweza akatusaidia nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie vituo vya afya. Kwangu niishukuru Serikali tumepata kituo cha afya na

kimeshaisha. Niombe katika vituo hivi ambavyo vinajengwa, kwenye suala la Madaktari na Wauguzi Serikali watoe kipaumbele tuweze sasa kupata Wauguzi na Madaktari kwa sababu, majengo ni mazuri yana kila jambo ndani mle. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hassan Mtenga,. Tunaendelea na Mheshimiwa Asya Mwadini, Mheshimiwa Joseph Mkundi na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo wajiandae.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukisoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 4, katika masuala mazima ya mambo yanayohusu Muungano na pia kuna masuala ya kodi na mapato. Maana yake kodi na mapato ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano bado ni sehemu ya Muungano, maana yake Wazanzibari wamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya ukusanyaji wa kodi kwa wawekezaji waliokuwepo Zanzibar. Zanzibar kuna mamlaka mbili za ukusanyaji wa kodi kwa wawekezaji wetu, kuna *ZRB* ambayo ni Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar, lakini pia kuna *TRA;* Bodi ya Mapato, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wetu ambao wapo Zanzibar wanalilalamikia suala hili sana na ni kwa sababu, ukiangalia halina tija na huelewi ni kwa sababu kwa nini vyombo viwili vinakusanya kodi kwa wakati mmoja kwenye nchi moja. Wawekezaji wamekuwa wanatengeneza mianya ya kutengeneza rushwa ili waweze kupona waweze kufanya biashara zao. Wawekezaji pia wamekuwa wanafunga hoteli na

taasisi zao za biashara kutokana na changamoto hii. Duniani, nchi moja haiwezi kukusanywa kodi na vyombo viwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, uchumi wa zanzibar unaporomoka kwa sababu ya changamoto hii. Ushauri wangu kwa Serikali, kuna haja sasa Mamlaka ya *TRA* ikasimishe madaraka kwa Mamlaka ya *ZRB* ili waweze kukusanya kodi, *then* watakutana juu kwenye *level* ya uongozi na kutambua asilimia ngapi ya kodi iliyokusanywa inakwenda kwenye Mfuko wa Muungano na asilimia ngapi itakwenda kwa Wazanzibari wahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wetu wanatulalamikia sana. Tuna Ushahidi, kuna kodi ambazo huwa zinatoka za misamaha, mwekezaji anakuja leo anafungua hoteli, anapewa ile miaka mitano ya msamaha wa kodi, akimaliza miaka mitano kwa sababu ya kukimbia hizi kodi mbili anarudi tena anabadilisha jina la hoteli na kampuni. Mwekezaji anaweza akawa ni huyohuyo mmoja. Hili jambo halina afya, hatuwezi kuwa na wawekezaji wakati mama kila siku anazungumza, lazima tuweke mazingira bora na rafiki kwa wawekezaji wetu na kuwe na kodi ambazo zitamfanya mwekezaji awe anamtafuta yule anayepokea kodi mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na vita vikubwa wawekezaji ambao wako Zanzibar wanalalamika sana. Kwa hiyo, niishauri sana Serikali waliangalie suala hili, Mamlaka ya Zanzibar ya *ZRB* na Mamlaka ya *TRA* kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lazima wakalifanyie utaratibu haraka, ili tusipoteze wawekezaji Zanzibar, tukuze uchumi wetu, tunahitaji mapato, lakini na ajira kwa watoto wetu ambao wako Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia bajeti ya mwaka 2022/2023, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania *(TRA)* ilipanga kukusanya trilioni 23, lakini wamefanikiwa kukusanya trilioni 17,

kwa hiyo, maana yake kuna trilioni nne zinaeleaelea hivi, hazijulikani zilikuwa wapi. Changamoto za ulipaji wa kodi kwenye Taifa hili zimekuwa sugu, lazima zirekebishwe, ili tuweze kukusanya kodi vizuri na kuweza kuleta tija katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Sekta ya Utalii. Nimesoma hotuba ya Waziri, ukurasa 56, *paragraph* ya 68, amezungumza kwamba, *the Royal Tour* ambayo imelenga kuonesha uwezo wa fursa za huku Tanzania katika sekta ya utalii na uwekezaji, lakini pia akawataka na wana-*diaspora* waje Tanzania kuwekeza. Tunapozungumza uwekezaji katika sekta ya utalii hatuwezi kuiacha ardhi, mwekezaji anapokuja katika Taifa hili lazima awe na ardhi ambayo haina mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza kelele zilizopo Ngorongoro, leo tunazungumza baadhi ya hifadhi na wananchi wanavamiana. Tume yetu ya Mipango ya Ardhi kwa mwaka huu wamehitaji bilioni 10 ili waweze kupanga na kupima na kuweka ardhi katika mazingira salama, leo wamekwenda kuwapa bilioni moja. Halafu Mheshimiwa Waziri alipokuja ku-*wind up* hapa aliliambia Bunge hili kuna mkopo ambao utakuja ndio utaipa hiyo bilioni tisa. Hivi kweli tunategemea mkopo ndio uende ukatupimie ardhi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni aibu, yaani ni aibu sana. Mama anazunguka duniani, mama wa watu hapati hata muda wa kunywa *juice* na wajukuu zake, leo yuko Ujerumani, kesho yuko Dubai, keshokutwa sijui yuko wapi? Mama hatulii anatafuta wawekezaji, anatutafutia kula Watanzania, lakini kama yeye anaenda kuhangaika huku na wengine wanatoboa mifuko, kuna jambo ambalo tutakwenda kufanikiwa hapa? Lazima ardhi ipimwe ili Taifa hili liweze kuleta uchumi. Ardhi ikipimwa vizuri maana yake tutaweza kupata mapato, tutatengeneza ajira, wawekezaji watawekeza bila bughudha yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta hiyo hiyo ya utalii nilisoma pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika masuala ya tozo, nimesikitika sana. Leo tunasema tunahitaji kuwa na wageni na kuwa na utalii ulio bora, lakini tunavyozungumza utalii hatuwezi kumwacha mgeni wala muwekezaji ambaye yupo hapa. Hatuwezi kumuacha mwekezaji ambaye yuko hapa ni kwa sababu, sekta hii yani inakua kupitia *private sector.* Sasa leo wameweka tozo ya *VAT* kwenye ndege ndogondogo ambazo zinapaswa zitue kwenye viwanja vidogo vidogo kwa ajili ya utalii wa uwindaji, tutaweza kufika kweli? Kama sisi tunataka ku-*compete,* wenzetu Kenya wametoa…

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asya, Taarifa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na mchango mzuri sana wa Mheshimiwa Mbunge, kuna eneo moja ambalo nataka tuliweke vizuri; juu ya mamlaka mbili za makusanyo ya mapato katika nchi, aliyoiita ni nchi moja. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema Tanzania ni Nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini Katiba ya Zanzibar inasema Zanzibar ni Nchi na ina Serikali yake Kikatiba, ina Baraza lake la Wawakilishi linalofanya kazi ya kuisimamia na kuishauri Serikali kama sisi tunavyofanya kwenye ngazi ya Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali hizi mbili kuwa na mamlaka za ukusanyaji wa kodi ni kutekeleza mamlaka ya Kikatiba kwa upande wa Zanzibar na mamlaka ya Kikatiba kwa upande wa Tanzania Bara, maana nao watahitaji kuwa na fedha za kuendesha Serikali ya Zanzibar na katika ngazi ya Muungano tunahitaji kuwa na chanzo cha mapato. Kwa hiyo, nataka niliweke hili bayana ili lisilete mkanganyiko kwa sababu, Katiba

zetu zinasema hivyo na mimi siji hapa kuleta tafsiri ya Katiba yoyote katika hizo, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asya unapokea hiyo taarifa?

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia mchango wangu, nimezungumza utalii wa ndege ndogondogo ambao unafanywa ndani ya Tanzania kwa wawekezaji wetu na ni lazima tuondoshe kodi ili tuweze kuweka mazingira bora. Wenzetu Kenya wameitoa hii *VAT* kwa hiyo, wawekezaji hawataweza kuja hapa watakwenda Kenya ili waweze kuwekeza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwenye suala zima ambalo mwenzangu, kaka yangu Mheshimiwa Mtenga alilizungumza, kuhusu mikopo ya wafanyabiashara wetu ambao wako nchini na watu wa benki, imekuwa ni changamoto kubwa. Watu wetu wanajaribu kujipambanua kibiashara, ukiangalia wafanyabiashara walio wengi wamepoteza maisha, wengine wame-*paralyze,* wengine wamepata matatizo mbalimbali wanashindwa kusomesha watoto wao ni kwa sababu ya benki hizi. Wanachukua mikopo, wanakubaliana, kabla ya kumaliza kulipa mikopo labda mtu amepata changamoto ya biashara, benki hazina simile ya kuwastahamilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nishauri Wizara ikae na watu wa benki wapitie tena kanuni na taratibu na sheria za benki, ili tuwanusuru wafanyabiashara wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asya Mwadini. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mkundi na Mheshimiwa Profesa.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake, kwa uongozi wake thabiti na imara sana na kwa namna anavyowatumikia wananchio wa Taifa hili. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote kwa namna walivyobeba maono ya Mheshimiwa Rais na kuwasilisha bajeti katika Bunge lako Tukufu, bajeti ambayo ni moja kati ya bajeti bora ambazo nimeshuhudia nikiwa Bungeni hapa. Jukumu letu ni kutoa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitachangia kwenye maeneo kama manne iwapo muda utaniruhusu na kwa kuanzia nitaanza na eneo la elimu. Kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 51, ameongelea maamuzi ya Serikali kuanzisha dirisha kupitia *TASAF,* kusaidia watoto ambao hawana uwezo wa kulipa ada. Ni jambo jema, lakini kwenye eneo hili ningeshauri watu wanaonufaika na Mfuko wa *TASAF* haujajumuisha wale wote ambao wangestahili kufaidika na Mfuko ule. Kwa mfano, kuna viongozi wa Serikali za Vijiji, kuna Viongozi wa Vyama vya Siasa, haijalishi kama kiuchumi hayuko vizuri, lakini kwa sifa hiyo tu ya kuwa kiongozi hanufaiki na Mfuko wa *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo tafsiri yake ni kwamba, watoto ambao kutokana na baba yao kutokuwa na uwezo kiuchumi hawawezi kunufaika na Mfuko huu. Kwa hiyo, ningeshauri kwenye eneo hili iangaliwe namna nyingine bora ambayo itabainisha

watoto ambao watanufaika na mfuko huu na dirisha hili la *TASAF* ambapo kwa kuanzia Mheshimiwa Waziri amesema unaweka bilioni nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la elimu vilevile niipongeze Serikali kwa kufuta ada ya kidato cha tano na cha sita. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huu, lakini niombe pamoja na kuondoa ada bado sehemu kubwa ya wanafunzi wetu na vijana wetu wanaathirika sana na michango mbalimbali. Kwa hiyo, ningeshauri Serikali iangalie namna bora ya kudhibiti michango hii na kuwe na chombo kama ni Wizara ya Elimu na chombo kingine chochote ili kuainisha ni michango ipi ambayo itapaswa kutozwa kwenye shule zetu, isiwe kikwazo kwa watoto wanaoenda kupata elimu kupata yale manufaa ya kufuta ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mipango yetu, sera zetu zinapaswa kujibu matatizo ya vijana wa Taifa hili, vilevile kwa dhamira hii njema ya kufuta ada ya kidato cha tano na cha sita, lakini na kuweka dirisha hili kupitia *TASAF,* bado kuna umuhimu wa Serikali kuona haja ya kugharamia ada za vijana wanaoingia kwenye vyuo vya kati, Vyuo vya *VETA,* tunajenga vyuo vingi sasa hivi, kuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, ni daraja ambalo linatengeneza vijana wengi sana ambao wanaingia kwenye soko la ajira, lakini wengi wanashindwa kuendelea kwa kukosa pesa za kugharamia mafunzo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaishauri Serikali ione umuhimu vilevile wa kugharamia *level* hii ya kati ambayo ndiyo ya watenda kazi ambao tunawaingiza kwenye soko la ajira lakini vilevile kuanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na baadae kuwa walipa kodi wazuri na kuweza kusaidia Taifa letu kujijenga kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni eneo la utalii. Ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa kutengeneza filamu ya *Royal Tour*. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ni njema na ina matokeo chanya, kwa mujibu wa Ilani yetu ya uchaguzi ni kweli na kwa kupitia *Royal Tour* itatusaidia sana, lakini nishauri pamoja na dhamira hii njema ya Mheshimiwa Rais ambapo ameonesha njia ametengeneza *skelton* wajibu wetu sisi Wizara nyingine nyingi, taasisi na watu binafsi ni kujaza nyama sasa kwenye *skelton* hii ili hii *Royal Tour* iwe na taswira iwe na *impact* chanya kwenye eneo la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo vivutio vingi sana vya utalii lakini bado hatujaweza kuvitangaza ni jukumu sasa la Wizara mbalimbali Wizara ya Uwekezaji, Wizara ya TAMISEMI kwenye miundombinu, Wizara ya Utalii yenyewe na maeneo mengine yote ili kuweza sasa ku-*compliment* hiki alichokifanya Mheshimiwa Rais ili kiweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kuna vivutio vingi kwa mfano mimi kwenye eneo langu la Ukerewe kuna vivutio vingi. Kuna jiwe linacheza kule, kuna *beach* ya Rubya kuna mapango ya Andebezi ambayo tokea shule za msingi tunasoma na maeneo mengine ninaamini hata maeneo mengine kuna vivutio vingi vya utalii lakini bado havijaweza kutambulika na kutengenezewa miundombinu ili hawa sasa tunaowashawishi waje kutembelea Taifa letu waweze kuvijua na kuweza kuvitembelea. Kwa hiyo, tu-*compliment* hii *Royal Tour* sisi kama Wabunge lakini na taasisi nyingine zote ili angalau iweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo ningetamani kuchangia ni eneo la kilimo. Ninaipongeza Serikali kwa mara ya kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais bajeti ya Wizara ya Kilimo imepanda kutoka Bilioni 294 mpaka Bilioni 954, haya ni mapinduzi makubwa sana na kwa mujibu wa hotuba ya

Mheshimiwa Waziri lengo ni kuongeza uzalishaji kwenye kilimo cha umwagiliaji kutoka asilimia 10 mpaka asilimia 50, ninaamini tunaweza tukafikia lengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *trend* ya kukua kwa uzalishaji kwenye eneo la kilimo imekuwa siyo nzuri sana. Ukiangalia kwa mfano, mwaka jana kwenye Pato la Taifa kilimo kimechangia asilimia 26.4 mwaka jana tukashuka mpaka 26.1 lakini kwa haya mapinduzi na mtizamo wa Serikali sasa kuongeza bajeti, ninaamini tutaenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuweka nguvu kwenye kilimo hiki cha umwagiliaji ninaamini tuna maeneo ambayo tunaweza tukayatumia tuna-*quick wins* nyingi sana, ni vizuri tukaangalia sasa maeneo ambayo tunaweza tukawekeza kidogo kwa kuanzia lakini tukapata tija hasa kwenye maeneo ambayo yanazungukwa na maji, kuna vyanzo vya maji tayari badala ya kwenda kwenye maeneo ambayo tunahitaji kuweka uwekezaji mkubwa, kuna maeneo yanayozungukwa kwa mfano na maziwa, yanazungukwa na mito tunaweza tukawekeza kwa kuanzia na kukawa na matokeo chanya kwa sababu tayari kuna vitu vya kuanzia kuna chanzo cha maji. Sisi Ukerewe pale kwa mfano, tuna hekta zaidi ya 2000 ambazo tungeweza kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji tukapata mavuno mengi sana mavuno makubwa, sambamba na Ukerewe lakini kuna maeneo mengine vilevile yana taswira kama hiyo, ni vizuri tukaangalia maeneo haya kwa kuanzia tukawekeza tukaweza kupata tija kwenye eneo hili la umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunawekeza nguvu kubwa kwenye kilimo cha umwagiliaji ni lazima tuangalie tumejiandaaje kwa sababu tumewekeza lazima tutapata matokeo chanya, tutapata mavuno mengi, tumejiandaaje sasa kupata soko la mavuno haya ambayo tutayapata kutokana na kilimo hiki cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri siyo vibaya Serikali vilevile ikatengeneza matajiri wazalendo kwenye Taifa hili, ikatengeneza watu ambao inaweza kuwatengenezea njia, kuwatafutia masoko ikawapa mitaji ili wakiwa wazalishaji wazuri na wakawa wametengenezewa masoko wakaweza ku-*supply* mavuno hayo ambayo tutakuwa tunayapata. Kwa sababu moja kati ya changamoto ambazo tumekuwa nazo kwenye Taifa hili ni kwamba tunazalisha chakula, tunapata masoko nje ya nchi, lakini sasa kunakuwa hakuna *consistence* ya uzalishaji wa mazao yale, kitu ambacho kinapelekea wale tunaowasambazia bidhaa zile wanakata tamaa na kuingia mikataba na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kulea watu wetu, tukawapa mitaji, tukawajengea mazingira wakawa wazalishaji wazuri, ina maana itatusaidia hata kuweza kupata masoko ya uhakika lakini tukaweza kuwasambazia na kusaidia Taifa letu kwenye kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la mifugo na uvuvi ninaipongeza Serikali kuongeza bajeti kutoka Bilioni 100 mpaka Bilioni 268, kwenye eneo la uvuvi pekee imeongezeka karibu Bilioni 176. Ninaendelea kuisisitiza Serikali iwekeze nguvu kwenye ufugaji wa Samaki kupitia vizimba, yatakuwa mapinduzi makubwa sana na kwenye eneo hili, itasaidia hata ajira kwa vijana wetu ambao tumekuwa tunawasemea ili waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nne na la mwisho ni kwenye eneo la ufanisi wa miradi ya maendeleo. Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 21 umeongelea juu ya eneo hili, ukasema Mheshimiwa Rais amekuelekeza kuangalia upya taratibu za ununuzi na thamani ya fedha kwenye miradi ya maendeleo, ni kweli tunapoteza pesa nyingi sana kwenye eneo hili, wamesema

wachangiaji wengine kama tutaangalia vizuri kwenye eneo hili itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano kwenye eneo langu la Ukerewe, mwaka jana nashukuru tumepata pesa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya lakini kuna sintofahamu namna gani mradi huu unatekelezwa, ni vizuri kwenye eneo hili Serikali ikasimamia kwa makini, tunapoteza pesa nyingi sana hasa kwenye Halmashauri zetu kwa sababu ya mifumo hii kwa kutumia sheria zetu za manunuzi, kwa hiyo, kama tutaliangalia vizuri jambo hili itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mkundi tunamalizia na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii, naomba nichangie mambo manne kama muda ukiniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwanza ni umuhimu wa bajeti umuhimu wa hotuba ya hali ya uchumi, ni hotuba muhimu sana kwa sababu ndiyo inayotuonesha uwezo wetu wa kiuchumi na uwezo wetu wa mapato ili tunapopanga matumizi tujue nguvu yetu iko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ndiyo hotuba ambayo inatupa vipaumbele vya Kitaifa, changamoto tu ni kwamba Waziri wa Mipango ndiye huyo huyo ni Waziri wa Fedha, kawaida Waziri wa Fedha ana mambo mengi ndiyo maana kitabu chake ni kikubwa wakati ile hotuba ya mipango ni kidogo, kwa sababu ina *concentrate* na mambo machache. Waziri wa Fedha anataka ikiwezekana fedha zote za nje ziingie Serikalini, yaani fedha zote

katika nchi hii awe nazo yeye na ikiwezekana mahitaji yote ayamalize leo, ndiyo maana utaona ikisomwa humu ndani kuna mambo mengi unasoma unakutana na kiswahili kitumike kwenye usaili, unaelewa ni jambo jema kubwa na tukalipigia na makofi ni jambo zuri, lakini yote hii ni kwa sababu Waziri wa Fedha ana mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *of course* nilikuwa nasoma nikasema dhima yetu ya mpango wetu wa maendeleo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu, nadhani kisera ni muhimu kuwasisitiza watoto wa Kitanzania na Watanzania ili waweze kushindana, wajue vizuri Kiswahili, wajue vizuri Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakubaliana hapa tena Waziri anafahamu, tumeshafungua soko la ajira *free movement of labor,* sasa watakapoenda kule Uganda kufanya *interview* watu wetu inabidi na wenyewe washindane kwa hiyo, hili ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na hiyo changamoto ushauri ni kwamba pengine Bunge hili linaweza likaishauri mamlaka lione umuhimu tena wa kutenganisha hizi sekta mbili, za mipango na fedha. Nadhani tulipoandaa ile dira yetu ya mwaka 2025 ukiisoma ndiyo maana aliyesaini pale, hakusaini Waziri wa Fedha wakati huo Mheshimiwa Daniel Yona alisaini Mheshimiwa Nassor Malocho aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango, nadhani hili kuna haja ya kulifikiria tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu tujielekeze wenyewe na kujishauri pengine kuna haja hii hotuba ya hali ya uchumi ikatolewa mapema kabla sekta hazijaanza kuwasilisha bajeti, ili sasa wanavyokuja kuwasilisha bajeti za kisekta tuone hizo sekta ambazo zinawasilishwa kama zinaendana na hali yetu ya uchumi

na vipaumbele ambavyo tunavyo *and then,* siku hii saa kumi ije bajeti ya *National Budget* ndiyo tuipokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kodi. Katika eneo la kodi nataka nianze kwanza kuwapongeza wafanyakazi wa Tanzania wanaoiongoza nchi hii siyo kwenye utumishi tu, lakini pia kwenye suala la mapato. Ukisoma takwimu za *TRA* wafanyakazi wa Tanzania ndiyo wanaoongoza kulipa *income taxes,* wanawazidi *business income tax,* wanawazidi mpaka *cooperation tax,* yaani ile tunayosema *large tax payers* hawawafikii wafanyakazi wa Tanzania. Wafanyakazi wa nchi hii wanalipa, ukisoma zile takwimu 12.3 *percent* ya makusanyo yote ya *TRA* ni *pay as you earn,* wafanyakazi wa Tanzania ukisoma zile za juzi 2.2 trillion shillings kutoka kwa wafanyakazi. Wafanyakazi wa nchi hii waheshimiwe, wanafanyakazi kubwa, tunawashukuru sana kwa mchango ambao wanaoutoa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi vilevile kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam, ukisoma takwimu za *TRA* asilimia 79 ya makusanyo yote ya kodi yamekusanywa kupitia Dar es Salaam, Dar es Salaam *is the largest tax collection center in the country*. Tunazungumzia Trilioni 13.9 kati ya Trilioni 17.6 ahsanteni sana Mkoa wa Dar es Salaam. Pia ukiangalia kwa maana ya wananchi wanaolipa kodi, asilimia 11 ya kodi zote za nchi hii zinalipwa na Mikoa Mitatu ya kikodi kwa maana ya Ilala, Kinondoni na Temeke *of course* kwenye Kinondoni pia pale Ubungo ipo, usisahau Ubungo ipo ndani ya Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa tunaozungumzia Trilioni 1.996, Mikoa mingine yote ukijumlisha wanalipa kodi Trilioni 1.921. Kwa hiyo, makusanyo ya Mikoa Mitatu ya kikodi Dar es Salaam inazidi Mikoa yote ya Tanzania ukijumlisha. Wananchi wa Dar es Salaam shikamooni sana, tunawashukuru sana kwa kuchangia. Nataka niwaambie shukrani za Serikali ya CCM….

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Stella Manyanya.

**T A A R I F A**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza namshukuru Profesa kwa mchango mzuri lakini naomba nimpe taarifa moja, sisi ambao tunatoka kwenye maeneo yasiyolipa kodi kiasi hicho siyo kwamba hatutaki, lakini uwekezaji mkubwa umefanyika kwenye maeneo hayo na lazima mlipe hizo kodi, ndiyo maana tunaomba sasa nchi, Serikali iangalie na maeneo mengine ili na sisi tuweze kuchangia kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siwezi kukataa taarifa ya Dada yangu naipokea tu hata kama siijui sana, hiyo naipokea haina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* yangu ni hapo hapo kwamba nataka nichukue nafasi hii kuwahakikishia wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam Serikali ya Chama cha Mapinduzi hii

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo *Chief Whip* anataka kuzungumza.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi ni shabiki wa kusikiliza michango ya Profesa, ili tuweke mambo sawasawa hapa, hizi trilioni 13.9 zilizokusanywa na Dar es Salaam, Da es Salaam siyo wazalishaji, wanaozalisha wapo Mikoani, ndiyo maana asilimia 90 ya magari yetu ya mizigo, yote yametizama Dar es Salaam, tukiziba hizi barabara Dar es Salaam mtakufa njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo wamezalisha Dodoma, wamezalisha Mikoa yote nilitaka kumpa taarifa tu hiyo ili Watanzania wengine wasije wakajiona hawa mchango kwa nchi yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo unaipokea taarifa?

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Taarifa yake haina shida naipokea, mambo ya kuzingatia ni mawili nimeweka takwimu mbili na naomba unitunzie muda wangu, takwimu mbili za msingi za kuzingatia. Dar es Salaam kama *collection center* ndiyo hiyo Trilioni 13.9, hizo maana yake Watanzania wote wamechangia, ikiwemo *airport*, ikiwemo bandari, ile ni bandari ya wananchi wote wa Tanzania, kwa hiyo, hiyo ni Watanzania wote mpaka wa Singida na Iramba wamechangia hilo halina shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna takwimu ya pili ambayo ni shukrani kwa Mkoa wa Dar es Salaam ni wananchi ambao wamechangia 1.996 *trillion* wananchi wa Ilala, Kinondoni na Temeke, hawa ndiyo nawalinganisha na wengine. Sawa hawa

Mheshimiwa Waziri hawa watatu hawa, wamekusanya kuliko nchi nzima ukijumlisha, wanastahili shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, nataka niwahakikishie wananchi wa Dar es Salaam kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi zile ahadi zake za kujenga barabara za mitaani itatekeleza ili mkusanye zaidi fedha. Nataka niwaambie Tarehe 31 Mei mwaka 2022, Mawaziri watatu walikutana na Wabunge Wabunge wa Dar es Salaam wakiongozwa na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, pamoja na Waziri wa Ujenzi na wametuhakikishia kwamba mradi wa *DMDP* upo, zile barabara zitajengwa na akitoa ahadi Mnyiramba huwa havunji, kwa hiyo hili litakwenda vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, nataka nipongeze *TRA* kwa kazi nzuri. Sisi tumekaa hapa tunachangia vizuri kwa sababu kuna watu wamekusanya mapato tukalipwa ambavyo tunalipwa na utaratibu wetu ukakamilika, *TRA* ahsanteni sana. Pamoja na hayo wameshasema Waheshimiwa Wabunge hapa tunachangamoto kwa kweli, bado tunakusanya kidogo sana! Kwa hapa *East Africa* sisi ndiyo tuko chini, wote tumewazidi *DRC* tu ambao wamejiunga juzi, lakini mpaka Burundi wametuzidi hii ni changamoto. Tunakusanya *only 4.5 percent* ya walipa kodi Tanzania. 2.7 *Million out of Six Billion, only 4.5 percent* ya watu wote wanaolipa kodi. Kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha lazima tutoke hapo, tusonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri, bahati nzuri *TRA* wamewahi kufanya *study*, *TRA* ilikuwa na maboresho katika maeneo mawili, eneo la kwanza ilikuwa ni hili kuitoa *TRA* kuwa chombo cha utawala kwenda kuwa *component tax* ya *TRA*. Eneo la pili ilikuwa waende kwenye ku-*improve efficiency* na walikuwa na mambo kadhaa, moja kupunguza viwango vya kodi, kurahisisha ulipaji kodi, wakaja na mapendekezo mengi

lakini moja ya pendekezo zuri sana ilikuwa ni kwamba tupunguze wigo wa *VAT* iwe kati ya asilimia 10 mpaka 20, halafu tupunguze utiriri wa kodi kwenye *Local Government Authority,* badala yake *VAT* inayokusanywa watakuwa wengi wakishaongezeka, Serikali Kuu ibaki na asilimia 75 halafu *Local Government Authority* ibaki na asilimia 25 ya *VAT,* hivyo tutakuwa tumesaidia sana kwa maana ya *accumulation* wa zile kodi ni za kwetu lakini pia kupunguza utitiri wa kodi katika maeneo ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu Dar es Salaam nimerudia tena hapo, nilishatoa hapa angalizo na nikasisitiza Majiji yote yana sifa Kumi, lakini kwa sababu ya muda nitaje mbili. Moja miundombinu nadhifu ya usafiri, hii ni muhimu na ninaipongeza Serikali kwa kujenga Daraja la Tanzanite, sasa Mheshimiwa Waziri tumejenga daraja lile zuri kwa mkopo halafu unakuja na tozo achana na hiyo biashara. Daraja la Tanzanite ni daraja zuri, lilijengwa kwa lengo la kupunguza foleni katika hii barabara ya Ali Hassan Mwinyi na ni daraja zuri, kwa hiyo usiharibu furaha ya Dar es Salaam kwa kuweka tozo, achana na hiyo biashara.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuna kitu kinaitwa 24 *hours activity,* Majiji yote yanakuwa na 'K' tatu, piga kazi masaa 24, kula maisha masaa 24, lipa kodi masaa 24, Mheshimiwa Waziri hawa watu ndiyo wanakulipa kodi, habari za kusema fungua biashara kuanzia Saa Sita, achana na hiyo kitu! Eti, Jumamosi unaambiwa kwamba msifungue biashara mpaka usafi ufanyike, mambo ya wapi hayo? Hayo mambo hayawezi kuwa katika Majiji Mheshimiwa Waziri, kwenye hotuba yako umesema sanaa na burudani ndiyo inayokuwa kwa kasi kiuchumi, sasa burudani makao makuu yake si Dar es Salaam? achia Dar es Salaam 24 *hours. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni ushauri. Mheshimiwa Waziri umeongeza *import duty* kwenye *cotton yarn,* Tanzania bahati mbaya Waziri wa Kilimo hayupo, hapa tuna *ginnery* peke

yake hatuna *spinning* ukiongeza *cotton yarn* itabidi ufunge viwanda vya *A to Z* utafunga *NIDA*, utafunga kama viwanda vitano hivi, kwa sababu hapa hatuna *raw materials.* Hili jambo tumelizungumza mwaka jana, ninaomba sana Kamati ya Bajeti na wewe Mheshimiwa Waziri mliangalie, kwa kuweka *import duty* 24 *percent* mpaka 35 *percent* hatutaweza kushindana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani *cotton yarn* viwanda viko vichache mno ambavyo vinazalisha vingi tuna-*import,* sisi shida yetu tunataka tupate *agro-processing industry* tusafirishe mazao ambayo yamechakatwa, kwa hiyo kuleta *yarn* hapa ni jambo jema naomba sana liangaliwe hili ili viwanda vyetu visije vikaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kitila muda wetu umekwisha.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka naomba ukae kwanza. Waheshimiwa Wabunge muda wetu umefikia hapa kwa leo, ninawashukuru kwa michango yenu mizuri sana lakini niendelee kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuzisoma Kanuni zetu na kuzifuata. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu zimetupa mamlaka na uhuru wa kufanya mijadala Bungeni na tumepewa kinga pia katika mijadala hiyo, lakini tunaelewa sote kwamba kila uhuru una mpaka, kwa hiyo, huo mpaka umewekwa kwa Kanuni zetu sisi wenyewe. Tunapozungumza na kuishauri Serikali Bungeni tutumie lugha za staha ambazo hazitovunja heshima ya mtu mwingine. Sisi ni Waheshimiwa tunapenda kuheshimiwa na ndiyo maana tunaitwa Waheshimiwa, kwa hiyo mamlaka nyingine

ikiwemo ya Rais ambaye ndiye Kiongozi Mkuu wa Serikali iheshimiwe pamoja na Serikali yake nzima.

Waheshimiwa Wabunge, tunaruhusiwa kama Wabunge kutoa ushauri siyo kuiponda na kuidharau Serikali, kwa hiyo tuwe makini katika hilo, tunapochangia tuwe na uhakika na jambo ambalo tunalizungumza ili hata ukiambiwa utoe ufafanuzi na hoja uweze kwenda kwenye mstari na kuwaaminisha Watanzania. Watanzania wengine hawafikiri mara mbili Mbunge anapozungumza, wanakubali kile unachozungumza hata kama si cha kweli. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa tulinde heshima na mamlaka ya nchi ili watanzania tuendelee kufaidika.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo dogo hapa; Waheshimiwa Wabunge wanatangaziwa kujiorodhesha kushiriki mafunzo ya JKT kwamba mafunzo hayo yanatarajiwa kuanza rasmi tarehe 4 Julai, 2022 katika Kikosi cha 834 KJ Makutupora - Dodoma na wanatakiwa kuripoti kambini kuanzia tarehe 1 hadi tarehe 3 Julai, 2022. Ili kupata idadi kamili ya washiriki na kukamilisha maandalizi muhimu tunaomba Waheshimiwa Wabunge wajiorodheshe wathibitishe ushiriki wao kwenye orodha ambayo itapitishwa humu Bungeni na wahudumu, Wabunge watakaothibitisha ndiyo watashiriki mafunzo hayo na taarifa kamili za mahitaji zitatumwa kwao baada ya ofisi kupata orodha hiyo.

Mheshimiwa Ole-Sendeka nakupa dakika chache.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa kutumia kifungu cha mwongozo wa Spika mwongozo wako, nikirejea pia Kanuni ya 71 juu ya baadhi ya mambo yasiyokubalika na kwa sehemu umesaidia kwenye maelezo yako ya matumizi mabaya pia ya majina ya

viongozi wa Kitaifa, maana nilikuwa naenda Kifungu cha 71(1) halafu nakwenda (g) lakini sehemu inayosema au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa maana ya kutumia jina la Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa nataka pia pamoja na hiyo kurejea Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema kutakuwa na uhuru wa mawazo majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hauwezi kukatizwa, kuhojiwa nje ya Bunge. Pia Ibara ya 63 (2) na (3) ambayo inaipa Bunge dhamana ya kuisimamia na kuishauri Serikali na kwamba kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Lucy Mayenga aliyekuwa akisema wanaopinga hoja za Mawaziri wana nia ya kumpinga Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limempongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan na kila Mbunge kwa kumbukumbu nilizonazo aliyesimama ndani ya Bunge hili bila kujali chama chake amesimama na kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa nchi yetu kwa kazi nzuri anayofanya hata wale wenzetu wa Vyama vya Upinzani wameonesha mapenzi ya ghafla na ya dharura, kwa chama chetu na kwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni kuomba mwongozo kama kwa kutimiza wajibu wa Bunge wa kuishauri na kuisimamia Serikali ni kumpinga Rais kwa sababu kazi ya Bunge siyo Kamati ya kushangilia, kazi ya Bunge imepewa dhamana kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali na kwamba wajibu huo lazima ufanywe na Bunge makini unaloliongoza wewe leo na linaloongozwa na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na siku zote tutaendelea kumpongeza Rais kwa mambo mazuri anayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka mwongozo wako kama kwa kukosoa Mawaziri, kukosoa Serikali katika taarifa zake, je, huko ni kumpinga Rais? Nilitaka Mheshimiwa mwongozo wako ili mambo haya uyaweke vizuri pamoja na kwamba ulishaanza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ole Sendeka umesimama kwa kanuni 76 kuhusu mwongozo na kwamba pia ametumia Kanuni ya 71(1)(g), maelezo yake sina haja ya kurejea lakini kama nilivyotangulia hapo mwanzo, kazi mojawapo kubwa ya Bunge ni kuishauri Serikali. Kwa hiyo, katika kushauri nikasema tuendelee kuzitumia kanuni zetu ambazo zinatupa uhuru wa kutoa maoni lakini kwa njia na lugha ya staha.

Kwa hiyo, yale maneno ambayo ameongea Mheshimiwa Lucy kama kuna watu yamewagusa maana hakumtaja mtu, wale watu kama kweli wanafanya hivyo waache lakini si maneno mazuri kuwaambia Wabunge kwamba hawamuungi mkono Rais na Serikali, lakini ninaamini kabisa Taasisi ya Bunge kama chombo tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais na tunafanyakazi kwa ajili ya kuimarisha nchi yetu na siyo Rais peke yake.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo kama kuna mtu ana fundo ndani ya roho yake abaki nalo peke yake asituumizie nchi yetu. Mwisho wa mwongozo na pia nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa Kumi na Moja kamili.

*(Saa 7.07 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*.

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Rais wetu Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kupambana kuhakikisha kwamba maendeleo ya wananchi wake yanaweza kusonga mbele. Vilevile niweze kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kutuletea bajeti ya wananchi; kwa maana ya kwamba imejielekeza jinsi gani inakwenda kushughulikia, kufufua uchumi na kuongeza uzalishaji ili maisha ya wananchi wetu yaweze kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taifa lolote ili liweze kuongeza uzalishaji basi lazima taifa hilo wananchi wake wawe na afya njema; na bajeti hii imejielekeza kabisa kwa kuendelea kuonesha kwa vitendo jinsi gani Serikali inaendelea kuongeza miundombinu ya afya lakini jinsi gani inaendelea pia kuboresha ile iliyokuwepo ili

kuhakikisha wananchi hawa wanapata afya njema. Tumeona jinsi ambavyo bajeti hii imenunua vifaa hasa kwa ajili ya uchunguzi mbalimbali. Tumeona imenunua *CT scan* 11 lakini imenunua *MRI* nne *Digital X-ray 104, echo cardiography saba*, lakini na vitu vya oxygen tumenunua *PET scan* kwa ajili ya *Ocean Road*. Hivi ni vifaa ambavyo vinakwenda kuongeza jinsi ya kutambua magonjwa kwa haraka ili wagonjwa hawa waweze kupata matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwasababu kipekee na sisi Mkoa wa Kigoma tumepata *CT scan* ambayo imewekwa pale Maweni kwa hivyo wananchi wetu watakwenda kufanyiwa uchunguzi wa *CT scan* pasipo kusafiri kwenda Mikoa ya mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo kuhusu *PET scan* ninaendelea kuipongeza Serikali kwasababu imeona ni jinsi gani iendelee kuwasaidia wagonjwa wenye magonjwa ambayo hayaambukizi, ikiwemo saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *PET scan* ambayo imefungwa pale *Ocean Road* tunayotegemea ianze miezi miwili au mitatu ijayo imegharimu takribani bilioni kumi na nane hii inakwenda kuwasaidia wagonjwa wa kansa tuliokuwa nao nchini; na hii ni mashine ya pili kwa East Afrika. Wenzetu Kenya walitangulia na sisi tumepata sasa. Hii inakwenda kuwasaidia wagonjwa wa Kansa kugundua ugonjwa mapema kugundua *extent* ya ugonjwa, na pale unapompatia matibabu basi utajua basi kansa imekwisha au haijakwisha, tofauti na zamani ambapo ukishampa matibabu basi unabaki unasubiri na kuona, *wait and see*, nimempatia tiba, je atapata dalili tena. Kwa hiyo hii haipo tena na tumesema tukimgundua mgonjwa mapema na akapatiwa matibabu basi saratani inakwenda kupona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwasababu kwa bajeti hii basi imemjali mwanamke; kwasababu wote tunafahamu kansa inayoongoza hadi sasa ni kansa ya mlango wa kizazi ikifuatiwa na kansa ya matiti. Ambazo hizi zote zinakwenda kumuathiri mwanamke. Kwa hiyo Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amejionesha kwa kitendo kwamba anawajali akinamama wa nchi hii, anajali afya zao ndiyo maana akaelekeza fedha zake kwenye kifaa hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niombe Serikali *PET scan* zinatakiwa katika hospitali zote za kanda ikiwemo *KCMC*, Bugando na Mbeya ili kusogeza hizi huduma. Niiombe Serikali, katika zile fedha ambazo tunakwenda kuziokoa kutoka kwenye kubana matumizi basi zifanya kazi hii ili wagonjwa *PET scan*. Wagonjwa hawa tena wapunguziwe mwendo na gharama ili wapate huduma hizi karibu. Hii iende sambamba na kuongeza *linear accelerators;* matibabu *modern* kwa ajili ya kansa, zipo mbili tu *Ocean Road*. Naomba Serikali iangalie tena upya na hospitali zote za kanda ziweze kusaidiwa *linear accelerator* ili wagonjwa wetu wapate matibabu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kigezo hiki wagonjwa hawa wakishapata hii *PET scan* na *linear accelerator* basi hatuna hata sababu ya kuwapeleka tena wagonjwa nje ya nchi. Ni ukweli usiopingika kwamba wagonjwa wa kansa ni wengi hapa Tanzania. Tunapata wagonjwa wapya takribani 14,000 kwa mwaka; na hawa ni wale ambao wanakwenda kuziona hospitali, ambao ni asilimia 33 tu ya wagonjwa tuliokuwa nao kwenye jamii. Kwa hiyo unaweza ukaona takriban 42,000 wapo mtaani, wanaogundulika kila mwaka kati yao ni 33 *percent* wanakwenda hospitalini. Kwa hiyo tuendelee kuwajali wagonjwa hawa wenye magonjwa ambayo hayaambukizi kwa kuendelea kuwaboreshea kuwapatia mahitaji hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kujenga Hospitali ya Rufaa ya Kanda Magharibi pale Mkoani kwetu Kigoma. Limekuwa ni ombi la muda mrefu; tangu mwaka 2016; wananchi wa Mkoa wa Kigoma walishatoa eneo lakini wakaenda mbali zaidi wakatoa hadi michango, tunazo milioni 100 kwenye mfuko. Hii ni kwa kuonesha jinsi gani tunahitaji hii hospitali ya rufaa kanda ya magharibi. Niiombe Serikali basi iharakishe mchakato wakupeleka fedha Mkoani Kigoma ili Hospitali yetu ya Kanda Magharibi iweze kuanza ujenzi mapema. Hii itakwenda kumuondolea mwendo mwananchi wangu anayetoka Muhambwe ambaye alikuwa akitaka kwenda kupata matibabu kwenye hospitali za rufaa *either* aende Bugando ambapo anatembea takribani kilometa 367 au aje Dodoma anatembea takribani kilometa 800, au aende Dar es Salaam ambapo anatembea takribani kilometa 1261. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwendo mrefu sana. Kwa hiyo kwa kutuletea hiyo hospitali pale Kigoma tunaamini huduma zitakuwa karibu lakini wananchi watakwenda mwendo mfupi na gharama pia za nauli na matumizi zitapungua. Niishukuru tena Serikali, na niombe fedha zile zije kwa wakati kwasababu tumeshatenga eneo katika Kata yetu ya Machinjioni pale Kigoma Kitongoji cha Kichangachui; tunaomba fedha zifike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma tumebahatika kupata miundombinu hii ya afya; na tunafahamu kabisa uhaba wa watumishi upo nchi nzima lakini unatofautiana. Kwenye ikama ya Watumishi wa Afya wa Mkoa wa Kigoma tuna uhaba wa takribani asilimia 33; kwa maana ya kwamba; I mean asilimia 67, tuna 33. Hii asilimia 33 ndiyo inayoitegemea sasa, maana tunakwenda kufungua vituo vya afya vingine tunakwenda kufungua Hospitali ya Halmashauri ya Kakonko na tunakwenda kufungua Hospitali ya Halmashauri ya Kigoma *DC*. Hii hii asilimia

33 ndio inategemea igawanywe katika hizo hospitali, kwa maana ya kwamba basi watendaji watakuwa wachache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali; tunafahamu imetoa kibali kwa ajili ya ajira, basi Mkoa wa Kigoma upewe kipaumbele kwasababu tuna uhaba mkubwa sana wa watumishi wa sekta ya afya. Nimalizie katika eneo hili kwa kukumbushia tena, nilichangia nilivyosimama mara ya mwisho hapa; nikumbushe tena bima ya afya kwa makundi maalum. Tunafahamu Serikali ina mpango wa kutoa bima ya afya kwa wote, lakini najua ni zoezi ambalo haliwezi kwenda kwa mkupuo. Basi tuanze na haya makundi maalum ambayo yanataabika sana nikimaanisha wazee, watoto na wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante muda wako kengele ya pili.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tekcla Mohamed, jiandae Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya mimi kuchangia bajeti kuu. Awali ya yote ninampongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka kipaumbele kuridhia mradi wa *LNG* kule Lindi kwa hiyo sisi wana Lindi na Mtwara na Taifa kwa ujumla tunashukuru. Hili ninajua kabisa ni kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu. Ninampongeza pia Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na timu yake yote kwa kuja na bajeti kuu hii nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitajikita kwenye Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Kukabiliana na Ukatili katika Jamii. Nakuja na takwimu chache tu angalau, Mpango Mkakati wa Kutokomeza Ukatili kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWA) mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022 ulidhamiria kupunguza ukatili katika jamii yetu kwa asilimia 50. Ukatili huu ni wa kimwili, kisaikolojia, kingono na hata kiuchumi. Pia kuna taarifa, walifanya hawa MTAKUWA, kwamba kati ya wanawake watano basi mmoja ame-*experience* ukatili wa kingono. Lakini pia kati ya wasichana watatu mmoja amepitia ukatili wa kingono. Kati ya wavulana saba mmoja amepitia ukatili wa kingono katika maisha yake. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tafiti za Serikali na *UNICEF* zimetoa taarifa kwamba ukatili huu kwa asilimia 60 unatokea nyumbani na kwa asilimia 40 unatokea shuleni. Hii ni hatari sana. Mtoto huyu atapona namna gani? Kama akinusurika ukatili pale nyumbani basi akienda shuleni atapata ukatili wa kingono na aina nyingine. Hili ni janga kubwa, tusilifumbie macho, hali siyo shwari. Madhara yake ni nini kwa ukatili huu; vijana wetu na wanawake wanaathirika kimwili, hata viungo vya uzazi vinaathirika lakini kikubwa zaidi afya ya akili inaathirika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapotendewa tendo hili la ukatili uwe wakingono iwe wa kiuchumi iwe wa kinini basi kijana huyu au mtoto huyu ana weka kumbukumbu zile kwenye *sub conscious mind*. Kinachotokea jinsi anavyoendelea kukua analeta ile *event* ama *seen,* inakuja usoni inakuwa kama *screen* inaendelea kum-*disturb.* Kwa maana hiyo sasa nini kinatokea; anakuwa na hofu hana ujasiri ni mwenye mashaka hata akienda shuleni hana mchango mzuri ndio wale unakuta hawana maendeleo mazuri kimasomo. Hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika Serikali yetu sasa, ninaona kwenye bajeti kuu hapa kuna rasilimali zimetengwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii imetengewa milioni 43; lakini pia afua maalum za kupambana na ukatili ni bilioni 2.65 kwa Mikoa yote. Ina maana katika Mkoa milioni 14 kwa mwaka. kwa wastani ni milioni moja kwa kila Halmashauri kwa mwezi. Hii ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili huu ni vita kubwa. Sasa vita kubwa hii tunaenda na silaha kidogo sana. Ninaomba kabisa, bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii naomba iwe *revised* na iongezewe. Lakini pia kuna watendaji wetu kule, maafisa maendeleo ya jamii na maafisa ustawi wa jamii, hawa kazi yao kubwa ni kuhamasisha uchumi katika kaya na kuhakikisha kutokomeza mila na desturi potofu zinazosababisha ukatili pamoja na kuimarisha mahusiano katika familia pamoja na. hata hivyo, watu hawa kwanza ni wachache, tumeona katika taarifa, maafisa maendeleo ya jamii wapo asilimia 43 lakini maafisa ustawi wa jamii wako asilimia 97 tu nchi nzima. Sasa vita yoyote…

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa

**T A A R I F A**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba ustawi wa jamii upungufu ndio asilimia 97, sio kama alivyoongeza ndugu Mbunge. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tecla.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, afisa maendeleo ya jamii kuna upungufu huo kama nilivyousema na afisa ustawi wa jamii pia upungufu wa asilimia 97.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwakuwa sababu mojawapo ya ukatili katika jamii yetu ni kutokana na changamoto ya uchumi, hivyo basi ile asilimia 10 iliyokuwa imepangwa kwa ajili ya kuhudumia jamii yetu; wanawake asilimia nne vijana asilimia nne, na wenye makundi maalum (walemavu) asilimia mbili ninaomba ibaki vile vile. Hata hivyo tulikuwa tunaomba hata iongezwe ifikie asilimia tisa kwa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari sana, kwa sababu hata kwenye halmashauri zetu ile tu iliyokuwa nne nne mbili (4:4:2) haitoshi. Bado kuna mlundikano wa maombi ya jamii yetu kuomba misaada hiyo ama mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafani ninaomba tuiangalie jamii hii, tuangalie kuwakwamua hawa wananchi, hususani wanawake katika jamii yetu. Bila kufanya hivyo ukatili huu utaendelea na matokeo yake huko miaka 50 ijayo miaka 20 ijayo miaka 30 ijayo sijui tutakuwa na Taifa gani la Tanzania lisilojiamini na lisilokuwa na ubunifu kwa sababu tayari wameathirika na ukatili wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbogo jiandae Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti kuu ya Serikali. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu, pamoja na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa kutuletea hii bajeti. Bajeti ni nzuri

imegusa maeneo makubwa ya mwananchi kwa ajili ya maendeleo. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kuliletea Taifa maendeleo, hasa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa kutoa ushauri upande wa vifaa vya ujenzi ambao bei imekuwa kubwa sana, ambapo kwa mwananchi wa kawaida kugharamia ujenzi wa nyumba kuweza kupata bati inakuwa ni tatizo kwa sababu wananchi wa Tanzania wengi wao vipato vyao ni duni. Kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize, kidogo, ukienda Uganda asilimia karibia 80 ule mji wa Kampala umeezekwa kwa vigae na vile vigae vinatengenezwa na wananchi wa kawaida kutumia tu udongo wanachanganya na simenti na baadhi ya *mechanical*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kama ikiweza kutoa elimu, utaalam kama wa Uganda wanavyofanya hata mwananchi wa kawaida ataweza kuezeka nyumba yake kwa kupitia vigae. Vigae ni mbadala wa bei ilivyo juu ya mabati na vifaa vya ujenzi, hasa kupitia *VETA,* majeshi yetu pamoja na magereza, hivi vyuo vya *VETA* tukiviwezesha tujenge na viwanda vya vigae, wanafunzi wanapopata utaalam wa utengenezaji wa vigae itamrahisishia mwananchi wa kawaida kwenda kupata huduma ya vigae na kuweza kuezeka nyumba yake kwa urahisi zaidi. Kwa sababu sasa hivi hata mabadiliko ya tabia nchi vijijini hata nyasi zenyewe za kuezekea nyumba hazipo kwa hiyo vigae ndio suluhu pekee hata nyumba za tembe wenzengu Wagogo wataezekea vigae Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije upande wa ranchi, hii ya Kongwa; kwenye bajeti yako ulielezea kuhusu Kongwa. Mheshimiwa Waziri ile ranchi ya Kongwa naomba uachane nayo kwa sababu mji wa Dodoma ni jiji; hadi sasa hivi kuna mahitaji makubwa sana ya nyama, hasa ukizingatia Kombe la Dunia.

Ukiingia huko bei ya nyama sasa hivi ni tatizo. Sasa ranchi hii tukianza kuivuruga na kuibadilisha kuwa ya kilimo ilhali Jiji la Dodoma linakua, na mahitaji ya nyama pia; hata mnadani tunaenda kula nyama kule, tutakosa kula nyama za mnadani siku ya Jumamosi.  Kwa sababu ile ranchi inasaidia, hata wafugaji wa kawaida wanaweza wakatumia kulisha wanyama kama ng'ombe katika hifadhi ya Kongwa. Tukiivuruga tutasababisha mahitaji ya nyama Jijini Dodoma kuwa ni ya shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mengi zipo skimu nyingi sana Mkoa wa Rukwa zimetelekezwa, miundombinu ipo, lipo ziwa Tanganyika hakuna gharama ya miundombinu; kuliko kuanza sasa kuivuruga Ranchi ya Kongwa. Naungana na wabunge wote, hii Ranchi ya Kongwa isiguswe. Ikiwezekana iboreshwe, mitambo ya ngombe pamoja na madume; hapa tunalalamika wananchi wetu wanafuga mifugo ya kienyeji ambayo haina tija. Sasa ranchi ile inatakiwa irekebishwe, iboreshwe hawa wananchi wafugaji wapewe mbegu bora kutoka Ranchi ya Kongwa na rachi nyingine zote zinazomilikiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye gridi ya Taifa. Mkoa wa Rukwa tunatumia gridi ya taifa kutoka nchi Jirani, siwezi kuitaja jina. Kwa sasa hivi ninamshukuru Mungu kwenye bajeti yako umesema unatuunganisha Gridi ya Taifa kutokea Iringa. Hili jambo linatakiwa lipewe kipaumbele kwa sababu tupo kwenye ushindani wa kiuchumi. Tupo kwenye ushindani wa kiuchumi lakini umeme tunategemea nchi Jirani. Kwa hiyo hujuma *(sabotage)* ya aina yoyote ile ya kuweza kudhoofisha maendeleo ya Mkoa wa Rukwa ni rahisi.

Kwa hiyo, hii gridi ya Taifa mmesema mnaunganisha na Iringa fanyeni hili jambo liwe la kipaumbele, hii kazi ikamilike mapema kwa sababu tupo kwenye shindano la kiuchumi, kwa hiyo *sabotage,* umeme unaweza ukakata, watu viwanda vyao

vikaharibika. Mambo ya kiuchumi na ushindani kuna *sabotage* nyingi, ni ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye uchumi wa bluu, uchumi wa bluu hasa mikoa mitatu; Rukwa, Katavi na Kigoma, tunashukuru mmetupatia meli kwenye bajeti, imeingia baada ya Wabunge wa mikoa mitatu kupiga kelele, tumepata meli Ziwa Tanganyika. Kwa hilo jambo, tunasema ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja upande wa miundombinu. Miundombonu bado. Kuna baadhi ya mikoa jamani, tuongee ukweli, ilisahaulika katika nchi hii. Hii mikoa ya pembezoni ilisahaulika na ndiyo maeneo yenye uchumi. Miundombinu mpaka sasa hivi kwa mfano kwenye Jimbo langu la Nkasi Kusini kata nne ambazo barabara hizi za uchumi, siyo za uchumi tu, ni pamoja na ulinzi kwa ajili ya wananchi, kwa sababu wananchi kule hata wakipata tatizo la uharamia, askari hawezi kufika kule kwa sababu miundombinu haipo. Kwa hiyo, ndiyo fursa ya maharamia na majambazi na wahalifu kwa ajili ya ukosefu wa miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuombe, Mheshimiwa Mwigulu unapokuja *wind-up,* utuambie hizi barabara za kimkakati katika majimbo yale yaliyosahaulika nchi hii hasa Kigoma, Nkasi Kusini toka uhuru barabara, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye soko la mahindi, tena mwaka huu ndiyo kuna changamoto kubwa sana. Soko la mahindi mkulima anahangaika huko pembejeo gharama; tunashukuru mmeweka ruzuku katika pembejeo, lakini mnapokuja kununua pamoja na kuweka ruzuku, kama ni *NFRA,* mje mkae na wakulima mjue gharama ya gunia moja huyu mkulima wa kawaida ameligharamia kwa Shilingi ngapi, ili muweke bei inayolingana na thamani ya gunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *NFRA* wanaweza wakaja wakasema hili gunia tunanunua kwa shilingi 55,000 kwa mkulima, kumbe gharama hizo za gunia ni shilingi 120,000 mpaka shilingi 100,000. Kwa hiyo, unakuta huyu mkulima hamumsaidii, mnamdidimiza. Kwa hiyo, wakati wakununua bei za mahindi *NFRA* mfanye utafiti kujua gunia moja huyu mkulima wa kawaida ametumia gharama ya shilingi ngapi mnunue kulingana na thamani ya gunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja vyuo vya kati. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais amefuta ada Kidato cha Tano na cha Sita. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya. Vyuo vya kati ndiyo vinavyotengeneza utaalam na ajira. Hivi vyuo mafundi gereji wengi mtaani huko ni darasa la saba. Pia ni mafundi wazuri mno, ambao hawa wanapomaliza Darasa la saba wakiingia kwenye *VETA* hapa, naomba Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ahakikishe kama Serikali aone namna ya kuweza kufuta ada kwenye vyuo vya kati, atasaidia kundi kubwa sana ambalo linachangamoto ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti yake ameisoma, upo ubadhirifu wa fedha za UVIKO. Mheshimiwa Rais anatafuta fedha, anahangaika huku na kule na ametuletea maendeleo makubwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo kengele ya pili.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay jiandae Mheshimiwa Bahati Ndingo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa inayofanyika nchini, ni kazi iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa za utatuzi wa matatizo ya wananchi wetu katika majimbo tuliyotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kuzungumzia suala la kikokotoo. Hali ni ngumu sana kwa watumishi ambao wamestaafu hivi sasa. Nadhani tutazame jambo hili kwa sababu kwenye vijiji tulivyotoka wastaafu wengi wanapofika umri wa miaka sitini, hawana zaidi ya miaka sabini; wengi wao umri wao unaishia kwenye miaka sabini au sabini na kitu. Kiwango hiki cha kikokotoo tunachoonyesha sasa, kwao siyo rafiki kwa sababu mahitaji ni makubwa kulingana na afya yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri Serikali, jambo hili kwa kuwa walikaa na viongozi wao na vyama hivyo na vikakubaliana, basi nao watoke hadharani walizungumze badala ya sisi tu kama Bunge kuhangaika kulizungumza na pengine tutapata tafsiri ya wazi kwa wananchi ili wananchi waweze kufurahia jambo hili na hasa wale wastaafu wetu. Unapofika miaka 60 kwa kweli wewe ni kambi ya matatizo mengi kwenye afya, lakini pia huduma nyingi zinahitajika, unarudi kwenye hali ile ya zamani kama mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri, kama inawezekana, eneo hili litazamwe upya kwa sababu wastaafu wengi wanatupigia simu wakizungumzia kwamba jambo hili kwao siyo rafiki, Serikali ilitazame kwa namna inavyoona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nije kwenye bajeti. Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Mawaziri bajeti zetu kila

mwaka, mimi nina mwaka wa saba katika Ubunge. Inaonekana bajeti zetu ni nzuri wakati zikiwasilishwa, lakini kwenye utekelezaji tunashindwa kufanikisha kwa sehemu kubwa. Kwa hiyo, nafikiri kama ambavyo fedha za Mheshimiwa Rais zile za *COVID 19* zilitoa taswira kubwa sana kwa wananchi na heshima kubwa sana kwa wananchi na ikagusa maeneo makubwa ya wananchi wetu, basi tutazame namna ambavyo na bajeti yetu inakuwa wazi na pia inagusa yale maeneo tuliyoazimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekaa kwenye Bunge hili nikiangalia, kila mwaka inapokuja bajeti tunaifurahia sana, lakini baadaye kwenye utekelezaji maeneo mengi yanakwama. Ushauri wangu ni nini hapa? Ushauri wangu ni kuona viasharia vilivyokwaza mwaka wa kwanza, basi tuone namna ambayo mwaka huu kwenye makusanyo yetu tunaweka vile vipaumbele kwenye maeneo yaliyokwama, lakini pia kwa jinsi ambavyo inaweza ikatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mchezo tunacheza huku Bungeni, huu wa kushika Shilingi na kurudisha. Mimi naona ni mchezo tu wa kushika Shilingi na kurudisha. Nimwambie Waziri wa Fedha na hata Mawaziri wengine wote, taarifa ya bajeti ya mwaka huu kwenye Jimbo langu la Mbulu Mji imeandika vitu vingi sana. Nina hofu kwamba haya yatatekelezeka? Kwa hiyo, kila Waziri nimwombe atusaidie. Nami nitoe tu tafsiri wazi kwamba mwakani mimi nashika Shilingi, wala siirudishi. Ninawa-*alert* kabisa Waheshimiwa Mawaziri, ikishindikana tafsiri ya wazi tuwe nayo kwa wananchi, kwa sababu hali ni mbaya ya jinsi ambavyo tunashika shilingi halafu tunarudisha; halafu mwaka mwingine tunakuja tunashika shilingi halafu tunarudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za mpango wa barabara ile ya Karatu – Mbulu – Hdyom ni mwaka wa nne ikitembea kwenye vitabu vya bajeti, lakini inashindikana kutekelezwa kwa sababu

hatuna fedha. Wananchi kule hawaamini hivyo, kwa sababu tayari tulishaweka nia yetu njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri hatamu hii ya mwaka huu, *tender* ilitangazwa na tayari toka mwezi Mei. Cha kushangaza kabisa, tunajua kwamba manunuzi yataishia mwezi wa Saba kwa ajili ya mchakato wa mkandarasi yule aliyewekwa kupeleka vifaa mwezi wa nane ili aanze kazi. Je, atakwenda, au ni maandalizi mazuri tu kwenye kitabu chetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nitakaposhika Shilingi wala siirudishi. Mawaziri wote ni marafiki zangu na huwa wanatekeleza mambo mengi, lakini kwa kuwa yanakwama na wananchi baadaye wanakuja na hoja ya kudai kwanini haikutekelezwa, basi ni wajibu wetu na sisi pia kuyakataa yale ambayo tunashika Shilingi halafu tunarudisha. Pengine utetezi wenu uwe wa wazi mbele ya wananchi na uweze kuleta taswira nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, nizungumzie suala la vifaa vilivyoagizwa vya *COVID 19*. Tumesubiri magari ya *ambulance* toka madarasa yale yamejengwa, toka Mheshimiwa Rais ameleta fedha, mchakato wa manunuzi Serikalini siyo mzuri mimi nawaambia, kwa sababu tayari toka zile fedha zimekuja, majengo yamejengwa, miradi mingine imeshaanza kutoa huduma, lakini vifaatiba, magari yale ya *ambulance* na vifaa vingine, hata mitambo ile ya kuchimba maji, mpaka leo bado. Hali hii inaonesha nini? Inaonesha wananchi wanasubiri sana huduma, lakini sisi tunakuwa hatujafika kwa wakati unaostahili. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri ifike mahali tuone utaratibu wa mchakato uangaliwe kwa namna ya pekee sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye eneo lingine la wahitimu wa vyuo vya kati. Kwa *VETA* nilikuwa nashauri kama itawezekana na vyuo hivi vya ufundi mlivyokarabati tutazame

namna ambavyo wale vijana wanapomaliza masomo yao au kipindi kile cha mafunzo, basi hata Serikali ione namna ya kuwapa vifaa. Vijana hao wanaosoma kwenye vyuo vya ujuzi kuna changamoto kubwa sana. Kwa nini kuna changamoto? Familia wanazotoka hazina uwezo. Zinapowapeleka kwenye vyuo, baada ya kumaliza mafunzo, hata ile *package* moja tu ya vifaa, hakuna, yaani hawawezi kununua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa ajili ya kuondoa ada ya Kidato cha Tano na Sita. Nadhani mwakani mje basi na namna ya kuondoa pia karo kubwa sana kwenye vyuo vya vyeti kwenye afya na vyuo vya ufundi stadi na vyuo mbalimbali vya ujuzi. Mara nyingi wale wanafunzi wanapata gharama kubwa na familia zinazopeleka wale vijana wanatoka shule za kata na familia zao ni za kipato kidogo. Kwa hiyo, wanasoma kwa gharama kubwa. Ukienda kwenye vyuo hivi vya *certificate,* kama ni afya ama ni vyuo hivi vya ujuzi, chakula tu inaweza kuwa zaidi ya Shilingi milioni tatu kwa mwaka. Ukichanganya na gharama nyingine kwa familia ya kaya ambayo uchumi wake ni mdogo, wanashindwa kumudu na hatimaye wale wanafunzi wengi wanasoma kwenye mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni la muhimu sana, hao vijana wa vyuo vya chini tuweze kuwaona, ni gharama gani wasaidiwe. Zamani Serikali ilikuwa inatoa chakula na kulikuwa na gharama ndogo kwenye familia zao kwa sababu sehemu nyingine Serikali inabeba. Tulipofuta, wameingia kwenye gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea vijana wanaomaliza Chuo Kikuu, baada ya kuonekana ajira imekuwa ngumu sana, sehemu ile ya asilimia 10 ya mikopo inaweza kuwa sehemu nzuri sana katika kuwasaidia namna ambavyo ile 4:4:2...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Ni kengele ya pili. Mheshimiwa Bahati Ndingo, halafu jiandae Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata fursa nami nianze kwa kuipongeza sana Serikali inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kufanya. Niungane na Waheshimiwa Wabunge kuipongeza sana Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri mnayoifanya kwa bajeti nzuri ambayo mmeileta Bungeni, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri bajeti hii kama ikitekelezwa kwa ufanisi walau hata kwa asilimia 50, kwa ufasaha, nina uhakikia uhakika kabisa tutapiga hatua kama Taifa. Leo hii mchango wangu niuelekeze kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa mashuhuda humu ndani na ripoti ambazo zimekuwa zikitolewa na Mdhibiti wa Hesabu. Ripoti zile zinakuwa na upotevu mkubwa sana wa fedha. Laiti kama tungeweza kuwekeza nguvu kubwa kwa huyu Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kumtengenezea miundombinu rafiki ya ufanyaji kazi wake, ninaamini kabisa tungeweza kuokoa fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sio mwanasheria, lakini nimejaribu kupitia na kusoma, nimeenda kwenye Katiba yetu ya mwaka 1977 na marekebisho yake, Ibara ile ya 143 imemtaja Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali na imeainisha pale majukumu makubwa matatu. Jukumu la kwanza; ni kudhibiti fedha zote zitakazotoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini jukumu la pili alilopewa mdhibiti huyu ni kuhakikisha matumizi yote

ya kwenye mfuko huo wa Serikali yamepitishwa na Sheria ya Bunge. Kazi yake ya tatu, ni kufanya ukaguzi walau mara moja kwa mwaka na kutoa ripoti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napata shida kidogo nikija kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma. Sheria yenyewe inaitwa *Public Audit Act,* ile Sura ya 418. Sasa sheria hii ambayo ndiyo inaanzisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, imeshaondoa neno "mdhibiti"; pale ni ku-*audit.* Nikisoma hiyo sheria hiyo, nimejaribu kusoma, kwa uelewa wangu, sijaona muundo wala uongozaji wowote wa mdhibiti huyo anafanyaje udhibiti wa hesabu. Nilichokiona hapa kwenye sheria hii, ni namna gani atakagua; kwa hiyo, nimeona muundo na utendaji kazi wake katika kukagua peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali anatembelea mguu mmoja wa *auditing* peke yake, lakini udhibiti sheria hii hatujaweza kuitafsiri vizuri Katiba inavyotaka. Ndivyo nilivyoona mimi kwamba sheria hii imetufanya tusiitafsiri vizuri Katiba, hivyo tumeelekeza majukumu yote ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali katika ku-*audit* lakini kwenye ku-*control* hatujaweza kulifanya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, kwa mfano kwenye ripoti ya ukaguzi, hii ya 2020/2021 *CAG* anahoji kuwepo kwa Halmashauri 19 ambazo zilipokea shilingi bilioni 47.19 za miradi ya maendeleo zaidi ya bajeti iliyopangwa. Sasa kama huyu ndio *controller,* ame- *control* vipi? Kama huyu *controller* naye anahoji kuzidisha na kuweka matumizi nje ya bajeti, kwa hiyo, tunaona kabisa suala la udhibiti kwa huyu Mkaguzi na Mdhibiti, bado suala la udhibiti hatujalipa nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba nishauri mambo mawili tu kwa Serikali kwenye suala hili. Kwanza, Serikali iangalie

uwezekano wa kutenganisha hizi nafasi mbili; ukaguzi na udhibiti; nasi tutakuwa siyo nchi ya kwanza kufanya hivyo. Nchi nyingi tayari zimeshaondoka huko, hata majirani zetu hapo Kenya. Ukishasema kwamba mdhibiti huyo huyo asaini fedha zitoke, huyo huyo akajikague, ufanisi hautakuwa vile kama ulivyo. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri tuone uwezekano wa kutenganisha kazi hizi mbili kuleta ufanisi na kupunguza na kutokomeza kabisa upotevu wa mali za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naiomba Serikali ili tuweze kudhibiti mali za umma, waje na miongozo iletwe Bungeni Sheria ya udhibiti ili tumwelekeze huyu atadhibiti vipi na atafanyaje kazi za udhibiti na ripoti zake zitakuwa zinaletwa vipi? Kuliko kusoma tu ripoti za ukaguzi wakati udhibiti tumeuacha pembeni. Kwa hiyo, naomba haya yazingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, hii nchi ni kubwa, lakini nchi yote hii kila Halmashauri inategemea Mfuko Mkuu wa Serikali. Tumeshauri hapa, tunaomba Wizara ya Fedha shirikianeni na TAMISEMI, wekeni mkazo kwenye hati fungani za Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa zianze sasa utaratibu wa kufanya miradi yao kibiashara, watu wanunue hisa zao watengeneze miradi. Hii ya kusema kila Halmashauri kutegemea Serikali Kuu, tunajicheleweshа, kwa sababu hatuwezi kama Taifa kila Halmashauri kuitimizia mambo yake. Hatuwezi!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana mjitahidi, msisitize uwazishwaji wa hizi hati fungani, ukamilike ili Halmashauri zetu ziweze kujiendesha kibiashara. Kwanza kwa kufanya hivyo, mtaweza kusaidia Halmashauri hizi, watu wawe wamiliki wa miradi ile, lakini vile vile watakuwa wanapata fedha kwa riba ndogo. Maana yake ni tofauti na kukopa fedha kwenye benki. Hati fungani zina riba ndogo. Kwa hiyo, mhakikishe hizi Halmashauri zinaweza kujifanyia miradi ya maendeleo na ikabuni miradi mikubwa ambayo baadaye itakuwa ndiyo vitega uchumi

vya Halmashauri zetu kuliko Halmashauri zote kutegemea Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, jiandae Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami nichangie kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/2023. Kwanza nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuijenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya pekee kuwapongeza Waziri wa Wizara ya Fedha, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kutuletea bajeti ambayo kabisa inaonesha nia ya dhati ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unaenda kujikita kwenye uchumi wa bluu kama sehemu mojawapo ambapo bajeti hii imeweka kipaumbele katika sekta za uzalishaji. Uchumi wa bluu unamaanisha mazao, uchumi unaotokana na uvunaji kutoka kwenye maji ya bahari, maziwa, mito, mabwawa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi inakua kwa asilimia 2.5 na inachangia pato la Taifa kwa asilimia 1.8 na inaajiri zaidi ya Watanzania milioni 4.5. Kiwango cha pato kinachochangiwa na sekta hii muhimu ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa na maziwa makubwa katika Bara la Afrika ambayo yanapatikana

Tanzania ambayo ni Victoria, Tanganyika, Rukwa, Nyasa na ukanda mkubwa wa bahari na maziwa mengine madogomadogo ambayo ni Eyasi, Natron, Manyara. Kwa maliasili yote hiyo ambayo Mwenyezi Mungu ametupa na ukalinganisha na mchango unaochangiwa na maliasili hii ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite kwenye Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika kabla ya uhuru ndiyo ziwa ambalo lililokuwa likichangia pato kubwa kwenye uchumi wa mkoloni. Tunapozungumza Ziwa Tanganyika, tulichozawadia dhahabu ya kwanza ya Ziwa Tanganyika ni dagaa, kwa jina maarufu dagaa wa Kigoma. Zawadi nyingine ya pili inayopatikana katika Ziwa Tanganyika ambayo tulipewa inaitwa ni almasi ambayo ni migebuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika lina aina za samaki zaidi ya 224 lakini samaki ambao ni wa kibiashara *(commercial fish species)* ziko mbili tu na sana ukiongeza ya tatu ni moja. Ya kwanza ni dagaa, ya pili ni migebuka na ya tatu ni sangara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2000 ziwa hili limedoroka katika mapato yake. Wavuvi wamekuwa wakihangaika, hawana miundombinu, lakini kitu kikubwa zaidi tunachoweza kukiangalia ni kipi. Naomba niende kwenye chimbuko lenyewe la uzalishaji la mapato ya Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya 1990 hadi 2000, uvuvi katika Ziwa Tanganyika, wastani wa mapato ilikuwa ni *metric tons* 200,000 na mwaka 2000 hadi 2013 uvuvi ulishuka hadi tukawa tunavuna kwa wastani wa *metric tons* 120. Kwa 2013 mpaka sasa inasemekana kiwango tunachokipata ni *metric tons* 80. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kushuka kwa mapato ya uvuvi yanatufikirisha sana. mwaka 1953 wakati wa utawala wa wakoloni, Mwingereza alipoona Ziwa la *Victoria* halina mapato makubwa yeye alichukua sangara kutoka katika Ziwa Tanganyika na kupeleka Kamati ya Utafiti ya Uvuvi ya Kikoloni ilichukua sangara kutoka katika Ziwa Tanganyika na kuipeleka kupanda katika Ziwa Victoria. Uchumi tunaoshangilia sasa hivi wa sangara umetokana na kazi nzuri iliyofanywa na mkoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize, tafiti zetu za uvuvi *(TAFIRI)* je, hawana mpango au wana upungufu wa fedha hawawezi wakafanya utafiti kuangalia namna gani ambavyo wanaweza wakachukua sangara wakaweka kwenye maziwa haya mengine ambayo siyo *productive* kama Ziwa Rukwa na Eyasi? Nashauri sana Idara ya Utafiri ya Uvuvi *(TAFIRI)* waongezewe fedha ili waweze kufanya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kushuka kwa mapato katika Ziwa Tanganyika, sasa hivi kuna zoezi linaloendeshwa na Serikali yetu ya *fish stock assessment* ambayo inafanyika upande wa Tanzania. Samaki walioko katika Ziwa Tanganyika ni *pelagic* ni *migrant* wana-*move*. Ili zoezi hili liwe na tija, basi ni vema nchi yetu ishirikiane na nchi zile ambazo zote zina-*share* Ziwa Tanganyika ambazo ni Burundi, Congo na Zambia. Hilo zoezi lifanyike kwa pamoja, zoezi hilo litaleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihamie kwenye nishati kwa maana ya kuleta msisimko wa kuleta viwanda nchini Tanzania. Nimepita nikiangalia nchi zilizoendelea, nchi zilizoendelea nyingi zilifanya utafiti na kuhakikisha kwamba zina nishati ya kutosha. Kwa mfano, Afrika Kusini ina megawati 80,000, Uturuki ina megawati 60,000. Sisi tukiangalia vyanzo vyetu pamoja na umeme uliopo vyote kama tutakuwa tumeviendeleza, tutaweza kupata megawati 5,579.8. Umeme ndiyo moyo wa viwanda…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Felix kwa mchango mzuri na hongereni kwa dagaa wazuri.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kaiza hayupo, nafasi yake itachukuliwa na Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi. Jiandae Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga.

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Moja ya jambo ambalo binafsi linanipa ukakasi ni suala la mgawanyo wa fedha za Muungano. Wazungumzaji wengi waliopita walimsifu Waziri na timu yake na wakamtaja Waziri kwamba ni mchumi aliyebobea, maana yake kwamba ni msomi, lakini sifa moja ya wasomi ni wale wenye kutumia taaluma yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo linanipa mashaka makubwa. Tukiangalia katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya Saba inazungumzia masharti ya kukusanya fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara ya 133 naomba ninukuu: "Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatunza akaunti maalum itakayoitwa "Akaunti ya Fedha ya Pamoja" na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili…"

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar. Hata hivyo, hadi leo hii bado Serikali haijataka kuweka wazi, je, hii akaunti ya fedha ya pamoja ipo? Je, hii akaunti ya fedha ya pamoja, kwa sababu hapa tuna

ushirika, tumekubaliana tunachanga, tutakachokipata tunakiweka sehemu moja, baadaye tunafanya matumizi, tunaambiana tumetumia kiasi fulani cha fedha na kitakachobaki tunakigawa kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa makubaliano tuliyokubaliana katika hii Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza, hatuna akaunti ya fedha ya pamoja. Hatujui ni mahali gani fedha hizi zinawekwa. Ni namna gani ambazo fedha hizi zinatumika. Leo kama haitoshi, katika ibara hiyo ya 134 pia ilipendekeza kuweko na Tume ya Pamoja ya Fedha, lakini hadi leo hatujui ni namna gani tume hii inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea tume hii iweze kukusanya fedha, lakini kutupa taarifa ni namna gani fedha wamekusanya kiasi gani, ni namna gani fedha hizi wametumia, ni namna gani fedha ambazo zimebaki na mgawanyo sasa tunagawaje kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inapelekea mgogoro na malalamiko makubwa juu ya suala zima la Muungano hususan kwa upande wa Zanzibar. Naomba ikumbukwe mwaka 2006 iliundwa tume iende ikafanye utafiti, ione namna gani ya mapato na matumizi ya fedha hizi za Muungano. Tume ile ikiitwa *PWC* ilianza kufanya kazi kuanzia mwaka huu 2014 hadi 2020, ilionesha ni kwa namna gani Zanzibar hatupati stahiki ya fedha zetu kwa mujibu wa Katiba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki hadi 2014, zaidi ya Shilingi Trilioni 11.2 Zanzibar tukidai Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa naamini Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, atatuambia sasa ni kwa asilimia ngapi Zanzibar tulipata fedha hizi kwa mujibu wa taarifa ya Tume hii ya *PWC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme. kwa sababu ya muda, mgawanyo wetu ni asilimia 4.5 lakini kwa *report* hii tulipata asilimia 1.1 kwa nini? Tumekuwa kama ni uhisani tunafadhiliwa wakati sisi ni washirika katika tume hii. Naomba nitoe rai au nitoe ushauri kwa Serikali. Kwanza, naomba Serikali kufuata Katiba na Nchi kwa kuanzishwa Akaunti ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa sheria ya mapato yote ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naiomba Serikali ifanye utafiti mpya wa mapato ya Muungano na matumizi kwa shughuli za Muungano tu ili kutoa takwimu sahihi kwa kipindi tulichonacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naiomba Serikali igawe ziada ya mapato ya Muungano kwa washirika wa Muungano kwa mujibu wa mgao na kanuni za mgao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, naiomba Serikali kumtaka *CAG* kufanya ukaguzi ili kubainisha mgao sahihi na fedha ambazo Zanzibar inaidai Serikali ya Muungano kwa kipindi chote toka kuanzishwe kwa jambo hili la Akaunti ya Pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tuna wanafunzi 36 na walimu watatu kutoka Shule ya *Bluebird Pre and Primary School* ya Wilaya ya Arumeru ya Halmashauri ya *Arusha DC* toka Jiji Arusha, karibuni na ahsante kwa kutembelea Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nyamoga, ajiandae Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali yake ya Awamu ya Sita kwa jinsi ambavyo inaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Nitahitaji karibu siku nzima kutaja miradi ambayo iko katika jimbo langu, kwa hiyo itoshe kusema tunamshukuru sana na tunaendelea kushukuru kwa niaba ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumzia miundombinu ya barabara na nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba wakati wa kusoma bajeti alitaja barabara kadhaa. Nitamweleza hii barabara na anahitaji tu kuiongeza, haiongezi fedha kwenye bajeti yake tayari ipo. Barabara ya kutoka Iringa kwenda Kilolo ambayo itajengwa kwa kupitia fedha za Rais. Nimejiridhisha na *TANROADS* kwamba ipo kwenye taratibu za kuandaliwa tenda, lakini wananchi wa Kilolo waliniuliza kwamba kwa nini Waziri hakuitaja. Basi kwenye hitimisho Mheshimiwa Waziri aitaje tu kwa sababu tayari iko kwenye mipango ili wananchi waweze kuelewa kwamba ni mojawapo ya barabara zitakazotengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiutaratibu magari yetu huwa yanakuwa na *spare tyre* kwa maana kwamba kukitokea dharura basi ile tairi inasaidia kufunga na kuondoka. Barabara ya kutoka Dar es Salaam hadi Mbeya, Tunduma na inayoenda Kyela ipo sehemu moja yenye shida kubwa ambayo huwezi kuchepuka kwa namna yoyote ile na hii ni ile sehemu ya Mlima Kitonga na nimeitaja mara nyingi hapa. Naomba nisikilizwe kwa sababu ni kwa maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika pale kama kukitokea gari ikaharibika kwa sababu zile kona ni nyingi na mara nyingine magari kupinduka na hayo ni matukio ya mara kwa mara, hakuna njia nyingine, kwa maana nyingine barabara ile inakuwa imefungwa na hakuna pakupita. Maana yake ni kwamba lazima kutafuta mbadala ili magari yaweze kuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kulitokea tukio kama hilo na wakati napita pale Ilula kulikuwa na *ambulance* tatu kutoka Mbeya na kutoka Iringa ambazo zilikuwa zinaelekea Dar es Salaam zina wagonjwa ndani. Kama hiyo haitoshi hivi karibuni kutoka Ruaha Mbuyuni kwenye Kituo cha Afya kuna mama mmoja ambaye alikuwa wa kujifungua, alifia pale kwa sababu tayari kulikuwa kumezibwa ile njia pale. Hayo ni matukio ya kiafya, lakini bado hatujazungumzia madhara ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Mkoa alishawahi kukwama pale, wako Mawaziri walishawahi kukwama pale na Mheshimiwa Waziri wa Fedha asisubiri aje akwame pale ndipo aseme, alichokuwa anasema Mheshimiwa Mbunge kilikuwa cha muhimu. Niombe barabara ya mchepuko ambayo nimesema kwamba tumeshaanza kuitengeneza kwa kupitia fedha za UVIKO kutoka Mahenge kwenda Udekwa, inapita inatoka pale Ilula ni kilomita chache sana na ikitengenezwa itakuwa ukombozi kunapotokea tatizo pale. Niombe sana hilo liangaliwe ili liweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo napenda kuzungumzia ni suala la lumbesa. Nalo nimeshalipigia kelele sana hapa. Mheshimiwa Waziri inabidi aelewe kwamba waitazame kwa lenzi ya kimapato. Sisi mapato ya halmashauri tunakusanya kwa kuhesabu magunia. Magunia mawili yanazalisha gunia lingine moja, maana yake ni kwamba wanapofika kule ukiwa na

gunia, ukiwa unakusanya shilingi bilioni tatu maana yake ni kwamba umepoteza shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila halmashauri kama tukihesabia magunia kwa vipimo vinavyotakiwa, halmashauri zingepata mapato moja ya tatu zaidi wanayopata sasa hivi, lakini tukizungumza kwa lenzi ya hasara wanayopata wakulima, nimeshalisema sana kwa sababu hamna kipimo kinachotumika. Tuangalie kwa lenzi ya kimapato, tunaweza tukaelewa ni mapato kiasi gani halmashauri zinapoteza kwa sababu tu suala la lumbesa linaonekana limeshindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, siamini kwamba Serikali imeshindwa kufanya udhibiti wa suala la lumbesa. Tungependa sisi wakulima wa kutoka Kilolo, Makete na mikoa mingine ambayo tunazalisha viazi, njegere na hivyo vyote visivyokuwa na vipimo, tunapenda kujua Serikali ina mikakati gani ya kukomesha tatizo la lumbesa ambalo linawaumiza sana wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kuzungumzia suala la ada. Elimu yetu inaenda kama *pyramid,* huku chini wanafunzi wengi wanakuwa shule ya msingi baadaye wanaenda sekondari, baadaye chuo. Wanapofika Chuo Kikuu wanakuwa ni wachache sana, sasa mtu ameshindwa kulipa 20,000 tumesema elimu bure, mtu ameshindwa kulipa 70,000 tumesema elimu bure, huyu mtu anamfikisha mtoto wake Chuo Kikuu tunasema alipe shilingi laki saba anatoa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu pamoja na kuweka dirisha maalum la kusaidia watu, iangaliwe namna ya watu ambao hawawezi kulipa ada za Vyuo Vikuu. Nimekusanya takwimu kwa mwaka mmoja kwenye Jimbo langu, wanafunzi walionijulisha kwamba wanaahirisha masomo ninao wanafunzi 14 kutoka vyuo mbalimbali walioahirisha masomo kutoka vyuo vya

Serikali, kwa sababu hawakuweza kumudu kulipa ada kwenye vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vyuo vya Kati imesemwa sana niombe kwa sababu tangu nimeingia Bunge hili tunazungumzia vyuo vya kati, watoto wale nao ni wa Watanzania, hatuwezi kuwa na watu wenye digrii watupu, nao waingizwe kwenye elimu bure kwa sababu wana haki kama wanaoenda vyuo vikuu. Nina uhakika na wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Spika na wengine wote tukipata shida za mifumo ya maji kwenye nyumba zetu hata leo, tunawaita hawa hawa ambao tunawakandamiza kwamba walipe ada na tunajua wametoka kwenye familia maskini, hili halikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kuzungumzia mikopo ya vifaa vya usafiri na kukumbusha tu, kwamba uendeshaji wa Serikali pia unaanzia kwenye ngazi za chini hasa kwa mfano ngazi ya Kata, ambapo tunao Watendaji wa Kata. Ukiangalia sekta nyingine kama kilimo, mifugo na idara nyingine zimeanza kuangalia sekta ya Kata, lakini ujumla wake wale Watendaji wa Kata wenyewe hawana vitendea kazi, hawana pikipiki. Sasa mtakapoanza kutoa vifaa hivi kwa utaratibu wowote mtakaoweka, kumbukeni kwamba ile miradi tunayoipelekea fedha nyingi, wanaoisimamia katika ngazi ya kwanza ni Watendaji wa Kata. Hivyo wakumbukwe ili waweze pia na wao kupatiwa vifaa vya usafiri weweze kuhudumia jamiii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Profesa Patrick Alois jiandae Mheshimiwa Venant Daud Protas jiandae Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kushukuru kwa kunipa fursa kuchangia katika hoja hii ambayo iko mbele yako. Nianze moja kwa moja kwa kumpongeza Shemeji yangu Waziri Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba kwa wasilisho zuri alilofanya, kuwasilisha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo na ile Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze sana Serikali yangu CCM inayoongozwa na Mama yetu Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutekeleza vyema sana ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Serikali yetu inatekeleza miradi mingi sana katika Majimbo yetu yote Serikali ya Awamu ya Sita na pamoja na miradi inayotekelezwa katika Majimbo yote, Serikali inatekeleza miradi ya mikakati ambayo ni miradi mikubwa ikiwepo ile ya reli ya *SGR*, mradi wa Julius Nyerere, Daraja la Busisi na miradi mingine mikubwa, kwa hiyo tunaipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sintokuwa na shukrani kama sitasema ahsante kwa kidogo ambacho Serikali imetupatia katika Jimbo langu la Moshi Vijijini. Naishukuru sana Serikali kwa sababu tumepata miradi ya kutosha kusema ukweli, tuna daraja la pale Rau, Rais wetu alikuja akalizindua ambalo liligharimu Shilingi Milioni 910, kuna Mradi wa Maji wa Telamande Waziri Mkuu alikuja akauzindua uligharimu shilingi milioni 905, kuna ujenzi wa madarasa 53 ya mradi wa UVIKO ambayo yamegharimu shilingi bilioni moja na milioni sitini, kuna mradi wa maji wa mradi wa UVIKO pia uko katika Kata za Kimochi na Mabogini ambazo ni bilioni moja, kuna ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo tumeshapata shilingi 500. Zahanati ya Uru Kusini ambayo tumeshapata shilingi milioni 500, ukarabati wa barabara saba kwa kiwango cha moramu ambapo tumepata shilingi bilioni 1.5 tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utaalam wangu mimi nitachangia kwenye Sekta ya Kilimo na nianze kwa kumpongeza

sana Waziri wetu na Serikali yetu kwa kupandisha bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294 mpaka shilingi bilioni 954 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 308.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pesa hizi ambazo zimepeleka Wizara ya Kilimo nina hakika zinakwenda kuhudumia wakulima ambao ni karibia asilimia 65 na wataenda kunufaikia vizuri sana. Ushauri wangu kwenye hili kwamba nitaongelea kilimo cha kahawa, kilimo cha mbogamboga, nafaka na mikunde kama muda utabaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kahawa tunaiita ni dhahabu ya kijani na bei ya kahawa ya *Arabica* kwenye soko la dunia sasa hivi ni dola 4.2 na ile ya *Robusta* ni dola mbili, na mwaka ulioishia wa fedha ni kwamba kule Moshi wakulima walipata mpaka shilingi 7,000 kwa kilo moja na leo asubuhi George alisema kule Bukoba wakulima walipata shilingi 3000.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa zao la kahawa hapa nchini kwa ujumla umeongezeka kutoka tani 60,651 mpaka tani 73,027 ikiwa ni ongezeko la asilimia 20.4 na ongezeko hili kwa mwaka huu ulioishia *data* za *TRA* zinasema kwamba nchi yetu mwaka 2021 ilipata kiasi cha pesa dola milioni 155 ikiwa ni zao la pili kutoka kwenye korosho ambayo ilipata dola milioni 159.

Mheshimiwa Naibu Spika, kahawa inazalishwa kwenye Mikoa mingi hapa nchini, kahawa inazalishwa Kilimanjaro, Kagera, Arusha, Ruvuma, Mbeya, Mara, Songwe na Kigoma. Sasa pamoja na umuhimu wa kahawa katika uchumi wa nchi yetu tumeshaona ni zao la pili ambalo linaliingizia Taifa letu pesa nyingi, lakini kuna changamoto ambazo zipo na ningependa tuzijadili hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote haya yanayozalisha kahawa changamoto yao kubwa ni upatikanaji wa maji ya

kumwagilia ili wakulima waweze kuvuna kwa wingi hiyo ndiyo changamoto ya kwanza, changamoto ya pili ni miche bora, na changamoto ya tatu ni pembejeo. Kama wenzetu wa korosho na tumbaku wanavyopata pembejea wakulima wa kahawa walikuwa hawapati pembejeo na hii ilisababisha tusiende vizuri sana. Kwa hiyo ninaishauri Serikali kwamba zile pesa za umwagiliaji ambazo zimetoka, tuwekeze kwenye mifereko ya asili ili tuwafikikishie wakulima maji na wakishapata maji watazalisha kahawa nyingi na tutaipatia Taifa letu pesa za kutosha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili ni miche. Kuna ile miche Milioni 20 ambayo Mheshimiwa Waziri Bashe amesema kwamba atategemea kwenye bajeti hii tunaomba miche na pembejeo wapelekewe wakulima ili tuweze kushiriki kikamilifu katika uzalishaji wa kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni kwenye zao la mbogomboga. Mbogomboga ni zao la thamani sana na sekta hii ikiandaliwa vizuri kama tutapanga vizuri tukiwa na mikakati ya kutosha, tukiwapa vijana kazi ya kutuzalishia mbogamboga, nina uhakika kama Taifa tutawatoa vijana na Taifa litapata pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka uliopita, ulioishia 2021 sekta ya mbogamboga iliingizia nchi yetu dola za Kimarekani milioni 373 na mwaka huu tunategemea mbogamboga zitaingiza dola milioni 750 na kufikia 2030 mbogamboga tunategemea zitaliingizia Taifa dola milioni mbili. Sasa niombe ukienda kwenye maeneo kama Mji wa Karatu, ule Mji umejengwa pale kutokana na zao la vitunguu. Karatu tunayoiona leo imetokana na zao la vitunguu, kwa hiyo tukiwekeza tukiwapata vijana kazi ya kuzalisha mbogamboga, tukiwawekea miundombinu ya kutosha kwanza, tuwaandae wawe kwenye vikundi, wakishakuwa kwenye vikundi tuwahamasishe wazalishe mbogamboga kwa wingi ili zile ndege tumenunua ziweze kupeleka nje na kuliingizia Taifa pesa za kigeni.

Tukiboresha huduma za ugani kwa hawa vijana ambao tutakuwa tumewaandaa tunaweza tukaanzisha viwanda vidogovidogo ambavyo pamoja na kupeleka mbogomboga nje pia tutaliingizia Taifa letu pesa za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho ni kwenye nafaka na mikunde. Tanzania yetu hii inajitosheleza kwa chakula, mwaka wa 2021 nafaka na mikunde uzalishaji uliongeza kutoka tani milioni 18 toka tani 18,196,733 hadi tani 18,665,065. Mafanikio haya ya uzalishaji mzuri wa nafaka ulitokana na uwepo wa mvua ya kutosha, lakini mwaka huu kama tunavyojua wote mvua ni kidogo sana, huenda tukapata matatizo na tukawa na uhaba wa nafaka na chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Waziri wa Kilimo na kwa Serikali kwa ujumla wake ni kwamba zile *scheme* mpya ambazo tunazianzisha sasa hivi, zilenge Mikoa ambayo ina maji mengi ya kutosha ili tusije tukaanzisha *scheme* kwenye maeneo ambayo hakutakuwa na maji na hazitakuwa *sustainable* tunaweza tukapata hasara. Kwa hiyo mchango wangu ni kwamba *scheme* hizi ziwekwe kwenye maeneo ambayo yana maji ya kutosha ili hii miradi iwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Profesa. Mchangiaji wetu mwingine Mheshimiwa Venant Protas, ajiandae Mheshimiwa Genzabuke ajiandae Mheshimiwa Zuwena Bushiri.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuwa miongoni mwa wachangiaji katika Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri bajeti ya mwaka 2021/2022 ambayo Bunge lako Tukufu lilipitisha kwa Jimbo langu la Igalula imekwishafika kwa asilimia 100, hiyo niwapongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya, zimebaki chenji tu kidogo za wahisani sasa sijajua zimekwama katika mlengo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza Serikali leo tuko katika Bajeti Kuu ya 2022/2203 ambayo tutakwenda kuitekeleza kuanzia Julai Mosi, mwaka 2022, pamoja na pongezi nzuri lakini mimi nilikuwa kidogo katika Bajeti ya Waziri kuna mambo ambayo nilitaka tuyazungumzie kama wananchi na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kwanza nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kupunguza tozo ya miamala ya simu ambayo ilikuwa ni changamoto na ilieleta taharuki lakini Mheshimiwa Rais baada ya kusikia kilio cha Watanzania alipunguza hiyo tozo na baadae kwenye bajeti yako hii umeonyesha kuwa utapunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tujue kama Watanzania kwa sababu tulipitisha tunaenda kukamilisha mwaka mmoja, tangu tumeanza kuchangia hizi tozo, *trip* ya kwanza ulikuja ukatuambia tumekusanya mabilioni ya fedha tukaona kwenye TV, lakini baadae tukaona kimya, sasa tunataka tujue haya makusanyo mpaka leo tulikusanya Shilingi ngapi ili tuwapongeze Watanzania ambao walivumilia maumivu na ninyi baadae mmekuja kuwaondolea kwa sababu ya hali ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili mimi nikupongeze pamoja na kuendelea kuwaona Watanzania na kuwapunguzia makali, mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri katika bajeti yako

umejikita sana kuwapunguzia mzigo Watanzania lakini umeenda zaidi, ukasema baadhi ya milolongo iwezwe kupunguzwa ili wananchi waweze kupata fursa na tunu na maendeleo ya Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema vizuri wananchi wanasafiri umbali mrefu kwenda kufuata huduma, na hii umeiweka vizuri sana ukasema baadhi ya vitambulisho viweze kutambulika, lakini Mheshimiwa Waziri nikuombe kuna kundi kubwa sana la Machinga na Bodaboda na hapa umeliweka vizuri sana, bodaboda ndio wengi zaidi katika maeneo yetu ya vijijini, sasa mimi nashindwa kuelewa, anayeendesha lori leseni yake ni Shilingi 70,000 anayeendesha Kirikuu 70,000, bodaboda 70,000! mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri, hebu punguza hawa watu wa bodaboda ili wasikimbizane na Polisi iwe tu tozo Shilingi Elfu Ishirini utakuwa umewasaidia sana na wataacha kuwa wanawakimbia Polisi na kwenda kufuata huko leseni, kwa sababu unakuta mafunzo 80,000, leseni 70,000 kabla ajaanza kazi Laki Mbili imeisha sasa unakuwa umemsaidia au umemsababishia hasara kwa sababu hiyo hela ingeweza kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite kwenye mambo mawili au matatu katika bajeti hii. Kwanza nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kutambua Sekta ya Kilimo. Nimpongeze Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Mheshimiwa Rais amesema ili kuweza kulikomboa Taifa lazima tujikite kwenye sekta ya kilimo, bajeti tumeiona imeongezeka mara dufu katika sekta ya kilimo, kazi yetu sisi kama Wabunge kwenda kuwahimiza wananchi wetu kuweza kwenda kuitetea sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2021 Mkoa wetu wa Tabora ulizindua kitabu ambacho walikuja Mawaziri wengi, kitabu hicho kilitangaza fursa mbalimbali zilizoko katika Mkoa wetu wa Tabora. Ninakumbuka Mheshimiwa Bashe leo ni Waziri wa Kilimo alikuwepo wakati huo akiwa Naibu Waziri alishiriki katika

kongamano hilo la kufungua fursa, kitabu hicho kipo na kumbukumbu ya Serikali ipo. Waliomba Mkoa wa Tabora uweze kutengeneza *block farm* mbalimbali ili ziweze kusaidia wananchi katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuondoka tuliweza kukaa kama Halmashauri, wakapendekeza eneo la Kalangasi Kata ya Tura Jimbo la Igalula itengenezwe *block farm ya* korosho. Jambo la kushangaza tulipitia michakato yote ambayo ilikuwa utaratibu na kwa mujibu wa sheria na Baraza la Madiwani liliridhia kuwa Kalangasi sasa tutakwenda kutenga ekari 15,000 itakuwa *block farm* ambayo tutalima kilimo cha korosho, ajabu imeingia mdudu asiejulikana sasa imeanza kupigwa danadana *block farm* ile haijulikani kama ipo au haipo, wanataka waweke kilimo cha mizinga ya asali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bashe unatoka Mkoa wa Tabora hebu naombeni mnitajie ni nani ametajirika kwa asali anayetoka Mkoa wa Tabora? Wananchi wetu wengi matajiri wanatajirika kwa nafaka za chakula, sasa tunakwenda kuweka kilimo cha asali, wananchi wa Kalangasi waliweka *block farm* ya korosho wameutunza msitu kwa muda mrefu sana. Mheshimiwa Jafo alikuja pale ziara akasema huu msitu muhimu sana. Sasa mimi nashindwa kuelewa, hivi Serikali huwa wanawasiliana?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anataka *block farm*, Mheshimiwa wa Mazingira anasema huu msitu utunzwe kwa sababu ya mazingira, sasa mimi niiombe Serikali, wananchi wa Jimbo la Igalula Kata ya Tura, Kijiji cha Kalangasi wako tayari kushirikiana na Serikali kuweka *block farm* ya korosho, pia wako tayari kushirikiana na Serikali kwa kila hatua ili kuhakikisha mradi huu unaleta tija kupitia Halmashauri yetu na kupitia Taifa na kuingiza pato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo yuko hapa kupitia majibu ya Serikali, tunataka tujue tunapoondoka kwenda Majimboni tuondoke na kauli moja, kwa sababu wameshaanza *TFS* kwenda kupima eti lile eneo liwe la uhifadhi, wakati miaka yote tangu uhuru hawajawahi kwenda kule, wananchi wamehifadhi kwa kutumia gharama zao, leo wanaenda kupima kule nini? Nasi kama Wawakilishi wa Wananchi tunakataa na tunalaani wasisogee tena huko kwenda kupima eneo hilo, nadhani watakuwa wamenielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufungua uchumi wa Mkoa wa Tabora tumepewa fedha nyingi za kujenga reli ya kisasa *(standard gauge)* ambayo katika Mkoa wa Tabora asilimia 70 ya reli kutoka Makutupora kwenda Tabora….

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa

**T A A R I F A**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kumpa taarifa mnenaji kwamba mabadiliko ya tabianchi duniani yamekuwa ni mabaya sana na mvua zimekuwa zikipungua mwaka kwa mwaka. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kutunza misitu, kwa hiyo nimeona kusema kwa kutumia neno kusema walaaniwe ni kosa, kwa sababu nchi inateketea na dunia inateketea kwa sababu ya mazingira. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hili neno walaaniwe sijalisema yeye ameongeza chumvi misitu Tanzania iko mingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa wewe sema tu unaipokea ama huipokei ni vitu viwili tu.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei taarifa kwa sababu mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Endelea na mchango wako.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ninalolisema uhifadhi upo, misitu ipo waende wakahifadhi kule, wananchi hawa walihifadhi kwa miaka yote, sasa hivi wanakuja kufanya nini, kwa hiyo tunataka kilimo cha korosho usinipoteze kwenye mada yangu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Genzabuke, jiandae Mheshimiwa Zuena Bushiri, jiandae Mheshimiwa Taletale, jiandae Mheshimiwa Edwin Swalle

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kunzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono, lakini nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu kwa namna anavyofanya kazi. nimekuja kugundua kumbe walioimba wimbo kwamba tunaimani na wewe Mwigulu hawakukosea, na sisi Mheshimiwa Mwigulu tuna imani na wewe. Ninampongeza pia Naibu wako, Katibu Mkuu na

watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa namna mnavyofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza mama Mheshimiwa Rais mama yetu mpendwa Mama Samia Suluhu kwa jinsi anavyofanya kazi ya kuwatumikia Watanzania ili kuweza kuwaletea maendeleo na kuwafanya waweze kuishi maisha ya furaha na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo naomba niongelee kuhusu wafanyabiashara wa vitenge ambao wako pale Kariako, wengine wapo Kigoma na maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ukienda madukani utakuwa akina mama wanauza vitenge, utakuta akina mama wengine wanimachinga wanatembeza vitenge. Kwa wastani biashara ya vitenge ndani ya Taifa letu akina mama inawasaidia sana. kwa hiyo mimi nilikuwa ninaomba, ieleweke kwamba viwanda vya ndani sisi hatuvichukii, tunavipenda hakuna mtu anayekataa kitu cha kwake, lakini jinsi tunavyoagiza sukari kutoka nje, tunavyoagiza mafuta kutoka nje, namna hiyo hiyo ndivyo tunavyoagiza vitenge kutoka nje. Hii ni kwa sababu sukari na mafuta havitoshelezi ndani ya nchi yetu, lakini vitenge pia havitoshelezi ndani ya nchi yetu ndiyo maana vitenge vinaagizwa nje ili kuja kuongeza vitenge kwa vile ambavyo vipo ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hyo nilikuwa ninaomba kodi ipunguzwe kwa waagizwa vitenge vinavyotoka nje. Jana Mheshimiwa Kilumbe alizungumza vizuri sana vitenge vinapita kwenye bandari yetu, lakini kwa bahati mbaya vitenge vinavyopitishwa kwenye bandari yetu vikienda nchi za nje kodi ipo chini lakini vitenge ndani ya nchi yetu kodi ipo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo nilikuwa namuomba Mheshimiwa Mwigulu ahangalie jinsi gani ya kuweza kupunguza kodi ili wafanyabiashara hawa wanawake waweze kufanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni ajabu wewe unapika chakula halafu hautaki watoto wako washibe lakini unataka Kwenda kuwashibisha watu wa nje. Kwa hiyo tunaomba kodi iwe rafiki kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano makontena yanayoingia nchini, makontena ya *on transit* ni mengi sana kwa sasa hivi. Mwanzo kontena za *transit* zilizokuwa zinaingia, kila mwezi, zilikuwa ni tatu, zimeenda zikawa mpaka kumi, lakini kwa sasa ni kontena 300 na kuendelea, unaweza kuona tofauti iliyopo. Kama mwanzoni ni kontena tatu mpaka kumi. Sasa hivi kontena hizo hizo za *on transit* ni kontena 300 hadi mia 500 zinazoingizwa kwenda nje, ni namna gani Serikali inapoteza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kontena hizo zinazopita nchini mwetu hizo za *on transit* kontena moja linalipiwa dola 400, angalia tofauti iliyopo. Yaani dola 400 kwa kontena moja halafu mtu anapitisha mzigo anapeleka mizigo inakwenda nje halafu mtu anapitisha mzigo anapeleka mizigo inaenda nje halafu mizigo hiyo hiyo inarudi kwa mlango wa nje kuja kuuza nchini mwetu. Tunaomba Serikali isikilize kilio cha wafanyabiashara wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi akina mama, tunavyomuona Mheshimiwa Rais anavyofanya kazi vizuri kwa kuwaongoza Watanzania, lakini pia Bunge letu linaongozwa na mwanamke ambaye ni Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunatamani kuona wafanyabiashara wanawake wa Tanzania wakipunguziwa kodi ili waendelee kufanya biashara zao vizuri. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, chondechonde, mwaka jana

nilikuja hapa nikazungumza kuomba kodi ipunguzwe iwe rafiki kwa akina mama wanaofanyabiashara ya kutoka nje. Kwa mara nyingine tena, na kwa heshima na unyenyekevu Mheshimiwa Waziri ninaomba ufikirie ili upunguze kodi ili wanawake waweze kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kodi kutokuwa rafiki Serikali inapoteza mapato mengi sana kwa sababu, kwanza tumepoteza walaji waliokuwa wakija kununua biashara nchini mwetu. Soko la vitenge Tanzania tumelihamishia nje. Tunaomba kodi ipunguzwe ili wale waliokuwa wamehamia nje warudi kwetu Tanzania ili tuweze kuendelea kufanyabiashara vizuri na kodi iweze kuongeza. Kuliko ilivyo hivi sasa tunapoteza mapato, na *TRA* wanajua ni jinsi gani walivyokuwa wakiingiza mapato wakati wafanayabiashara wa vitenge walipokuwa wakiingiza mizigo nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza maneno hayo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** … ninarudia tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Mwigulu tunaomba ufanye kodi iwe rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zuwena Bushiri jiandae Mheshimiwa Taletale jiandae Mheshimiwa Edwin Swalle.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia bajeti hii ya Seikali. Nianze kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi

inayoongozwa na Mama yetu Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anazozifanya. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutuletea bajeti hii, bajeti ambayo imekonga mioyo ya Watanzania wote. Pia nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa mikopo ya halmashauri; mikopo hii ya halmashauri imekuwa ikiwajenga sana akina mama kiuchumi. Akina mama wengi wamechukua mikopo hii na wanalea familia zao na wanasomesha watoto Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanawake ambao tupo hapa Bungeni ni wawakilishi wanawake wenzetu, tumekuja ili tuwasaidie na wenyewe waweze kunyanyuka kiuchumi. Mikopo hii ya 4:4:2 wanawake asilimia nne, vijana asilimia nne na wenye ulemavu asilimia mbili bado imekuwa haitoshi, kwa sababu wanawake wengi wanaopata hii mikopo wanafanya biashara na wanapofanya biashara wakirudisha ile mikopo unakuta vikundi vingi vimejiunga na bado fedha haitoshelezi. Niiombe Serikali iache mikopo hii utaratibu huu wa 4:4:2 na wamachinga Serikali kuu iwatafutie fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka katika mchango wangu wa kwanza nije katika sekta ya uvuvi; nitaomba kuchangia Ziwa Jipe. Ziwa Jipe lipo katika Mkoa wa Kilimanjaro katika Wilaya ya Mwanga. Naongea kwa masikitiko makubwa sana, na Wabunge wenzangu nawaomba mtusaidie katika ziwa hili. Ziwa Jipe lipo katikati ya mpaka wa Kenya na Tanzania, lakini Ziwa Jipe limekuwa na magugu kiasi kwamba shughuli zote za uvuvi pale hakuna tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba chanzo cha maji cha Ziwa Jipe kinatoka katika Mkoa wa Kilimanjaro, lakini wenzetu upande wa pili wametengeneza mazingira mazuri,

wametengeneza miundombinu ya utalii wana hoteli za utalii, wanafaidika kupitia chanzo chetu cha maji ambacho kinatoka Mkoa wa Kilimanjaro. Lakini kwetu sisi magugu maji yamezidi kiasi kwamba hata wakazi wa pale hata kuvua samaki wameshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, walishafika viongozi wa mazingira akiwemo Mheshimiwa Waziri Makamba na Mheshimiwa Waziri Chande, wamefanya vikao na Vijiji vya Butu ambavyo vimezunguka Ziwa lile la Jipe. Lakini wamewapa wananchi matumaini, kwa sababu wananchi wanapoona viongozi wa juu wakija wanapata matumaini kwamba angalau tumesikilizwa shida yetu itatekelezwa. Hivi ninavyoongea wale Wapare hata Samaki kwa ajili ya chakula hawawezi kuvua

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali iangalie kwa kina sana na ifanye haraka iwezekanavyo kutoa yale magugu kwa kuwa Ziwa lile la Jipe ndilo linaloshisha Bwawa la Nyumba ya Mungu. Bwawa la Nyumba ya Mungu linazalisha umeme *megawatt* tano mpaka nane; lakini bwawa lile sasa hivi pia kutokana na yale magugu ambayo maji yanashindwa kupita vizuri maji yake yanaenda yakipungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi karibu tu Mheshimiwa Rais alipitisha kwamba, mradi wa maji unaokwenda kuanzia Same, Mwanga, Korogwe umetengewa fedha. Sasa fedha hizo zimetengwa, mradi huo wa maji unategemea maji hayo ambayo yanatoka katika Ziwa Jipe. Niiombe Serikali itusikilize sana kilio hiki na niombe Waziri atakapokuja ku-*windup* atueleze ni lini lile Ziwa Jipe litatolewa magugu, Wapare wamechoka, wanashida hata Samaki kwa ajili ya chakula hawapati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Hamisi Taletale jiandae Mheshimiwa Swalle jiandae Mheshimiwa Muharami Mkenge.

**MHE. HAMIS S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa nipende kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kile anachokifanya kwenye Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki na Wilaya yetu ya Morogoro Vijijini kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii unatembea Morogoro Vijijini ukiona kwamba huduma za kiafya zinakuja, huduma za shule pamoja na maji zinakuja. Wiki iliyopita tumepata mradi wa maji wa Morong'anya wa bilioni 24 na vilevile tumepata mradi wa maji wa Mtambarani bilioni nne, nani kama Mama Samia! Mama Samia hajaishia hapo kulitendea haki Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki. Ninavyozungumza hapa ametuletea kituo cha afya kwenye Kata ya Kinole ambacho hatukutegemea kabisa. Na kutokana na zile fedha za UVIKO Mama Samia ametuletea kituo cha afya kwenye Kata ya Mkulazi. Kutoka Kata ya Mkulazi mpaka unakwenda Ngerengere ulikuwa unatembea kilometa 70.4 lakini Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameliona na amatutatulia hilo tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja. Nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Waziri Mwigulu na mtani wetu. Kwenye huu mradi wetu wa *SGR,* ule mradi naamini unaanza mwezi wa kumi treni inatoka Dar es Salaam inakwenda Morogoro. Ni vituo vitano kutoka Dar es Salaam, kituo cha tano ni Ngerengere. Ngerengere ya sasa tofauti na Ngerengere ya zamani. Leo hii kama tunakwenda kupokea kituo cha mwendokasi maana yake mkazi wa Ngerengere anaweza akaenda Dar es Salaam kufanyakazi, akaenda Dodoma kufanyakazi Ngerengere inatanuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuombe kaka yangu Bashungwa, leo hii Ngerengere tuna kituo cha afya ambacho hakina *mortuary*. Leo hii kama kuna mtu anafariki asubuhi saa moja Ngerengere basi anatakiwa azikwe saa nne, la sivyo maiti itaharibika kwa sababu kituo cha afya hakina *mortuary*. Kituo hiki cha afya tumekirithi kwa wakoloni. Sasa nakuomba kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa, najua hushindwi. Kama umenipa Kituo cha Afya Mkulazi, umenipa Kituo cha Afya Kinole naomba ukatupe Kituo cha Afya Ngerengere linawezekana kwako kaka yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si tu *mortuary* leo hii tunasema Kituo cha Afya cha Ngerengere kina changamoto ya mama na mtoto. Kama leo hii mama anakwenda kujifungua kwenye Kituo cha Afya cha Ngerengere yaani hakuna pa kupumzika. Yaani huyu anajifungua huyu mwingine akae amsubirie. Mheshimiwa Bashungwa, nakuomba kaka yangu kwa heshima na taadhima kwa niaba ya Wanakusini Mashariki tunakuomba uitazame Ngerengere kwa ajili ya kile kituo cha afya. Tunaua watu na watu wanateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mji unakua lazima uwe na afya lakini vilevile lazima uwe na ulinzi uliotukuka. Kama tunakwenda kwenye Kata ya Ngerengere leo hii tuna kituo cha polisi cha kurithi pia, hatuna kituo cha polisi Kata ya Ngerengere, Kata ambayo tunakwenda kuwa na kituo kikubwa cha mwendokasi. Huu ni mtihani, na mtihani huu ninaamini kabisa wa kuutatua ni wewe Mheshimiwa Mwigulu. Ninakuomba kaka yangu, tunaomba utuletee fedha na sisi wana Ngerengere tupate kituo cha polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimuona juzi kaka yangu akitamba kuhusu Yanga kuhusu nini lakini pia akazungumzia miradi mikubwa ya Serikali na pia akauzungumzia Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere; naomba nimuelekeze kaka yangu,

Bwawa la Mwalimu Nyerere wakati unakwenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere lazima upite Bigwa Kisaki. Leo hii katika barabara zetu; tunakushukuru umetupa barabara ya Bigwa Kisaki kilometa 78, lakini haipo kwenye kipaumbele chako. Twende tukailinde Ilani yetu ya Chama Cha Mapundizi Mheshimiwa Mwigulu, twende tukawasaidie, na mje mtusaidie wana Morogoro Kusini Mashariki. Leo kama tunakwenda kulitazama Bwawa la Mwalimu Nyerere mnakwenda kwa kupitia helkopta, wageni wakija wanapanda ndege wanashuka; huu ni mtihani

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna njia ya Bigwa-Kisaki, kilometa 78, na pia kuna njia ya Ubena-Zomozi-Ngerengere-Mvuha. Tukitengeneza hizi njia tunaenda kufika kirahisi kwenye mradi wa kimkakati. Ninakuomba Mheshimiwa Mwigulu, kama unaamini mradi wa kimkakati ni Bwawa la Mwalimu Nyerere weka imani kwamba Bigwa-Kisaki ni njia ya kimkakati, iende ikatengenezwe; tusije tukasema tu tumetangaza kilometa 78 lakini hatuzioni. tunaomba tuione barabara yetu ya Bigwa Kisaki ni mtahani. Nakupongeza sana kwa vile ambavyo unatutazama, lakini nakuomba kwenye hili utupiganie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi wiki iliyopita niliongea na ndugu yangu, kaka yangu, mtani wangu, Mheshimiwa Bashe; nikasema leo hii sisi wanakusini mashariki tunalima karafuu inawezekana tunachuana na Pemba. Lakini utaratibu wa kupata wateja, utaratibu wa kupata wanunuzi inakuwa ni shida kwa sababu ya barabara ya Bigwa Kisaki. Leo hii hapa Dodoma watu wanakula machungwa, Iringa wanakula machungwa kwa asilimia hamsini yanayotokea Morogoro Kusini Mashariki. Ninakuomba ulisimamie hili suala kwa sababu Kusini Mashariki …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, *mortuary* hakuna wasaidie.

**MHE. HAMIS S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Kombo na Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwa bajeti hii ya Serikali.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nani?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, uliniita kwamba nitaanza kuchangia baada ya Msemaji aliyemaliza. Nimeitwa Swalle kwenye meza yako.

**NAIBU SPIKA:** *Yes,* ni Mheshimiwa Swalle, samahani. Mheshimiwa Swalle, halafu atakuja Mheshimiwa Mkenge.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii muhimu sana ya bajeti yetu ya fedha kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri waliyofanya kwenye kuandaa Bajeti hii ya Serikali. Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ambayo ni Bajeti ya Mheshimiwa Rais ya mara ya pili kwenye Bunge lako Tukufu ni

ya kihistoria ni hotuba ya kimapinduzi makubwa na uzalendo mkubwa sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hotuba yote, ukurasa kwa ukurasa. Kimsingi bajeti hii imejikita katika mambo yafuatayo; kwanza ni bajeti ambayo imekusudia kuinua kilimo na kumwinua mkulima wa Tanzania. Pili, hii ni bajeti ambayo imekusudia kuhimiza sekta binafsi na biashara pamoja na wajasiriamali wa nchi. Hii ni bajeti ya kihistoria kwa sababu pia imekusudia kukuza ajira nchini; ni hotuba ya kihistoria kwa sababu imekusudia kutoa tija na motisha kwa wafanyakazi wa nchi yetu ya Tanzania; pia ni hotuba ya kihistoria kwa sababu imedhamiria kuboresha huduma za kijamii zikiwemo, afya, maji, elimu, barabara, utalii na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imepokelewa vizuri sana na Watanzania wote nchini kote. Nampongezz Waziri kwani kwenye hotuba hii amedhihirisha wazi kwamba alichukua muda kujiandaa na kufanya utafiti, hongera sana. Pamoja na uzuri wa hotuba hii ya Waziri wa Fedha naomba ninukuu maneno ya Makamu wetu wa *CCM* Taifa, *Comrade* Kanali Abdulrahman Kinana aliyoyasema wakati akishiriki sherehe za *Iftar* tarehe 23 Aprili, 2022 kwenye kuadhimisha miaka 18 ya Kampuni ya Usafirishaji *(Silent Ocean Company)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kinana anasema hivi, "nataka vikao vizae matunda. Nchi hii imeharibiwa na "vikao," nchi hii imeharibiwa na "mchakato," nchi hii imeharibiwa na "tutafanyia kazi," nchi hii imeharibiwa na "tupeni muda," nchi imeharibiwa na "tutasikiliza," nchi hii imeharibiwa na "tutakwenda kutatua kero." Makamu wa *CCM* anasema yote tumesikia, tunataka vitendo. Huyu ni Makamu Mwenyekiti wa *CCM,* Abdulrahman Kinana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uzuri wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kwa kutembea kwenye maneno ya Kiongozi wetu wa *CCM* Taifa ni kwamba, hotuba hii ni nzuri sana, imejaa mapinduzi makubwa, imejaa uzalendo mkubwa, lakini haitakuwa na maana kama haya ambayo yamesemwa hayatakwenda kwenye maneno hayo ambayo Makamu wa *CCM* anasema, tusiendelee kusema "mchakato unaendelea, tunakwenda kufanyia kazi." Tunakuomba Mheshimiwa Waziri, hotuba hii ikatekelezwe ili ionekane wazi kwamba tumetafsiri kwa vitendo maono ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na sehemu ya kilimo. Kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, ukisoma kwenye ukurasa wetu wa 29 utaona wazi kwamba Mheshimiwa Rais anatembea kwenye Ilani ya *CCM*. Ukurasa wa 29 ile sehemu ya kwanza inasema katika miaka mitano ijayo *CCM* itaielekeza Serikali kuongeza fursa za ajira katika sekta rasmi na isiyo rasmi zisizopungua milioni saba kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani yetu inasema kuchochea ukuaji wa uchumi hususan katika sekta ya viwanda vinavyotumia malighafi za kilimo, mifugo, uvuvi, madini, maliasili na sekta ya huduma za kiuchumi ikiwemo utalii. Tumemwona Mheshimiwa Rais akitekeleza maono haya ya Ilani ya *CCM* kwa vitendo. Rais wetu kwenye sehemu hii ya kilimo kwenye hii bajeti yetu ameongeza zaidi ya shilingi bilioni 700 kwenye kilimo. Kwenye sekta ya Utalii peke yake Rais wetu amezunguka nchi mbalimbali akitangaza *Royal Tour* ambayo sasa imeanza kuzaa matunda makubwa kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa upande wa ajira, kwa mara ya kwanza kwa miaka mitano iliyopita Mheshimiwa Rais wetu ametoa ajira kwa vijana wetu zaidi ya 30,000 katika mwaka

huu wa fedha. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais amedhamiria kuboresha huduma mbalimbali kwa mujibu wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kwenye maneno haya ambayo nimesema kwamba tunaomba vitendo, naomba Mheshimiwa Waziri, kwenye hotuba yako amependekeza maeneo mbalimbali ya kuwabana watumishi na kufuatilia kodi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo ambayo yako chini ya uwezo wetu kama Serikali ambayo tunaweza kuongeza mapato. Kwa mfano, wananchi wa Jimbo la Lupembe kwa mfano, wana Kiwanda cha Chai ambacho Serikali imekitelekeza kwa muda mrefu. Nimekuwa naongea mara nyingi humu ndani nikisema kwamba Kiwanda hiki kama Serikali ingekuwa na nia thabiti ingeweza kuingiza fedha nyingi sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemwambia Waziri juzi kwa barua, kwamba kwenye Wizara yako Mheshimiwa Waziri kuna jambo limekwama kuhusu Kiwanda Lupembe. Naibu Msajili au Msajili wa Hazina amekalia maamuzi ya Mahakama yanayomtaka atekeleze uamuzi wa Mahakama wa kumtaka Mwekezaji wa Kiwanda cha Lupembe *Do Mecan TYRE* aweze kuachilia kile kiwanda ili Serikali iweze kuendelea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Swalle kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Muharami Mkenge, jiandae Mheshimiwa Kombo na baadaye Mheshimiwa Maganga.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya. Bajeti ya mwaka 2021 Wabunge wengi sana alituvisha nguo katika Majimbo yetu. Miradi mingi ya maendeleo imefanyika na hilo halina ubishi kabisa, kila Mbunge aliyekuwa hapa katika Jimbo lake, basi kuna kikubwa ambacho amekipata kutokana na bajeti ya mwaka uliopita. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa anayoifanya na pia napenda kumpongeza Naibu wake Bwana Hassan Chande, Katibu Mkuu pamoja na viongozi wote wa Wizara, wamejitahidi sana. Bajeti ya mwaka huu ni bajeti ya mfano ambayo inakwenda kuwaweka Watanzania katika hali nzuri ya maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka niuelekeze mchango wangu katika Sekta ya Nishati. Nchi imefunguka, Serikali inataka mapato, lakini mpaka leo bado tuna tatizo kubwa sana katika nchi la Nishati ya umeme. Umeme wetu bado haukidhi vigezo au viwango katika uzalishaji ambao unahitajika katika nchi yetu. Kwa mfano, viwanda vingi sasa hivi vinazalisha lakini unapokatika umeme kunakuwa na tatizo, *production* ikisimama, mpaka itakapoanza upya ni hasara kubwa ambayo wanaipata wazalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanalipa umeme bei kubwa sana na matokeo yake wanashindwa kulipa kodi inayopaswa kwa Serikali. Kwa hiyo, naiomba Serikali katika Bajeti ya mwaka huu iangalie sana katika suala zima la nishati ya umeme ili kuboresha viwanda vyetu na hatimaye uzalishaji uweze kufanyika katika kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuipongeza Serikali ni suala la ongezeko la bajeti ya Kilimo. Serikali imefanya jambo kubwa sana, kutoka Shilingi bilioni 294 hadi kufikia Shilingi bilioni 954, siyo padogo! Ongezeko la karibuni Shilingi bilioni 660 ni hatua kubwa mno imepigwa. Naomba Serikali ihakikishe kwamba hii pesa ambayo wametengewa Wizara ya Kilimo, basi yote iende katika Wizara ya Kilimo ili tuweze kuwa na uzalishaji ulio bora wa chakula pamoja na bidhaa nyingine za kilimo ambazo zitakwenda katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza ni suala la Bandari zetu. Kumekuwa na changamoto kubwa sana katika Bandari ya Dar es Salaam ambayo kwa sasa hivi imezidiwa. Ukisafiri kama unakwenda Zanzibar utakuta meli zimejazana kule mbele. Kama kilomita chache kutoka Bandarini pale, meli nyingi mno; zaidi ya meli 25 mpaka 30 utaziona zimetia nanga, zinasubiri kwenye kupakua mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Bandari ya Bagamoyo ambayo kila siku inazungumziwa. Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake aliizungumza katika ukurasa wa 47, namnukuu: "Serikali inaendelea na majadiliano na Wawekezaji watakaowekeza katika eneo maalum la uwekezaji la Bagamoyo, hususan katika miradi ya misingi mitatu; Bandari ya Kisasa *(Modern Sea Port);* sehemu maalum ya kusafirishia na kuhifadhia mizigo *(Logistics Park);* namba tatu, sehemu ya Mji wa Viwanda *(Port Side Industry)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri umuhimu wa hiyo Bandari unajulikana, kama tunakata Serikali iongeze kipato na ipate pesa, basi ichukue hatua za dharura na za makusudi kabisa kuhakikisha hii Bandari inajengwa haraka. Bandari hii itakapojengwa itaipunguzia mzigo Bandari ya Dar es Salaam na

kuiingizia Serikali pesa nyingi za kutosha. Kwani mpaka sasa bado Bandari haifanyi kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika Bandari yangu ya Bagamoyo. Mheshimiwa Waziri, pale kwangu Bagamoyo kuna Bandari. Ile bandari inafanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana, lakini nilikuwa naomba sana hapa Bungeni kwamba pale Bagamoyo imefikia wakati sasa Serikali iangalie uwezekano wa kujenga gati la kupaki zile meli *(boat)* au majahazi yanayokuja kwa ajili ya kushusha mizigo. Bandari hii inaingiza Shilingi bilioni 27 kwa mwaka, Shilingi bilioni mbili kwa mwezi. Hii siyo hela ndogo. Miundombinu ya Bandari ile ya Bagamoyo imechoka, haiko vizuri, sehemu za kupaki meli hakuna. Kwa hiyo, kidogo kunakuwa na changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuangalie kwa undani kabisa jinsi gani tunaweza tukairekebisha miundombinu ya Bandari ile ili iweze kuingiza pesa zaidi. Kwa sababu mpaka sasa sehemu kuba sana ya mapato inakwenda katika sehemu tofauti, yaani kuna mianya ya kutorosha mapato. Kuna bandari bubu nyingi, nyingi kule. Hii ni kwa sababu miundombinu ya pale siyo sahihi. Kama kungekuwa na miundombinu sahihi na tukaweka ulinzi katika sehemu za Bagamoyo, nafikiri Bandari hii ingeweza kutuingizia pesa nyingi. Hii Shilingi bilioni 27 kwa mwaka ingekuwa ime-*double* au ikawa zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa sana niipongeze Serikali kwa kundoa ada katika elimu ya Kidato cha Tano. Kwa kweli Serikali ya Mama Samia naipongeze sana kwa jambo hili, wamefanya kazi kubwa sana na Mwenyezi Mungu atawalipa kwa hili kwa sababu wazazi wengi wamefurahia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nataka kuzungumzia kidogo ni suala la utalii na hasa katika upande wa barabara. Pale

kwangu Bagamoyo kuna barabara ambayo inaenda Pangani, Tanga, inatokea Makurunge. Ile barabara katika uchumi wa nchi ni muhimu sana, kwa sababu Mbuga ya Wanyama ya Saadan, watalii wote wanapita katika ile barabara. Ile barabara ikinyesha mvua kidogo haipitiki, kwa hiyo, ile Mbuga ya Wanyama ya Saadan ina-*cease*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbuga ya Wanyama ya Saadan ni mbuga ambayo watalii wanaipenda. Kwa sababu ni mbuga ambayo unakaa Baharini unamwangalia twiga, unamwangali mnyama yoyote, ukiwa *beach*. Kwa hiyo, ni mbuga ambayo ni ya pekee kabisa. Tatizo kubwa ni miundombinu. Kwa hiyo hii barabara ya kutoka Makurunge kwenda Saadan ikianza kutengenezwa itahamasisha utalii, na hii *Royal Tour* ya Mama Samia, ambayo ameanzisha Rais wetu itakuwa na faida kubwa sana. Kwa hiyo, nawaomba mlizingatie hili, kama tunataka kukusanya mapato, tuangalie sehemu ambazo muhimu zitakazotuingizia mapato haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bagamoyo ina vivutio vingi sana vya utalii. Bagamoyo ni sehemu ambayo ina utalii wa asili, utalii wa bahari. Kwa hiyo, narudi pale pale, itakapotengenezwa gati ya *speed boat* au gati ya kupaki vyombo vya majini, watalii wengi kutoka Zanzibar watakuja Bagamoyo na hivyo Serikali itaongeza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bahati Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Maganga na Mheshimiwa Amandus Chinguile.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Kwanza,

namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaali kunipa uzima na kuweza kusimama mbele ya Bunge letu kuweza kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niendelee kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha kwamba analeta maendeleo katika nchi yetu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha pamoja na timu yao yote kwa kutuletea bajeti hii ambayo imemgusa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi. Pia niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Nitakwenda katika meli yetu ya MV Mwanza Hapa Kazi tu. Meli hii pamoja na changamoto zilizopo, tuwapongeze sana vijana wetu wazawa ambao wameshiriki katika ujenzi wa meli hii. Kwa kweli vijana hawa wamefanya kazi kubwa na ni vijana wa mfano. Naomba tu Serikali itakapomaliza meli hii, basi nao waweze kupatiwa ajira kwa wale ambao wanaweza kufanya kazi katika meli ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niende moja kwa moja katika Sekta ya Kilimo. Naomba nisome kidogo maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza kwamba, Tanzania ni aibu kulia kwa shida ya ngano au mafuta ya kula, kwani tunayo fursa ya kulisha Afrika, Ulaya, Asia katika baadhi ya mazao. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hili. Kama Tanzania kweli tunaweza, na tunaweza kwa kila upande. Hata kule Zanzibar kwa upande wa Pemba sasa hivi tunapata *tender* kubwa sana kwa ndizi zetu za mkono wa tembo au kwa jina jingine mkono mmoja. Hili ni soko kubwa na tunaiomba Serikali wale wakulima waweze kupatiwa mikopo ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni soko kubwa na tunaiomba Serikali wale wakulima waweze kupatiwa mikopo ya uhakika. Vilevile nije katika zao letu la alizeti, niiombe Serikali kupitia Mfuko wa *TASAF* kule Zanzibar, wananchi waweze kuelekezwa juu ya kilimo hiki cha alizeti, bado Zanzibar hatujawa na utaalam wa kulima alizeti. Kipindi ambacho Waziri wa Kilimo wa Tanzania Bara na Waziri wa Kilimo wa Zanzibar watapeana ushauri wa kusaidiana, basi naamini kwamba tatizo hili la mafuta litaondoka Tanzania nzima. Nije moja kwa moja katika sekta ya elimu, tunavyo vyuo vikuu vingi hapa Tanzania Bara, lakini kule Zanzibar tunakosa matawi yake. Tunaiomba Serikali vile vyuo ambavyo kule Zanzibar hatuna matawi yake basi tuweze kupatiwa matawi, ili wale wanafunzi ambao wanahitaji kuomba nafasi zile za kusoma wasipate ule usumbufu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naamini kwamba sekta ya elimu ya vyuo vikuu ni sekta ya Muungano, niiombe tu Serikali kwa upande wa Pemba, tuweze kujengewa chuo kimoja kikuu ili iwe urahisi kwa wananchi ambao wako kule kupata ile elimu. Pia, tutapata fursa nzuri ya watoto wetu ambao wako Mwanza, wako Kigoma kuja kusoma kule Pemba. Hii pia itasaidia na wao kuijua nchi yao lakini pia wataiona kwamba Pemba kweli inanukia marashi ya karafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, wajiandae Mheshimiwa Chinguile, Mheshimiwa Antipas Zeno na Mheshimiwa Turky.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili niweze kuzungumza na wananchi wote pamoja na nyinyi Wabunge wenzangu. Napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu huu muda mfupi wa

dakika 10 nami niweze kushauri na kutoa mawazo yangu katika Bajeti Kuu hii ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza napenda nimpongeze sana Waziri jinsi *proposal* alivyoiweka ya bajeti kuu. Nampongeza Mheshimiwa Rais maana nina imani bajeti hii anaijua kikamilifu Waziri hawezi akaleta tu hivi vitu bila kujua Mkuu wa Nchi. Ninachotaka nishauri hapa yapo mambo mengi ambayo yamezungumziwa humu na nashukuru Mungu kabisa toka tarehe 14 nasikiliza michango ya wenzangu. Sasa naomba niweke mchango wangu tofauti kidogo nisifuatishe kule walikopita wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la asilimia 10 wenzangu wengi wamelisema sipendi nilirudie. Pia lipo suala hili la watu wenye umri wa miaka 18 nashauri hapo Mheshimiwa Waziri ajaribu kuliangalia na ushauri wangu asiliweke kabisa; kwamba kila mtu anapofikisha miaka 18 aingizwe kwenye *TIN Number,* hilo litatuletea *double standard* katika maisha yetu hayatakwenda sawa, nashauri Waziri aliache.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine hapa nikumbushie, mwaka jana nilishauri mambo mengi, mengine yalifanikiwa lakini mengine hayajafanikiwa. Naomba niyagusie yale ya muhimu ninayoyaona mimi. Kuna hawa viongozi wa Serikali za Mitaa, napenda awaweke na wao wawe wanapata posho mbalimbali, ili kusudi shughuli wanazozifanya wazifanye kwa moyo mmoja, Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Wenyeviti wa Vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lingine upande wa *TARURA,* mwaka jana kila Mbunge tulipewa Shilingi milioni 500, mimi nikaweka mawazo yangu kwamba hizi fedha ziende kwenye vifaa vya ujenzi. Mheshimiwa Waziri alinikubalia kwamba watafanya hivyo, lakini baadaye ulitolewa Mwongozo *TARURA* ukikataa hayo mawazo. Naomba kwa kuzingatia kama Waziri

alivyokusudia kubana matumizi, tukiangalia barabara zote zilizochongwa mwaka jana zimenyeshewa na mvua mpaka sasa hivi maeneo mengine hayapitiki, lakini hapa kama halmashauri zingepewa vyombo vya kutengenezea barabara wangeendelea kuchonga na barabara zingeendelea kupitika. Kwa kuwa, tunakwenda kwa *style* ya kubanana, nashauri Waziri wasirudi nyuma, sio mbaya hata watumishi wengine wakiwa wanaambulia *Noah* tu kulingana na hesabu zao za kwenye mishahara katika kuwakopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana ukiangalia hesabu aliyoitaja Mheshimiwa Waziri juzi hapa na nimekaa siku tatu nikaitathmini vizuri nika-*calculate* kweli hizi gari kila mwaka zinakufa. Matengenezo huwa yanakwenda kufanyika *garage* za gharama kubwa lakini sisi wenyewe wengine humu tunamiliki hayo magari. Ukiangalia hesabu wanazotengenezea halmashauri huwa haziendani. Ukiangalia hizi ofisi za manunuzi sana sana ni hasara tupu, ni kuwaingiza hasara wananchi na kushindwa kuwasaidia wananchi kwenye masuala ya msingi. Ukiangalia wananchi wetu kuna kilio kikubwa, tunapitia kwenye kipindi kigumu mwaka huu, nikiangalia hali halisi kwanza kuna dalili ya njaa vyakula vinavyotembea kwenda nje ya Mataifa sidhani kama Serikali itakuwa na *stock* ya kutosha kuwalisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni mwezi wa Juni lakini mchele unauzwa mpaka Sh.2,500 mjini hapa, mwezi wa Julai tuko kwenye msimu. Mahindi yanauzwa mpaka Sh.120,000 Moshi na magari yanatembea usiku na mchana na nikiangalia watu wetu, ni kama vile hawajiandaa kabisa kwamba kunaweza kukachelewa mvua kunyesha maana hizi skimu zinazosemwa zinaweza zisitusaidie. Kwa hiyo, naishauri Serikali iliangalie hilo suala ikiwezekana tufunge mipaka kwanza ili watu wetu wasife kama hatuna *stock* za kutosha. Huo ndiyo ushauri wangu kwa Serikali, waliangalie sana hilo suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka nilizungumzie ni suala la kupoza maisha kwa mwananchi. Mheshimiwa Rais amefanya jambo jema mwezi uliopita Juni, ametoa Shilingi Bilioni 100 ili wananchi waweze kupata unafuu kimaisha, lakini hiyo fursa wananchi wale wa kawaida hawajaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iangalie na lazima tufahamiane kila mtu *rank* yake, Rais ni Amiri Jeshi Mkuu, Rais ni mwanzo mwisho akisema kitu ina maana kinatakiwa kizingatiwe, sio Rais amesema tena halafu tangazo lingine linatoka kwamba nauli hazitashuka bei. Niliona watu wa *SUMATRA,* baada ya kutangaza Rais kwamba natoa bilioni hizi ili maisha yapungue, lakini kuna tangazo lilitoka kwamba nauli hazitashuka. Matokeo yake hizi fedha kama vile zimepotea maana kule Rais alipokuwa amelenga ziende hazijaenda. Kwa hiyo, niishauri Serikali wawe wakali sana katika masuala ya watu wanaojaribu kuleta *disturbance* katika maisha ya watu hao wanaopata shida kwenye hili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuondoa ada kwa kidato cha tano na cha sita, lakini lipo suala moja kwenye shule, michango michango, wanafunzi wamekuwa wakilia sana. Naomba nalo hili Serikali ilitolee ufafanuzi maana kuna hatari unaweza ukaondoa ada lakini michango ikawa mingi, ikawa hakuna ulichokifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine niwaombe Mawaziri, sasa hivi kidogo tunaendana nao, maana tumeshazoeana ni miaka miwili sasa. Zipo ahadi nyingi ambazo wamenipa kwenye Jimbo langu, Mawaziri wale waliofika kwenye Jimbo langu na uzuri walifika kampeni nilishaimaliza, nina imani ahadi walizokuwa wakinipa ni za ukweli kabisa. Hivyo, ni wakati sasa wa kuzitekeleza hizi ahadi, maana mimi sio mtani wao wa kusema kwamba labda walikuwa wanatania au walikuwa wanafurahisha watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine Waziri wa TAMISEMI tumeshaongea na yeye *confidential,* naomba nilirudie tu hapa, Wilaya yangu inakabiliwa na Makaimu, kila Idara imekaimiwa. Mkuu wa Wilaya mwenyewe sasa hivi kuna Kaimu, ukienda *DMO* Kaimu, kila sehemu Kaimu, wilaya yangu inakuwa haihudumii vizuri wananchi wangu, unajua Kaimu ni tofauti na bosi mwenyewe, kibarua ni tofauti na tajiri mwenyewe akikuhudumia, naomba waniangalie kwenye Wilaya yangu. Hata hivyo jamani napambana, *nime-sacrifice* maisha yangu kwa ajili ya hilo Jimbo kutoka Shilingi milioni 700, wilaya ilikuwa haikusanyi lakini mpaka sasa hivi tunakusanya Shilingi Bilioni tatu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha *a-sacrifice* maisha kama alivyolianzisha hili asirudi nyuma, kodi zetu ziko bandarini pale, huku kwingine ni kama vifaranga tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari pale nina wasiwasi, bado kuna vitu vinapenyezwa, hebu wajaribu hata siku moja kuweka Jeshi wiki moja wasimamie Jeshi watoe hawa waliozoea kusimamia, wasikilize tutapata trilioni ngapi? Hii trilioni 41.48 naiona kwanza ni kidogo sana, hakuna haja ya kuongezea tena chanzo kingine, nashauri hivyo. Hivi vyanzo vilivyopo hebu tuvisimamie tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Mtwara ikisimamiwa vizuri na Bandari ya Tanga, bado migodi, miamala, bado tunahangaikia trilioni 41 tu, hakuna hili suala haliwezekani. Nawaomba waliopewa dhamana wasimameni imara ,wengine huwa tunasali hatujui hata siasa kusema kwamba tuongee sijui tujipendekezeje. Nashauri kabisa katika roho na kweli na wala sihitaji kuleta magumashi sijui longolongo ya mara nini, mara nini, Taifa hili tutarudi nyuma. Rais wa Awamu ya Tano alitangaza vita ya uchumi nina imani haijaisha; na wakumbuke wengine walikuwa Mawaziri, wakati tukitangaziwa sisi wengine tulikuwa tunachunga ng'ombe. Ile vita ya uchumi haijaisha inaendelea

mbona wamelala, mbona hatusikii viwanda, kuna vitu vingi vimelalalala, hatusikii Mawaziri wakisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri wanatembelea *V8* na tukimaliza hili Mheshimiwa Mwigulu turudi kwa Mawaziri, hizi gari ziwe zinatumika kwa utaratibu kwa vile tumeamua kubana bajeti. Ikiwezekana kila Waziri akitaka kufanya safari, lazima aangaliwe anakwenda safari gani, anatumia mafuta gani, hapo ndio tutakuwa na usawa ili na wanyonge nao wapate haki yao, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, hiyo ni kengele ya pili lakini endelea kusimama. Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Maganga tulimtangaza kuwa ni mchezaji bora katika mechi zilizopita. Kwa bahati mbaya *tv* ilikuwa haiku-*zoom* kwake na alipata unyonge. Sasa leo nampa nafasi *tv* zi-*zoom* kwake ili jimboni kwake wamuone, ndio amekuwa mchezaji bora kwenye mechi... *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana au umeniongezea na dakika kidogo niongezee katika mchango wangu?

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini. Mheshimiwa Amandus Julius, atafuatiwa na Mheshimiwa Antipas na jiandae Mheshimiwa Turky.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nizungumze kidogo kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali. Awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya, kwa kweli Watanzania wanaona. Hata wale ambao wanasema hawaoni basi moyoni wanajua na wanakiri kwamba Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan anaupiga mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye barabara. Iko barabara ya Nachingwea – Masasi, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umefanyika na umekamilika zaidi ya miaka tisa iliyopita, lakini imetengewa fedha zaidi ya miaka mitano mfululizo lakini haijapelekwa hata senti moja. Kwenye hotuba ya bajeti ya Waziri wa Kisekta aliizungumzia hii barabara ya Masasi – Nachingwea kwamba iko kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alielezea ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya kutoka Nachingwea kuelekea Liwale. Sasa wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasoma hii Bajeti Kuu sijasikia. Sasa nikawa napitia kishikwambi changu nikasema labda hii *page* imeruka au namna gani? Tukiwa tunaomba hizi barabara, tunaomba kutufungua ili na sisi kimaendeleo tuwe sawasawa na maeneo mengine, hali huko ni ngumu. Ukizungumzia barabara ya kutoka Masasi – Nachingwea, Nachingwea – Liwale, Liwale - Nangurukuru, Nachingwea kuelekea Ruangwa wakati wa masika huwezi kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia hapa nilikuwa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tulikaa mahali tumesimama zaidi ya masaa mawili, hiyo barabara ni mbovu. Sasa sijui tumekosea wapi na kwenye hili nimwombe sana kaka yangu Dkt. Mwigulu Nchemba atakapokuja kuhitimisha, wananchi wale wa Masasi, Nachingwea, Ruangwa na Liwale wanataka kusikia barabara hii mpango wa kujenga ukoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Ujenzi ametupa matumaini makubwa, lakini sasa kwa hotuba hii sielewi kama atakuja kuhitimisha mwishoni au la lakini kwa kweli wanasubiri kusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke hapo nijielekeze kwenye kilimo. Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutupatia

pembejeo za kilimo na hasa kwenye zao la korosho, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Kwenye hili naomba nishauri eneo moja, tuna changamoto ya upatikanaji wa hiyo *Sulphur*. Makisio ya mwaka huu ni kupata tani 25,000, lakini mpaka sasa imepelekwa tani 10,000, tayari msimu unakwenda. Maana yake hapa wakulima watapata pembejeo wakati muda wa kuzitumia umeshapita, sasa eneo hili nishauri sana Serikali kwa sasa tunatumia vyama vikuu vya ushirika kununua hizi pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe jukumu hili tuwape Bodi ya Korosho Tanzania, kwanza ni chombo cha Serikali, lakini pia tunaweza tukazipa taasisi zingine za Kiserikali na hii itatusaidia hata wakati wa kufanya *auditing*. Natambua Wizara ya Kilimo inafanya kazi nzuri basi na lenyewe walichukue ili waweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo suala la tembo. Nilisimama mbele ya Bunge lako Tukufu, nikalia sana, nikalalamika sana juu ya kadhia ya tembo na nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Sekta ya Maliasili na Utalii, tunawashukuru sana, jambo lile wamelifanyia kazi na kazi inaendelea. Tunajua kwamba changamoto haijaisha na naamini kwamba bado wataendelea kutuondolea kero hii ili wananchi wangu wa Jimbo langu la Nachingwea waweze kuishi kwa raha kama maeneo mengine. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo juu ya asilimia 10. Wakati inatengwa ile asilimia 4:4:2, ziko halmashauri zingine mapato yake ni kidogo sana, hayatoshelezi. Sasa leo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasema twende tukaondoe asilimia tano…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kuna taarifa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kuwa nitakuwa na muda wa kujumuisha, lakini nimehofia nisije hoja zikawa nyingi nikasahau jambo hili. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge makini kabisa anayeongea kwamba hii barabara anayoitaja ni kweli ni *omission,* tuliisahau kuiorodhesha, kwa hiyo iingie kwenye kumbukumbu za *Hansard* kwamba na yenyewe ni sehemu ya zile barabara zilizowekwa kwenye ule mpango ambao Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi aliusema. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa hiyo.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, iingie kwenye kumbukumbu kama ilivyotajwa kwenye Wizara ya Kisekta, imo kwenye utaratibu ule ule na wananchi wote na Wabunge wote wa Kusini waipate hivyo kama ambavyo ilisomeka kwenye Wizara ya Kisekta. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa umeipokea?

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naendelea na mchango wangu kwenye asilimia 10, bado mahitaji ya watu wetu kwenye haya matumizi ya asilimia 10 ni makubwa kuliko hata hiyo asilimia 10 inayopatikana. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali bado hii asilimia 10 kwa maana ya 4:4:2 tuiache, badala yake sasa tutafute vyanzo vingine ambavyo tutakwenda sasa kuwahudumia wale wamachinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba hizi fedha pia na hao wamachinga ni sehemu ya wale vijana ambao wanakopa, ni sehemu ya wale akinamama ambao wanakopa. Hilo naomba lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba, kipo Chuo cha Ualimu Nachingwea, ni chuo kikongwe na cha muda mrefu sana. Tulizungumzia hapa juu ya kuiomba Serikali ione uwezekano wa kukipandisha kile chuo kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo hiki ni kikubwa, chuo hiki kina eneo, lakini pia Nachingwea ni tajiri kwa maeneo, tunayo maeneo mengi ya kutosha, wakiwa tayari tutawapa maeneo ya kutosha kabisa. Chuo hiki kinabeba wanafunzi kutoka kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kwa hiyo, wakitupatia, hii ni fursa kwa uchumi wa Nachingwea, lakini pia tutakuwa tunasogeza elimu zaidi kwenye maeneo ambayo vijana wanatoka huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya furaha ya kusikia lile jambo la barabara, nisije nikaondoa utamu huu, hapa tayari nimeshaanza kupokea *message* za kupongeza. Nikushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antipas Zeno, jiandae Mheshimiwa Turky.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Nina masuala kadhaa hapa ya kuchangia, kwanza ni migogoro ya ardhi baina yetu wananchi wa Bonde la Kilombero na Wizara, lakini suala la biashara ya viumbepori hai ambayo imesitishwa, suala la kutaka Jeshi la Uhifadhi li-*retain*

mapato yake, pia ukamilifu wa Jeshi la Uhifadhi na mwisho masuala ya wastaafu kama muda utaniruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukrani kwa Serikali, hasa kwa Mheshimiwa Rais kwa kuunganisha barabara yetu ya Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma kwa lami ambapo kwa sasa haipitiki. Tumetajwa kwenye mpango kupitia Mpango wa *EPC + F*. Natoa shukrani sana kwa hilo kwa niaba ya wenzangu wa Ruvuma na wa Malinyi, pia kuna suala la vifo vya wananchi na usumbufu kwenye mazao kutokana na tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipiga kelele na mwezi huu nadhani mlisikia wananchi watatu wa Malinyi walipoteza maisha kutokana na ajali ya tembo, lakini bahati nzuri Wizara imeridhia wametuweka kwenye mpango tutapata kituo cha kudumu cha Askari Wanyamapori kule Kilosa kwa Mpepo. Kwa hiyo, kwa hayo natoa shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mhifadhi Mstaafu. Nimehudumu Wizara ya Maliasili na Utalii miaka kadhaa, nikahudumu katika Jeshi la Uhifadhi kama Afisa Askari miaka kadhaa, katika maisha yangu yote niliapa kwamba, sitakubali kushiriki kuharibu uhifadhi kwa sababu ya umashuhuri wa kisiasa, huu ndiyo msimamo wangu mpaka sasa hivi. Tofauti napishana na wenzangu jambo dogo tu, kwa maana ya wahifadhi wenzangu wa maliasili na wale mabwana Waheshimiwa Mawaziri Nane ambao walikuwa *assigned* ku-*solve* migogoro ya nchi hii. Shida yao kubwa ninayopishana nao ni *approach,* namna gani wana-enenda katika suala la ku-*solve* migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu katika Bonde la Kilombero kwa maana ya Wilaya ya Malinyi na majirani Mlimba, Ulanga na Kilombero tuna migogoro na Wizara kwa namna mbili. Kwanza kuna Kijiji kinaitwa Ngombo kule kwangu Malinyi, wananchi wanaishi pale tangu mwaka 1935, thelathini na kitu mpaka leo,

lakini pia lile bonde limekuwa hifadhi mwaka 1952, iliwekwa *GN*. 107 na wakoloni tangu kipindi kile mpaka leo Wizara ime-*maintain.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuna tatizo. Nafahamu kulingana na uhifadhi eneo lolote likionekana ni nyeti kuna haja ya kuhifadhiwa, Serikali inaamua inafuata utaratibu na inakuwa hifadhi. Kama kuna wananchi, wanapisha, ndiyo utaratibu. Kwa hiyo, nilitarajia watu wa maliasili na Mawaziri Nane walipaswa kusema tunatambua Kijiji cha Ngombo ambacho kimesajiliwa na Serikali, wananchi wanaishi miaka hiyo kabla hata uhifadhi pale kuanza. Tunafikiria kuna haja ya watu kutolewa kwa sababu ya mradi wetu wa *Stigler's Gorge* na vitu vya namna hiyo kama kuna haja. Wangetusikiliza, tusikilizane nao, pengine tusingeweza kubisha. Watu wa maliasili mara zote wamekuwa wakiimba hata wakijibu maswali yangu hapa walikuwa wanasema wananchi wamevamia kule Ngombo, wamefanya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nawauliza walivamia mwaka gani? Ukisema umevamia lazima uwe *specific* utaje mwaka gani wamevamia? Hawakuweza kutaja na mpaka kesho hawataweza kwa sababu wananchi wameanza kuishi kabla ya uhifadhi. Kwa hiyo, sisi hatuna shida sana na hilo, nilikuwa nasema suala la *approach.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana Mawaziri Nane wamekuwa *assigned,* wakati tunawasubiri wao wafanye maamuzi ya mwisho kuhusu Kijiji chetu cha Ngombo, wananchi waendelee na Maisha, watakapoamua tutachukua kile ambacho Serikali itasema, lakini mpaka sasa maamuzi hayajatoka, wananchi kule tunalima kwa kubahatisha, Askari Wanyamapori wa *TAWA* kila mara wamekuwa wakiingia kufanya doria. Watu wanaishi kuna nyumba, kuna shule, kuna kila kitu, tunaendelea kuishi mpaka leo, wananchi zaidi ya Elfu Nne.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa ambaye amemaliza kuzungumza sasa kwamba, ni kweli kuna Kamati ya Mawazi Nane ambao wamezunguka, lakini Kijiji cha Ngombo hakiko kwenye hifadhi ambayo watumishi wa *TAWA* wanasimamia mapori. Pori ambalo linasimamiwa na watumishi wa *TAWA* ni Pori la Kilombero. Kijiji cha Ngombo kiko mbali kidogo na Pori la Kilombero. Kwa hiyo, haya maamuzi siyo kwamba ni ya uhifadhi wa maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa tu mzungumzaji kwamba, maamuzi ya Baraza la Mawaziri hayakuangalia pori hili kwamba linasimamiwa na watu wa Maliasili, isipokuwa vyanzo vya maji viliangaliwa kwenye eneo ambalo ni kijiko au bakuli ambalo eneo hilo Kijiji cha Ngombo kiko ndani yake. Tuliangalia hilo kwamba, eneo hili ni mahsusi kwa ajili ya mchango mkubwa wa maji ambayo yanatiririka kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antipas.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri Mary Masanja ninaheshimiana nae, ninajisikia vibaya kumsema vibaya kwa hiyo, ninamsitiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kijiji cha Ngombo hata ukichukua ramani mpaka leo wanakijadili kwenye Pori Tengefu la Kilombero kipo katikati ndiyo ukweli wake, kipo katikati. Kama hafahamu, nadhani anafahamu, wanaruka na ndege mara

nyingi kipo katikati, aidha hakumbuki au pengine hafahamu au anajisahaulisha, sitaki kumsema vibaya. Namsitiri, naomba nisizungumze juu ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliomba na mimi niliomba Kijiji chetu cha Ngombo kulingana na unyeti wake kama kinataka kitolewe *it is ok,* pengine tunaweza tukaridhia, niliomba tupunguze hata ukubwa wa Kijiji tuko radhi tubki eneo letu la asili dogo, watu waendelee kuishi, watu wanaishi pale miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamfahamu Waziri Juma Ngasongwa kazaliwa mwaka 1941 katika Kijiji cha Ngombo, kasoma shule ya msingi pale Ngombo, Shule ya Msingi ipo kabla ya mwaka 1950, wao wanasema wananchi tumevamia! Mzee wangu Mzee Zeno Mgungusi Mhifadhi, kazaliwa Ngombo, kasoma shule ya msingi pale kabla ya uhifadhi. Hawa wanaendelea kusema tumevamia, siyo sahihi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niliomba, sibishani na Serikali, nimeomba tuko radhi kupunguza ukubwa wa Kijiji sehemu nyingine iwe hifadhi, sehemu ndogo ibaki tuendelee kuishi. Kama mnafahamu kabila linaitwa Wandamba akina sisi, akina Joti, akina Ngasongwa, akina Beno Ndulu wote asili yatu ni Ngombo. Tuko radhi tupunguze ukubwa wa Kijiji libaki eneo dogo tuweze kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema tusifanye kilimo kikubwa cha matrekta na kadhalika tuko radhi, nilisema …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antipasi lakini bila maji vilevile hamtaweza kuishi.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naam.

**NAIBU SPIKA:** Bila maji hamtaweza kuishi. Maji alikuwa anazungumzia Mheshimiwa Waziri hifadhi, bila maji hamtaweza kuishi. Wewe endelea na mchango.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa, ninalifahamu hilo ndiyo maana nimetoa mapendekezo. Tulikuwa tunaomba tuko radhi kupunguza idadi ya mifugo hata kwa asilimia 90, tupunguze ukubwa wa Kijiji hata kwa asilimia ngapi, nilitoa maombi nilikuwa natarajia Serikali ikubali, lakini hata kama ikikataa sina tatizo, basi wafanye maamuzi kwa wakati. Kama wanasema hatusikilizi mawazo ya Mbunge tunataka watu watoe *it is ok,* waseme hata kesho, mimi kama Mbunge nitatoa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wanashindwa kuamua kila siku tunaviziana, tunaviziana. Mpaka sasa hivi ninavyokuambia watu wamekamatwa kule wananyang'anywa mchele, wananyang'anywa mpunga, watu wanaishi mpaka leo. Toeni tamko kwamba watu waondoke, tunaondoka, sasa hamsemi. Kila siku mnasema Mawaziri Nane wanakuja kesho, Bunge lijalo, kesho, Mimi Mbunge nifanye nini? Tukisema mtaanza kusema Mbunge mkorofi anaonea Serikali, sasa mimi nitakuwa Mbunge wa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa iwe *serious,* wafanye maamuzi, kama mnataka mtutoe basi isemwe hata kesho, mimi kama Mbunge sitabisha, nitawaambia watu wangu, tutatoa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili mgogoro huo ni mpaka. Kuna mpaka wa mwaka 2012 wa hilo Bonde la Kilombero lote, Majimbo Manne ya uchaguzi. Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori *(TAWIRI)* ilisema ili bonde liwe salama mpaka ukae hapa na tukaweka mpaka 2012. Wananchi tumeshirikishwa, tumeridhia, hatuna shida, lakini 2017 ukaja mpaka mwingine kuja

kuchomekwa, wamekuja watu wa maliasili wameweka *beacon* mpaka ambao mpaka leo hauna *GN,* lakini mpaka leo kuna watu wamewakamata wamepewa kesi za uhujumu uchumi, wapo ndani ya hifadhi, lakini kwenye mpaka ambao hauna *GN*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nalo mimi silibishii, wakisema na huko tuache kulima tutaacha, nitawaambia watu wangu, lakini Serikali watamke wanapochelewa kufanya maamuzi maana yake wanatuweka sisi kwenye wakati mgumu. Mnataka sisi tunyamaze, sasa mimi nitakuwa Mbunge wa namna gani? Tukisema mnasema tunaionea Serikali, mnataka tufanyeje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siasa zetu zinakuwa ngumu, wenzetu Mawaziri Nane watusaidie. Ninajua muda mwingine tunagombana na watu wa maliasili, watu wa *TAWA, TANAPA,* wanaonewa, lakini nadhani asilimia kubwa ni wale Mawaziri Nane ndiyo tatizo. Huu ni mwaka wa Sita tangu Tume imeundwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kituko kingine hawa Mawaziri Nane hawajawahi kukanyaga Malinyi, hawajawahi kufika hata pale Mlimba, wanaruka na ndege tu juu Kilombero wanaondoka, hawajawahi kufika, lakini pamoja na hayo mimi sijali sana, fanyeni maamuzi sitabisha. Msitutafutie lawama tuonekane wajeuri naomba mfanye maamuzi tutazingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, suala la pili ni suala la Mheshimiwa Waziri wa Fedha anahangaika kutafuta vyanzo vipya vya mapato fedha zipo Maliasili. Kuna biashara ya viumbehai pori kwa maana ya wadudu, kusafirisha wadudu nje ya nchi, hawa panzi mnawajua, kumbikumbi, sijui vinyongana kadhalika. Biashara hii ilikuwa inafanyika tangu uhuru Mwalimu Nyerere anaifahamu, walikuwa wanafanya Wazungu, badaye Shirika la *TAWICO* likapewa kazi ya kusafirisha wadudu nje ya

nchi. Mwalimu Nyerere akazuia akasema wazawa wafanye hii kazi mwaka 1967 mpaka leo Watanzania walikuwa wanafanya biashara ya kukamata wadudu wanapeleka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii ilizuia mwaka 2016, Machi 2017, Waziri Maghembe alitoa sitisho hawa wadudu wasipelekwe nje ya nchi tena, nadhani ilikuwa kwa miaka mitatu, lakini mpaka leo mwaka wa sita, wale wafanyabiashara walishalipia kila kitu, wamelipa leseni, wamelipa kodi, wametumia gharama zote, tangazo limetolewa ghafla la kusitisha na tangazo lenyewe nadhani halikuwa kisheria, wale wafanyabiashara wamepata hasara zaidi ya Bilioni 1.6 Serikali haijawarejeshea.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wakisema waende hata Mahakamani ni kesi nyepesi, mnaitia hasara Serikali, kwa nini? Wanasheria huko maliasili wapo, mnashindwaje kuishauri Serikali ama wawalipe fidia, lakini wenyewe wanazungumza hawana haja sana ya fidia wanachotaka wafungue biashara iendelee?

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine najua kuna hofu, wengine wanasema wadudu wetu wanasafirishwa nje ya nchi, kule Wazungu watawazalisha watakuwa wengi, wakiwa wengi wadudu Wazungu hawatakuja kutalii Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa wale wadudu hawakamatwi hifadhini wanakamatwa mitaani, pili mnafahamu Wizara ya Kilimo inatenga bajeti, dawa ya kuuwa wadudu…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo. Malizia sekunde kumi, ahsante.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, aah, umeniongezea.

**NAIBU SPIKA:** Eeh, sekunde kumi.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, hawa wadudu bajeti wanatenga Wizara ya Kilimo kuua ndege kweleakwelea, kuuwa viwavidudu, wale sijui viwavi jeshi na kadhalika, ambao wanaathiri mashamba ya watu. Wale wadudu ni *deal* watu wanawahitaji, wanakamatwa mtaani wanapelekwa nje tunapata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hatupati fedha, tunatumia fedha kuwauwa wadudu ambao wanatakiwa kule Ulaya, kama kulikuwa na kutokuwa na uadilifu kwa wafanyabiashara au watendaji haipaswi kuwa kisingizio. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ifungulie biashara ya viumbepori hai tuweze kupata fedha za kigeni tupate mapato. *(Makofi)*

**NAIBUU SSPIKA:** Haya ahsante, mengine andika. Tunaendelea na Mheshimiwa Turky.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mwaka uliopita Rais wa *African Development Bank* alihutubia akasema kuwa, katika jambo rasilimali ambayo itakuja kuwa ghali basi itakuwa ni chakula. Tumeshafika asilimia, sasa hivi nimetizama dunia inapoelekea inaenda katika *exhaustion* na ukitizama watu tumeshazidi Milioni Saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kupitia kwa Mama yetu Rais mpendwa kuona uono huo na kuja na mapinduzi makubwa sana ya kilimo Tanzania. Ukitizama katika historia ya Tanzania basi hii tumeupiga tena tumeupiga mwingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kumshukuru sana Waziri husika kuja na taswira tofauti, kuna kitu kinaitwa *agriculture* na *agro-business. Agriculture* tunaenda katika tamaduni, lakini

safari hii tukasema hatutaki kilimo cha utamaduni, tunataka kilimo cha biashara. Kwa hivyo, nampongeza sana Waziri Bashe kuja na mfumo mpya. Pia lazima nimshukuru Bwana Mzee wa Mayele kuhakikisha katenga bajeti. Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu pale akasema aah! safari hii nitachumba huku, nitachumba huku, uono wa Mama hii *agro-business* na tunapoelekea dunia inayohitajika kilimo kuweza kupatikana kwa hivyo, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani jana nilipata fursa ya kuonana na wanafunzi kutoka *UDOM,* wanamaliza *research* zao na tulikuwa tunabadilishana mawazo tu, wakawa wanazungumza kuna mmoja kamaliza uchumi, ananiambia Mheshimiwa tunamaliza sisi uchumi tayari, sasa a tunataka kuja huko utusaidie tutafanikiwa vipi? Tutapata fursa gani katika biashara au katika ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwambia sasa wewe umekuwa mchumi, sisi kawaida yetu kule watu wenzetu wanapomaliza vyuo wanakuwa wameshakuwa wachumi wanakuja na maarifa. Sasa hebu nikuulize mwenzangu, wewe sasa hivi umeshakuwa mchumi, unaona katika hali halisi sasa hivi ya nchi yetu, kitu gani kinaweza kutusaidia sisi katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kanambia mambo mengi tu. Nikamwambia mambo mengi gani, niambie? Akaniambia unajua kama sera zetu. Sera kama zipi? Akasema unajua kuna sera nyingine haziko sawa, lakini ukienda huku, vipi, tunaweza tukaziweka sawa. Kama zipi? Akawa hakamati sehemu. Nikamwambia inawezekana tuambie pengine tuambie *Fiscal Policy, Investment Policy* au *Policy* ya aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukitizama akawa ameganda. Baada ya hapo tukaitizama sasa tulilokuwa tunaongelea suala zima la hapa tunapozungumzia kabla ya hapa katika michango

yangu ya kabla kuwa, wanafunzi wengi tunamaliza *University,* lakini wanakuwa hawana mchango katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mama juzi karibuni kati hapa alikuja Zanzibar katika *organization* ya *MIF, (*Mwanamke *Initiative Foundation),* akawa anaongelea suala zima la kubadilisha *curriculum.* Namshukuru sana Mama kwa kuja na uono wa kuona sasa elimu yetu nafikiri umefika wakati wa kuja na mageuzi na hilo ni muhimu sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekaa na vijana wanamaliza, wenzetu mataifa mengine wanatumia fursa hizi wanakuwa wanakaa na makampuni. Wanaenda katika *Universities* wanafanya *interview* kwa sababu tunajua umuhimu wao kuwa sasahivi tunawahitaji wao wanakuja na maarifa mapya, lakini wanafunzi wetu bado wanategemea maarifa yaleyale yaliyopita na siyo maarifa mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia huko wakaja pia wakaniambia kabisa sisi bwana Walimu wetu wanatuambia, ukitaka kufaulu au kuendelea kimaisha lazima unatakiwa mtu akukamate mkono uwe nae hivi ndiyo maisha utapiga, lakini siyo kwa elimu yetu tuliyo nayo. Hao ni Maprofesa wetu wanaongea lugha hizo, sasa hawa wanafunzi wetu watakuwa na dira gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani watu wengi sana pengine au mtakuwa mnajua, hamfahamu, lakini tajiri wa dunia wa sasa hivi anaitwa Elon Mask, watu wengi labda wanaweza wakafikiri kuwa huyu ni Mmarekani, lakini huyu ni mwana Afrika, kazaliwa Pretoria, South Africa. Kuna wakati mmoja akaulizwa kwa nini ulitoka zako Afrika unaendazako Marekani? Akasema unanua mimi nilitengeneza *instrument* ya kulipa inaitwa *PayPal,* alianzisha yeye na mwenzake, lakini baada ya hapo wakaiuza, baada ya hapo akaenda zake Marakeni. Akaulizwa kwa nini ulienda zako

Marekani? Akasema nimeona Afrika hakuna mtu anaewekeza katika ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afrika tunabonyezwa tunabakia huku, nimekuja Marekani nikasema mimi nataka nianzishe gari lisilokuwa na dereva, nitaanzisha *battery* ambayo haitaki mafuta haitaki chochote itakuwa inafanya kazi. Afrika hakuna mtu kanisikiliza. Nimeenda Marekani watu wamenisikiliza na leo ile kampuni inaitwa *Tesla* ni namba moja duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukitizama jamani duniani kwetu huku Afrika, imekuwa ni jambo la ajabu sana kwamba hatutaki kuwekeza katika suala zima la ndoto ya *research*. Katika Bara linaloongoza sasa hivi kwa kukua katika masuala ya teknolojia ni *South Korea.* Waliulizwa ilikuwaje wewe ghafla umekua kwa haraka katika Bara hili la Asia? Akasema tumetenga asilimia Nne ya *GDP* yetu katika *research and development,* na leo wao ni viongozi katika masuala yote ya *electronics. Samsung* sasa hivi anaendana pamoja na *iPhone* na kampuni nyingine kubwa, Hyundai, ana kampuni nyingi sana, anashindana na Japan. Leo tujiulize tumewekeza kiwango gani katika *research and development? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo watu wanafanya *research, Oxford* wamefanya *research, Universities* zinafanya *research,* Imetoka AstraZeneca ndiyo imekuwa *vaccine* ya *COVID-19*. Tujiulize *Universities* zetu *research* zao zinasaidia nini katika uchumi wa Taifa? Jibu litakuwa hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Serikali ilitazame suala zima la *research and development* kwani kama tunataka tuendelee katika dunia hiyo, tusibakie katika ndoto tu, basi lazima tuende na wenzetu katika masuala ya *research and development. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, jana walikuja wenye viwanda wanaotengeneza *biscuit, biscuit* viwanda wazalendo wamezidishiwa 500 *shillings* kwa kilo *as excise duty*. Wanasema sisi tuna viwanda sote tunafahamu sasa hivi mfumuko wa bei viwanda vinatumia unga, unga wenyewe kupatikana taabu, bei zimepanda, leo tunakuja tunaambiwa tulipe 500 *Shillings per* kilo *as excise duty* na wakati watu wa *importation* hali iko vilevile, sasa hapa tutaishi vipi? Sasa nilikuwa naomba sana kupitia Waziri, Wizara ya Fedha, walitazame hili suala na nyakati zilivyo. Nafahamu tunatafuta mapato ya tofauti katika sehemu na nyanja tofauti, lakini hii *biscuit* tuitizame wanakula akina nani? Ni watoto wetu wa shule kwenye vishughuli hivyo vya madarasani na sehemu nyingine, kwa hivyo, nilikuwa naomba sana katika sehemu hizi….

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Turky, mengine andika.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga hoja kwa asilimia zote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha haya ni pamoja na mchango wa Mheshimiwa Mkenge wa bidhaa zinachelewa kushushwa bandarini kutokana na msongamano wa meli, msongamano wa meli unatokana na *agency* ambayo ndio ina-*clear* hii mizigo, Serikali imeshasema kuwa hamfanyi biashara lakini bado taasisi yenu ya *TASAC* inaendelea kufanya biashara.

Mheshimiwa Waziri, ngano hii inatoka nje, ikichelewa kuna *congestion fee, congestion fee* analipa mlaji, gharama zinazidi kupanda kwa wananchi kutokana na kulipia foleni za meli kwa sababu ya kutokuziingiza hizi meli mapema. Ninakuomba tu, tulitegemea labda kwenye *Finance Bill* hii mngeweka kuwatoa *TASAC* kutokufanya biashara, lakini naona bado haipo. Hebu una lolote la kusema? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Ninakuomba wewe pamoja na Bunge lako tukufu mridhie tulichukue jambo hilo ili tuweze kukamilisha na wenzetu Wizara ya Kisekta pamoja na Kamati halafu tutoe taarifa kwa sababu bado tuna fursa ya kutoa taarifa kuhusu haya masuala. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa michango. Wachangiaji wote wamekwisha na muda wetu umekwisha. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis, Tarehe 23 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*

# 22 JUNI, 2022